ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**

19.	**Mhe.**	**Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe.**	**Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe.**	**Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe.**	**Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe.**	**Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe.**	**Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe.**	**Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe.**	**Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe.**	**Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe.**	**Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe.**	**Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe.**	**Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Saba – Tarehe 17 Mei, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2018/2019.

Mhe. Suleiman Makame Ali (Kny) Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mhe. Naibu Spika, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani (Kny) Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirikia na Umma (*PAC*) kwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti Mkuu. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 49

Ukosefu wa Upatikanaji wa Huduma ya Utoaji Vyeti vya Vizazi na Vifo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny) Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:

Tunaipongeza sana serikali kwa kuanzisha mfumo mpya wa usajili wa vyeti vya kuzaliwa pamoja na kifo hapa Zanzibar.

(a) Kwa nini, mfumo huo umeshindwa kufanya kazi ipasavyo na hatimae kupelekea kutopatikana kwa huduma hiyo takriban miezi minne sasa.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo, ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa kuja na kurudi bila ya huduma yoyote kupatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ilianza kutumia mfumo wa kielektroniki katika kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kuanzia mwezi wa Aprili, 2016. Mfumo huo ulianza kufanya kazi kwa majaribio katika Wilaya tatu za Mkoa wa Mjini Magharibi ambazo ni: Wilaya ya Magharibi 'A', Wilaya ya Magharibi 'B' na Wilaya ya Mjini.

Mhe. Naibu Spika, mnamo mwezi wa Oktoba, 2017 mfumo huu ulipata hitilafu za kiufundi na kushindwa kufanya kazi. Hata hivyo, huduma za usajili na utoaji wa vyeti ziliendelea kutolewa kama kawaida kwa utaratibu wa *manual* ambao ndio uliokuwa ukitumika kabla, jambo ambalo ndilo lililopelekea kupungua kwa kasi ya kiutendaji kwa kiasi fulani.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, kwa vile mfumo huo ulianza kwa majaribio hivi sasa ofisi kwa kupitia wataalamu wake wa TEHAMA wameweza kuugundua tatizo lililosababisha kusita kufanya kazi kwa mfumo huo na wapo katika hatua za mwisho katika kuufanyia marekebisho ambapo unatarajiwa kuanza kufanyakazi tena hivi karibuni. Aidha, kwa hivi sasa ofisi ipo katika mpango madhubuti wa kutanua mara baada ya kumalizika kazi ya kusambaza mkonga wa mawasiliano katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Mhe. Naibu Spika kazi hiyo ambayo pia inatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimwambie tu anieleze jana darsa tulolipa kwa Mhe. Waziri au bosi wake, serikali haitaki kuona wananchi wake wananyanyaswa, lakini ni mdomo tu vitendo havipo, ndio binadamu siku zote unatakiwa maneno mengine usimalize uweke hakiba. Swali langu.

(a) Je, mfumo huu ulokuwepo wa hivi sasa na huo unokuja mpya, bado wananchi wanaendelea kuteseka na kunyanyasika na rudia tena huu mfumo ulokuwepo wa zamani *manual* na huu mpya ulokuwepo bado wananchi wanaendelea kunyanyasika wanafanya mazoezi bila ya kutaka ngazi na kushuka. Je, mtachukuwa utaratibu gani wa haraka kumaliza tatizo hili na ukizingatia ni haki yao ya msingi.

(b) Ni sababu gani za msingi zinazopelekea mtu kutoka Mahonda au Makunduchi kuja kufata cheti chake na kwenda kukaa foleni Benki ya *BPZ* kuteseka kutwa nzima kwa shilingi 2,000/=, hamjawa tayari kutafuta *formula* nyengine msiseme tu kwa mdogo serikali hii haitaki kunyanyasa wananchi, kumbe ndio wizara yenyewe ya mwanzo inayonyanyasa wananchi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kwanza nataka afute kauli yake, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hainyanyasi wananchi na kama anaushahidi basi autoe ndani ya Baraza hili kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inanyanyasa wananchi.

Lakini katika kujibu swali lake utaratibu wa kutoa vyeti vya kuzaliwa na *certificate* nyingene zote za matukio ya kijamii zipo kwa mujibu wa sheria, utaratibu wa kuzitoa zinaendana na mfumo. Kwa kweli, mfumo wa mwanzo ulikuwa *manual* wa njia ya kutumia *typewriter* katika maeneo ya meneo ya wilaya nyengine zote ukiacha wilaya za Mkowa wa Mjini Magharibi, mfumo huu ulianza na ulianza kwa mafanikio makubwa sana.

Hata hivyo, binadamu Mwenyezi Mungu katuumbia uhai lakini katuumbia pia maradhi kama ilichoumbwa na Mwenyezi Mungu kinaweza kikapata athari seuze kile kinachotengenezwa na binaadamu kwa nini kisipate uharibifu. Mhe. Naibu Spika, kilichosababisha mufumo huu kusita ni kwamba *saver* yetu iliharibika, serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya kurekebisha *saver* hiyo, ili wananchi waweze kupata huduma kama ilivyokusudiwa. Sasa anapokuja Mhe. Mwakilishi akasema kwamba serikali inanyanyasa wananchi Mhe. Naibu Spika, hili naomba niliache kwako lakini lazima Mhe. Mwakilishi afute kauli yake kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inanyanyasa wananchi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum umemtaka Mhe. Jaku Hashim Ayoub afute kauli yake ya kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inanyanyasa wananchi wake. Nafikiri Mhe. Jaku Hashim Ayoub amesikia na sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub ufute kauli yako, kwa hiyo nakuomba ufute kauli yako.

Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kwa hoja na kanuni nilichozungumza ni Kiswahili wala si Kihindi wala Kizungu. Je, nikishakumpa ushahidi atakuwa tayari kujiuzulu huo uwaziri tukubaliane hapa tujenge hoja, atakuwa tayari kujiuzuru.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hiyo kauli haikuwa nzuri umenifahamu, na unachotakiwa ufute au ubadilishe, lakini huwezi kusema kwamba hili ni kwako wewe ni sawa sio kauli nzuri, futa au badilisha kauli.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nilichosema mimi serikali kazungumza jana haitaki kuona wananchi wake wananyanyasika kauli yake kaitowa mwenyewe jana hata masaa 24 hayajafika sasa tuthibitishe tu.

Mhe. Naibu Spika: Sawa Mhe. Mjumbe, kama ni hivyo basi Mhe. Waziri ametaka uthibitishe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nikishakuthibitisha hatua gani itakayofuata kwake yeye.

Mhe. Naibu Spika: Aaa! Wewe si umesema hivyo sasa thibitisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sasa sheria isiwe upande mmoja Mhe. Naibu Spika Manispaa ...

Mhe. Naibu Spika: Sasa basi Mhe. Jaku Hashim Ayoub usitupotezee muda.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ngoja nithibitishe sasa jana hata msaa 24 hayajafika soko la Mombasa watu wanakwenda *rain boot* kakiri suala hilo, lakini bado usumbufu upo, ufungaji wa magari kiholela kwa ubaguzi na ushahidi ninao baada ya maswali na majibu nitamletea ushahidi aje aone kwamba nyengine hazifungwi nyengine zinafungwa baada ya majibu nitamwita mtu hapa aje athibitishe kwake.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, futa kauli, Mhe. Jaku Hashim Ayoub nakutaka nasema mara ya tatu futa kauli. Mhe. Jaku Hashim Ayoub toka nje.

(Hapa Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitolewa nje ya ukumbi wa Baraza baada ya kukataa kufuta kauli yake)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuendelee.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nilikuwa na swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Naibu Spika, ukiacha kuharibika kwa mfumo ambao ulikuwa katika hatuwa za majaribio Taasisi hii ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii inakabiliwa na utatizo la uchakavu wa vifaa na mashine mbali mbali zikiwemo *printer*.

(a) Je, Mhe. Waziri analifahamu tatizo hili.

(b) Je, ni hatua gani sasa wizara imelichukuwa ili kuweza kutatua ama kupunguza tatizo hili la kuchelewe utolewaji wa Vitambulisho vya Wazanzibari. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ : Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Rashidi Makame Shamsi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, naomba tukiri kwamba katika taasisi yetu hii tumekuweko na uchakavu mkubwa wa baadhi ya vifaa ambavyo vinatumika katika shughuli hizi. Kwa hiyo, naomba nikubaliane kwamba tunalifahamu.

Kuhusu hatua ambazo zimechukuliwa au ambazo zinaendelea kuchukuliwa Mhe. Naibu Spika kama ambavyo majibu ya mwanzo tumeweza kujibu kwa sasa hivi tunataka kwamba tuondokane na usumbufu ule ambao wananchi wanaweza wakaupata wakati wa kutoa huduma zetu kama vile ambavyo tumeelezea. Kwa hiyo, kiufupi ni kwamba tunaendelea kuboresha na kwa kuwa jana Mhe. Naibu Spika, tumeshapitisha bajeti ya wizara yetu ni iimani yangu kwamba hali hii tutabadilisha, ili tuone kwamba tunafanya kama vile ambavyo tumelenga katika kupitisha bajeti yetu ili kuona kwamba tunaweka mambo yawe vizuri zaidi. Ahsante.

Nam. 11

Muhali kwa Wanaofanya Vitendo vya Udhalilishaji

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny) Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Wakati Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akifunga Mkutano wa Tisa wa Baraza la Tisa la Wawakilishi alisema kuwa serikali haitamvumilia mtu yeyote, wa cheo chochote au hadhi yoyote ambaye atabainika kujihusisha na vitendo vya udhalilishaji watoto. Kwa kuwa, sheria ni msumeno na huku sheria mpya imeshapitishwa.

(a) Je, ni watu wangapi ambao wanafahamika kwa vyeo vyao na hadhi zao ambao wanajihusisha na matendo ya udhalilishaji watoto wameshachukuliwa hatua.

(b) Je, watuhumiwa wangapi wameshachukuliwa hatua tokea sheria mpya ya adhabu kupitishwa na Baraza hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 11 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, Sheria mpya ya Adhabu Nam 6 ya mwaka 2018 imeanza kutumika kuanzia tarehe 16 Machi, 2018 baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein ambapo makosa mbali mbali yameoneshwa ndani ya sheria hiyo ikiwemo makosa ya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na adhabu zake kwa mtu atakae patikana na hatia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu swali la msingi la Mhe. Jaku Hashim Ayoub lenye kufungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtka haina taarifa za watuhumiwa ambao wana hadhi zao na vyeo vyao ambao wamechukuliwa hatua kwa vitendo vya udhalilishaji hapa Zanzibar.

(c) Mhe. Naibu Spika, kwa vile sheria hii imetiwa saini mnamo tarehe 16/3/2018, hakuna watuhumiwa ambao wameshachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hii. Hii inatokana kwamba sheria hii haiwezi kutumika kwa makosa yaliyofanywa kabla ya kutiwa saini sheria hii. Ahsante

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsnte sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Rais kwa kuweka saini yake katika sheria hii muhimu juu ya kuhakikisha kwamba vitendo vya udhalilishaji katika nchi yetu vinaondoka kabisa. Lakini pamoja na hayo niseme tu kwamba majibu aliyoyajibu Mhe. Naibu Waziri ni mazuri lakini katika kuhakikisha kwamba sheria iliyowekwa inapata hukumu ya haraka, wizara ina mpango gani wa makusudi kuhakikisha kwamba inatowa taaluma kwa wananchi siku hadi siku ili kufika katika Mahakama na kutoa ushahidi na adhabu ikamilike bila ya kuwa na matatizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Ali Suleiman Ali kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba taaluma ni jambo muhimu katika mstakbali mzima kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaelewa umuhimu wa kwenda Mahakamani kutowa ushahidi.

Mhe. Naibu Spika, taasisi zetu mbali mbali zimekuwa zikitoa baadhi ya vipindi kuhakikisha kwamba wananchi wanapata uwelewa zaidi, lakini nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi kwamba na sisi tuna nafasi vile vile, sio suala la kuwaachia serikali tu moja kwa moja kwamba ndio itoe taaluma, lakini na nyinyi au sisi wawakilishi katika majimbo yetu tunatakiwa tuwe na utaratibu huu, inawezekana wewe mwenyewe Mhe. Mwakilishi, huna ile elimu ya sheria, lakini inawezekana kwamba ukamtafuta mwanasheria, ili aweze kuja kutowa taaluma katika majimbo yenu. (*Makofi*)

Kwa kweli, mimi nitakuwa tayari kuhakikisha kwamba pale ambapo mtakuwa tayari kupata wataalamu wao wa sheria basi *inshaallah* tutasaidiana kuonesha kwamba, na nyinyi wananchi wenu wa majimbo yetu wanapata taaluma hii, ili iwe rahisi pale ambapo zinapotokea kesi kama hizi wawe tayari kutoa ushahidi mbele ya Mahakama, kwani bila ya ushahidi kunakuwa hakuna hatia. Tunashukuru.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, na katika jibu (b) amesema kwamba sheria imetiwa saini mnamo tarehe 16-03-2018, na kuna watuhumiwa wote wameshachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria hii, hii inatokana na kwamba sheria hii haiwezi kutumika kwa makosa yaliyofanywa kabla ya kutiwa saini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kumetokezea mgongano wa kisheria baina ya Waheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Mahakimu na Mawakili juu ya mgongano huu, na kuna ushahidi wa kesi ya ndugu Zahor Makame Ali iliyofanyika machi kabla ya kutiwa saini hii, na amehukumiwa kwa kifungu cha sheria 15(1) cha sheria hii ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya CPA 7, 2018 na ameshindwa kupewa dhamana kwa sababu kesi yake imeanza kuhukumiwa kutokana na sheria ya sasa hivi, na Mhe. Waziri anatambiya sheria sasa hivi haifanyi kazi kwa watu ambao wametenda makosa kabla ya sheria hii kutiwa saini.

Je, Migongano hii ya kisheria anatusaidia vipi ili kuweka sawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe, amesema kuna migongano ya kisheria kwa kweli mimi sijaiona aina hiyo ya migongano ya kisheria. Lakini ninachokisimamia kwamba zile adhabu ambazo zimetolewa au zile kesi ambazo zimefunguliwa kabla ya tarehe 16-03-2018, katika sheria hii, basi kesi zile zitaendeleshwa kwa mujibu wa sheria ile.

Lakini kesi zote mpya ambazo zimefunguliwa baada au kuanzia tarehe 16-03-2018 basi adhabu zake na taratibu zake zitafuatwa kwa mujibu wa sheria hii. Kwa mfano, inawezekana sisi Waheshimiwa tumepitisha Mswada ule ambao sasa hivi ni sheria ilikuwa masuala ya udhalilishaji dhamana inapatikan, kwa hivyo sasa hivi masuala ya udhalilishaji hayana dhamana. Kwa hivyo, kama kuna kesi ya mtuhumiwa ambaye masuala ya udhalilishaji, kesi yake inaendelea kwa hiyo usije ukashangaa kwamba yuko nje, ndio yuko nje kwa maana anakwenda na anarudi kufuatia kesi yake. Ndio ni sahihi kwa sababu kesi yake imeanza kabla ya sheria hii kutumika. Hata hivyo, kesi zote zile za udhalilishaji na mtuhumiwa ameonekana kwamba kweli ametenda hili kosa, kwa hivyo huyu atakuwa hana dhamana, kwa hii ni tofauti tuione baina ya hii sheria ambayo tulifanyia marekebisho kwa maana kufutwa na hii sheria ambayo iliyokuwepo sasa. Nashukuru sana ahsante.

Nam. 2

Ulipaji wa Madeni ya Kiinua Mgongo kwa Wastaafu wa Serikali

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliweka vipaumbele vyake 9 kwa mwaka 2017/2018 ambavyo itavitekeleza, ikiwemo kusimamia ulipaji wa madeni ya kiinua mgongo kwa wastaafu wa serikali na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa mkakati wa maendeleo Zanzibar.

(a) Je, hadi kufikia Disemba, 2017 ni wastaafu wangapi wameshalipwa na wangapi waliobakia ambao walistahiki kulipwa.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika kulipa malipo hayo na kiasi gani serikali inadaiwa na wastaafu hao.

(c) Je, mfumo wa kuimarisha ufuatiliaji umefikia katika hatua gani hadi kufikia Disemba, 2017, katika mkakati wa maendeleo Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali Nam. 2 la Mhe. Shehe Hamad Mattar kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa 2017/18 ilikuwa ni kusimamia ulipaji wa madeni ya viinua mgongo kwa wastaafu wa serikali na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini (MKUZA III).

Majibu kwa swali lake lenye vifungu (a) (b) na (c) ni kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia Disemba, 2017 jumla ya wastaafu 1,075 wamelipwa mafao yao na wastaafu 67 wamebakia ambao walistahiki kulipwa mafao yao katika kipindi hicho.

(b) Jumla ya shilingi bilioni 17.776 zimetumika katika kulipa malipo hayo na jumla ya shilingi bilioni 1.335 ni deni la serikali kwa wastaafu hao 67 waliobakia katika kipindi hichi.

(c) Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tayari Tume ya Mipango imekamilisha mfumo wa ufuatiliaji na Tathmini kwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini. Muongozo huo umechapishwa na kugawanywa kwa wizara zote kwa matumizi.

Muongozo umetoa muundo wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, namna ya kukusanya taarifa na kutayarisha ripoti za ufuatiliaji na tathmini na umetoa pia viashiria na zana za kutumika katika kukusanya taarifa. Matarajio ni kuwa utekelezaji wa mfumo huo utasaidia sana katika kuondoa kasoro za ufuatiliaji na tathmini hasa kwa miradi mikubwa inayotekelezwa hapa nchini.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha kwa majibu yake mazuri na serikali jitihada yake iliyofanywa kuwalipa wastaafu. Lakini pamoja na majibu mazuri naomba nimuulize swali la nyongeza (a) na (b).

Lakini pamoja na majibu mazuri naomba nimuulize swala la nyongeza (a) na (b).

(a) Sababu zipi zinazopelekea mstaafu aliyestaafu awali kulipwa mwisho na mwisho kulipwa awali mafao yake.

(b) Ni wizara ngapi pamoja na mashirika yake yamesharejesha taarifa ya ripoti ya ufuatiliaji na tathmini hapa Zanzibar na matokeo yake ni yapi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza wastaafu hawalipwi kwa mpangilio huu Mhe. Mwakilishi ameusema, wa kwamba wa mwisho analipwa mwanzo na mwanzo analipwa mwisho, hakuna utaratibu huo na niseme tu

kwamba wastaafu wote kwa mujibu wa maombi yanayopokelewa au hesabu zinazopokelewa Wizara ya Fedha, wanawekwa katika makundi ya miezi mitatu mitatu.

Na niseme tu, hadi Disemba, wastaafu waliostahiki wamekwisha lipwa waliobaki ni wale 67, ambao hivi sasa tunatarajia wastaafu hawa watalipwa wote hadi kufikia mwezi Juni 2018, na wastaafu waliobakia tuna wastaafu 478 ambao tunatarajia kulipa shilingi karibu bilioni 10.8 na kwa kuanzia tutawalipa wastaafu 120 ambao wanatarajia kutekeleza Ibada ya Hijja mwaka huu hawa watalipwa mwanzo, lakini waliosalia mpaka ikifika Juni, 2018 wote watakuwa wamekamilika.*(Makofi)*

Watakaobakia ni wale ambao wataanzia mwezi wa Mei, ambao bado maombi yao hayajapokelewa Wizara ya Fedha lakini hili la pili, kwamba wizara zote zinafanyiwa tathmini, kwanza zinafuatiliwa na kufanya tathmini na ripoti zinatayarishwa ripoti ya miezi mitatu, miezi sita na miezi tisa. Na ripoti hizo zinawasilishwa na hapa Baraza la Wawakilishi na zitakapowasilisha Mpango wa Maendeleo tutatoa tathmini ya kazi iliyofanyika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri yanayowapa matumaini wastaafu wetu.

Lakini Mhe. Waziri, naomba tukubaliane kwa mfumo huu uliopo hivi sasa wakati fulani unaleta mashaka na mpaka kupelekea baadhi ya taasisi hasa zile zinazokwenda kuthibitisha, wakathibitisha vitu ambavyo si sahihi na kuna kesi ambazo zinawahusu baadhi ya watu wanaotengeneza hivi viinua mgogo kwa ajili ya wastaafu zinaendelea.

Je, katika kuondoa hilo serikali au wizara ina mpango gani ambao utarahisisha kutengeneza haki za wastaafu hawa kwa haraka zaidi, lakini na kuondoa yale malalamiko ambayo wanasema faili si liko kwa Mdhibiti limechelewa kidogo linahakikiwa lakini wakati mwengine linahakikiwa vibaya. Sasa utaratibu gani kwa ujumla ambao umejipanga kupitia wizara yako utaondoa usumbufu huu ulioko hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa, kwanza swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kwa wastani mtu tokea anastaafu na kupata mafao yake kwa wastani nasema, inachukuwa kama miezi mitatu ambayo hiyo ni hatua kubwa sana kutizama au kulinganisha na hali ilivyokuwa huko nyuma, inawezekana wengine wakaongeza kidogo muda na wengine ukapungua zaidi ya hapo, lakini wastani miezi mitatu na hilo limefanyika makusudi, serikali imechukua hatua makusudi ya kuhakikisha inawaondoshea usumbufu wastaafu, baada ya kufanya kazi kwa muda mrefu kulitumika taifa lao.

Sasa yanayotokea baadhi ya wakati taarifa ya wafanyakazi huwa zinakuwa na mashaka, kwa sababu baadhi ya wafanyakazi wanahama kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyengine, na ili wafanyakazi hawa wasidhulumiwe haki yao inabidi ifanyike kazi ya kina kabisa kuhakikisha kwamba taarifa zao zinahakikiwa kikamilifu.

Kwa kweli, utaratibu unaanzia kwenye wizara yake au taasisi yake anayoifanyia kazi, zinakwenda kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, baadae ndio zinaletwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo, lakini kwa wastani inachukuwa miezi tatu. Hata hivyo, pamoja na usumbufu huo ambao anauzungumza labda niseme tu, kilichotokea hivi karibuni ni kwamba bajeti tuliyoipanga ya kulipa mafao ilizidiwa kutokana na kuongezeka kwa kima cha mshahara, kwa hivyo kuongezeka kwa mafao ya wafanyakazi.

Na ilibidi ililazimishwa lazima serikali ifanye uhaulishaji wa vifungu kuingiza fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali hicho kidogo kilisheleweshe. Lakini *otherwise* walikuwa wameshalipwa karibu takriban wote.

Nam. 8

Idadi ya Ajali kwa Mwaka 2017/2018 na Kiasi cha Fidia Zilizolipwa

Mhe. Shehe Hamad Mattar – Aliuliza:

Kwa kuwa, moja kati ya malengo ya Shirika la Bima ni kumrudisha mteja wao katika hali ya zamani mara baada ya kupata janga au ajali yoyote.

(a) Je, ni ajali ngapi zilitokea kwa mwaka 2016/2017 na kuripotiwa katika shirika.

(b) Je, ni ajali ngapi ziliweza kulipwa kwa wateja wao.

(c) Je, ni kiasi gani kilitumika kulipia fidia hiyo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali Nam. 8 la Mhe. Shehe Hamad Mattar lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, ajali zilizotokea na kuripotiwa katika Shirika la Bima ni ajali 2,855. Ajali zilizoweza kulipwa fidia ni katika kipindi hicho cha 2016/2017 ni ajali 2,751 na kiasi kilichotumika kulipa fidia ni shilingi bilioni 7.9 kwa kipindi cha 2016/2017.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Naibu Spika, kwa kunipa fursa niulize swali la nyongeza.

(a) Kwa kuwa, kuna wananchi wanakata bima kamili na kutimiza muda mrefu bila ya kupata ajali yoyote. Je, Shirika la Bima lina motisha gani inayotoa kwa mteja wao ambaye kuwa amechukuwa muda mrefu bila ya ajali.

(b) Wananchi wanapopata na ajali huweza kumkamata dereva ambaye kuwa ana bima kamili ya gari yake au chombo chake, lakini hawaelewi kwamba Shirika la Bima ndio litalowajibika kulipa mafao yake au kufanya marekebisho yale.

Je, ni elimu gani wanayotowa Shirika la Bima kwa wananchi kuelewa kwamba utaratibu wa bima ni mtu gani anastahihi kutengeneza chombo kile alichopata ajali.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kuna bima za aina mbili, kama alivyozungumza, kuna bima kubwa ambayo ni *comprehensive* nadhani hiyo aliyozungumza kama bima kamili, lakini kuna Bima ya upande wa tatu kwa maana *third part*, kwa wanaokata bima *comprehensive* bima kamili, huyu anapotokewa na ajali bima ile inamjumuisha yeye, pamoja na yule atakayathirika. Lakini kiutaratibu ni lazima mara baada ya kutokea ajali au kutokea tatizo ambalo liko *covered* na bima ni lazima atoe taarifa yule muhusika mwenye bima ndani ya siku 7 anatakiwa atoe taarifa kwa maandishi pia atoe *verbal* ndani ya masaa 48, na asipotoa taarifa ndani ya kipindi hicho kwa mujibu wa mkataba malalamiko yako yanaondoka. Kwa hivyo, kwanza ni kuifahamu hiyo sheria.

Lakini la pili, alizungumzia suala hilo halitochukua muda kama wewe umeripoti kwa mujibu wa taratibu na kwa mujibu wa mkataba ambao yule ambaye aliyekata bima ameingiliana na Shirika la Bima, hatuna taarifa kwamba watu hawa wamesheleweshwa. Sasa kwa wale wananchi hawaelewi taaluma inatolewa, sasa kama haitoshi basi Mhe. Naibu Spika niahidi tu, kwamba tutazidi kutoa taaluma hiyo ila wananchi wajue, hasa wale wenye bima na wale wanaoathirika kutokana na madhara yaliyosababishwa na wenye bima. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana, Mhe. Naibu Spika, *Bismillah Rahman Rahim*. Naomba nimuulize swali la ziada lenye (a) na (B) Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

(a) Ni utaratibu gani au kiwango gani ambacho mnacho tumia kwenye kuwalipisha watu *comprehensive insurance* kutokana na mfano nitakupa, nchi nyengine hasa za nje *insurance* ya milioni 30 anaweza akaamkia gari thamani ya milioni 30, anaweza akaambiwa alipe *comprehensive insurance* labda laki tatu kwa mwaka. Lakini Zanzibar gari hiyo hiyo ya milioni 30 *comprehensive insurance* anaweza akaambiwa alipe milioni 3,800 ni vigezo gani mnatumia hata kiwango *insurance* kikubwa sana na watu wengi wanashindwa kulipia *comprehensive insurance*.

(b) Kwa kuwa, serikali ina gari nyingi sana na nyingi ni za thamani kubwa. Je, Serikali gari zake zote zimekaliwa *full insurance.*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf, swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwanza nchi hazilinganishi namna hiyo, kwa sababu kila nchi ina mazingira yake na kila nchi ina *risk factor* yake katika bima kitu kikubwa kinachoangaliwa ni ile *ris factor* ya lile tukio lenyewe na ile nchi yenyewe. Kwa hivyo, huwezi kulinganisha Zanzibar na Kenya na huwezi kulinganisha Zanzibar na Marekani ni mahala tofauti, kuna *risk* tofauti. Sasa ukihitaji *formula* naomba tuonane baadae nitakupatia hiyo *formula*.

Lakini la pili serikali kwa mujibu wa sheria, vyombo vyote vya serikali vinatakiwa vikatiwe bima kamili, bima *comprehensive* na hivyo ndivyo inavyofanyika, hata gari yangu ina bima kamili.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Lakini kwanza nitangulize pongezi kwa Mhe. Waziri wa Fedha kwa majibu mama ya swali lililotangulia. Nichukue fursa hii kulipongeza Shirika la Bima kwa kazi njema na hususan kwa kiwango hichi cha fidia ambacho kimelipwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika swali langu lina (a) na (b),

a) Kutokana na fidia zilizolipwa Shirika la Bima kwa mwaka 2016 limepata faida kiasi gani.

b) Kuna kawaida baadhi ya wenye vyombo huweza kufanya udanganyifu wa kuweza kuvisababishia vyombo vyao ajali, aidha kwa kugonga au kwa kuviunguza moto. Je, Shirika la Bima linatumia mbinu gani za ki-*intelligencer* katika kuweza kubaini haya ili kuweza kupunguza fedha za fidia ambazo zinalipwa. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe, Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Suala la faida kwa bima hilo naomba nimpatie kwa maandishi, sina *figure* ya faida kichwani ambayo Shirika hili limetengeneza, lakini najua kwamba limefanya faida katika mwaka wa fedha wa 2071/2018, lakini *figure* kamili nitampatia.

b) Suala hili la watu wadanganyifu. Mhe. Naibu Spika, watu wadanganyifu wapo na kweli wakati mwengine yanatokea mambo na hasa katika hizi ajali za moto kuna watu wengine wanatia nyumba zao moto kwa makusudi ili waweze kulipwa Bima, wengine wanatia gari zao moto kwa makusudi na hasa zenye hasara ni zile bima ambazo ni *comprehensive.* Sasa kwa ajili hiyo na kwa ku-*avoid* hilo kwa mfano una gari lako, pengine gari lako lenyewe bovu lakini unalikatia *comprehensive* kwa ajili ya kuja kufaidika baada ya kulifanyia hujuma, kinachotakiwa saa hivi na bima kwamba kwa mtu yeyote anaekata bima *comprehensive* kama ni gari lazima ipelekwe kituoni ikaguliwe. Ukaguzi unafanyika ili kupunguza athari ya udanganyifu.

   Lakini kwa zile bima za *third part*, kwa sababu yule mwenye bima siye anayefaidika na bima kunakuwa hakuna vishawishi vya namna hiyo, kwa sababu anayefaidika ni *third part* ni yule aliyeathirika kutokana na ajali au janga linalotokea. *(Makofi)*

Nam. 42

Upungufu wa Madarasa Skuli ya Konde Sekondari

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa, Skuli ya Konde Sekondari imekuwa na kilio cha muda mrefu cha uhaba wa madarasa kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi ambao zaidi hutoka skuli jirani.

(a) Je, ni lini wizara itaanza mpango wa ujenzi wa madarasa kwenye eneo lenye madarasa sita (6) yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuliondoa au kulipunguza tatizo la madarasa kwenye skuli hiyo.

(b) Je, wizara inautambua uzito wa tatizo la walimu kwenye skuli hiyo na lini italipatia ufumbuzi.

(c) Je, ni lini wizara itayakarabati madarasa yote yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kuyawekea *"ceiling boards"*, *plaster* na milango madarasa hayo ili kudhibiti viti, meza na vyenginevyo ambavyo havina uhifadhi kwa sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 lenye vifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mji wa Konde ni moja katika miji ambacho ina idadi kubwa ya wanafunzi na kutokana na wingi huo wa wanafunzi, wizara ilijenga skuli ya kisasa yenye madarasa 12, maabara tatu, maktaba na chumba cha kompyuta kutokana na mkopo wa Benki ya Dunia. Pia, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na mchango wa wizara ilijenga madarasa 6 ambayo hivi sasa yamekamilika na yanatumika. Skuli ina wanafunzi 1134 na vyumba 18 vya kusomea ambavyo vinatosheleza mahitaji kwa utaratibu wa kusoma kwa mikondo miwili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo sasa naomba kumjibu kama ifutavyo:-

(a) Wizara, haina mpango wa kujenga madarasa mapya katika Skuli ya Sekondari ya Konde. Hata hivyo, iko tayari kusaidia nguvu za wananchi pale wananchi wakishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi watakapoanzisha ujenzi wa madarasa mapya.

(b) Wizara, inautambua uzito wa tatizo la walimu katika Skuli ya Sekondari ya Konde na skuli nyingine hasa katika Wilaya ya Micheweni. Wizara, inaendelea na uajiri wa walimu wapya, kwa ajili ya kutatua upungufu wa walimu katika skuli mbali mbali Unguja na Pemba. Ahsante.

(c) Mhe. Naibu Spika, naomba kufanya mabadiliko kidogo ya majibu, kwamba mpaka sasa kwa mujibu wa uchambuzi wa madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi tunayo madarasa 533, madarasa 200 yamekamilishwa na wizara, yamebakia 333, sasa haya wizara itaendelea kuyakarabati na kuyakamilisha hatua kwa hatua ikiwemo hili la Skuli ya Konde. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Waziri.

Kwa kuwa, Mhe. Waziri Skuli ya Konde anaifahamu na kinachozungumzwa pia hilo jengo lenye madarasa sita analifahamu, kwa kuwa bado kunahitaji kuwekwa *ceiling board* kunahitaji kuwekwa milango na ndani ya majengo hayo kupo wazi kuna viti na meza na vitu vyengine ambavyo vinaharibiwa kutokana na kutokumalizwa kwa eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, napenda Mhe. Waziri anihakikishie nini muono wake au lengo la wizara yake kulimalizia kwa hatua ya kuliwekea *ceiling board*, kulitia milango na madirisha lile jengo tulilolijenga kwa nguvu zetu sisi na nyinyi, ili liweze kuwa lipo salama pamoja na madawati na vitu vyote vilivyomo mule tofauti na ilivyo hivi sasa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba naifahamu skuli hii na nayafahamu madarasa yenyewe. Sasa niseme kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwamba wizara itafanya kila linalowezekana kuona madarasa haya yanakamilishwa katika kiwango kinachotakiwa wakati wowote kuanzia sasa. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri umesema katika majibu yako kwanza unawapongeza wananchi kwa kujitolea kuhakikisha kwamba wanajenga majengo ya skuli pamoja na sisi Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, katika Jimbo langu la Ziwani, Skuli ya Kwale namshukuru sana Naibu Katibu Mkuu wa CCM kwa kuchangia shilingi milioni 3,500,000/= kwa kumalizia *staff* ya walimu kutia madirisha, milango na kufanya *finishing* nyengine, lakini pia vile vile na mimi nilichangia shilingi milioni 9 za jimbo na milioni 1 mimi mwenyewe binafsi na hivi sasa wanafunzi wale bado wanatatizo la madarasa, Konde huna mpango wa kujenga. Je, katika Jimbo langu la Ziwani, wizara yako ina mpango gani ya kuwajengea wanafunzi wale madarasa ili waweze kusoma kwa utulivu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kwa sasa Sera ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iko zaidi katika kuwashajihisha wananchi ili baadaye wizara iweze kukamilisha. Nimuombe Mhe. Mwakilishi aendelee kuwashajihisha wananchi kuanzisha madarasa haya na baadaye wizara itayafanyia kazi kama inavyofanyia kazi skuli nyengine na madarasa mengine yaliyoanzishwa kwa wananchi.

Lakini pia, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa nguvu anazozitumia katika kuhudumia Sekta ya Elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona naomba kumpongeza Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, amesema watashirikiana na nguvu za wananchi ili kujenga madarasa hayo waliyojengwa wananchi, swali langu liko hapa kuna Skuli ya Bwagamoyo na Kisiwani tayari wananchi wale wamejenga madarasa yale na sasa hivi yameshafika hatua ya kuezeka. Je, ni lini watashirikiana nao katika kuezeka mabanda yale katika skuli zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi. Nimesema kwamba madarasa haya yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yapo mengi na sasa yamebakia kama 333 zikiwemo na Skuli zake za Bwagamoyo na nyenginezo. Kwa mwaka wa fedha unaokuja baadhi ya madarasa haya yatakamilishwa, kwa hivyo tuombe dua na Skuli ya Bwagamoyo iwemo yatakamilishwa kwa wakati huo kupitia Wizara inayoshughulikia na Tawala za Mikoa, kwa sababu ukamilishaji wa nguvu za wananchi kazi hii sasa tunawapelekea wao, wao wapo karibu zaidi na nchi na kwa maana hiyo nadhani na skuli yako itazingatiwa, ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla sijajibiwa swali langu kwa ruhusa yako naomba nitoe maelezo machache halafu nipate mengineyo. Namuomba Mhe. Waziri akae.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri sisi tunaongozwa na Mhe. Rais wetu wa Zanzibibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa, kuhakikisha kwamba tatizo la Mwanakwerekwe kwenye bwawa la maji litaondoka kwa muda mfupi na katika jitihada za Mhe. Waziri na watendaji wake amenijibu vizuri katika maelekezo niliyoyapata kuna mradi wa *ZUSP* kama alivyosema Mhe. Haji Omar Kheir, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ambayo mkandarasi *CRGE* yuko tayari kufanya kazi mara baada ya mvua hizi zitakapomalizika.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa heshima kabisa namheshimu Mhe. Rais wangu wa Zanzibar pamoja na Waziri kwa majibu mazuri, naomba kuliondoa swali hili katika Orodha ya Shughuli za Leo.

Nam 202

Tatizo la Kutuwama kwa Maji katika Eneo la Mwanakwerekwe

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, swali linalofuata swali na 212 la Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Nam. 212

Mapato ya *ZMA* Kusajili Meli za Nje

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:

Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ya Zanzibar (*ZMA*) imekuwa ikifanya shughuli zake mbali mbali kwa mujibu wa sheria kama vile usajili wa meli za nje ambao ulikuwa ukileta mapato makubwa nchini. Ni hivi karibuni SMT imezuia *ZMA* kusajili meli hizo wakati suala hilo lipo kwenye mamalaka ya Zanzibar.

a) Kiasi gani cha mapato *ZMA* na Zanzibar inapoteza tokea kuzuiliwa kusajili meli za nje.

b) Kuna ukweli gani kuhusu sababu zilizotolewa na SMT kuhusu meli zinazosajiliwa na *ZMA*. Je, SMZ imefanya utafiti wake kujua ukweli wa madai ya SMT.

(c) Je, hatua gani stahiki zinachukuliwa na SMZ kuhakikisha kuwa Zanzibar inalinda maslahi yake katika suala hili.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 212 lenye vifungu (a), (b) na (c). Kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa swali hili huwa sina kawaida ya kutoa maelezo marefu lakini kwa hili leo kidogo nipeni ruhusa nieleze jinsi gani utaratibu ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini wa Zanzibar (*ZMA*) imekua ikifanya shughuli zake mbali mbali kwa mujibu wa sheria na katika jumla ya shughuli hizo ni usajili wa meli za nje ambo ulikuwa ukiileta mapato makubwa Zanzibar. Naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba hivi karibuni SMT imezuia *ZMA* kusajili meli hizo.

Mhe. Naibu Spika, *ZMA* kama Mamlaka, ina majukumu mengi katika nafasi yake hiyo na katika jumla ya hayo ni usajili wa meli za nje au kwa ufafanuzi zaidi ni usajili wa meli za kimataifa. Usajili huo ulikuwa ukileta mapato makubwa nchini na upo kwa mujibu wa sheria.

Lakini Mhe. Mjumbe na Wawakilishi wengine mliobaki pamoja na wanaotusikiliza ni vyema tukaelewa ni sababu gani iliyofanya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwe na uwezo wa kuisimamisha shughuli hiyo ya *ZMA*.

Sasa, nataka tufahamu kwamba meli ikisajiliwa na *ZMA* ina maana kwamba ni kupewa ruhusa ya kupeperusha bendera ya Tanzania, wakati inapofanya shughuli zake za safari baharini. Kwa hiyo, kama kuna kosa litafanyika ndani ya meli hiyo na ikagundulika huko inakosafiri hii ina

maana ni kwamba imevunja sheria. Na wakati huo huo Tanzania ndio iliyoiruhusu kupeperusha bendera yake nayo imevunja sheria.

Kwa mantiki hiyo, kama tujuavyo Rais wa Tanzania ni Mhe. John Joseph Pombe Magufuli na kama mnaufahamu Muungano wa Tanzania ni Tanganyika na Zanzibar, basi Malaka yake ya utawala yamefika Zanzibar na ndio mana tulimpigia kura. Kwa hiyo, meli ikisajiliwa Zanzibar ikiharibu imeharibu Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Tokea usajili wa meli za kimataifa kusimamishwa, ni kweli limesababisha hasara kwa serikali kwa kushindwa kukusanya mapato kulingana na bajeti iliyopangwa na hasa kwa vile biashara hii ni ya ushindani.

Kwa kipindi hiki cha Januari hadi Machi, 2018, Mamlaka ilijipangia kukusanya katika usajili wa meli za kimataifa jumla ya shilingi milioni 638,830,000 ambazo hadi kufikia tarehe 31 Machi Mamlaka iliweza kukusanya jumla ya shilingi 379,622,565 ikiwa ni pungufu ya shilingi 259,207,435. Mapato hayo yaliyokusanywa yalitokana na kuhuisha vyeti na utoaji huduma katika meli zilizosajiliwa kabla ya kusimamishwa usajili huo.

(b) Kuhusu sababu zilizotolewa na SMT kuhusu meli zilizosajiliwa na *ZMA* kuna ukweli kwamba, baadhi ya meli chache zilizosajiliwa na *ZMA* na kupeperusha bendera ya Tanzania zimejishirikisha na vitendo vya kusafirisha dawa za kulevya, kitendo ambacho ni cha kuvunja sheria za kimataifa.

(c) Mhe. Naibu Spika, hili halitaki tochi, wala kufanya utafiti, meli ikishukiwa kuwa imebeba vitu visivyo kubalika ikiwemo dawa za kulevya na usafirishaji wa magendo ya silaha hicho ni kinyume na sheria. Sasa, Mhe. Naibu Spika, na anambie kwa hali kama hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikuchukuwe hatua gani kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania? Na maslahi gani SMZ inayoyalinda?

Hatua zimechukuliwa na *ZMA* kwa niaba ya SMZ kuzifutia usajili meli hizo, na kwa sasa serikali imesitisha usajili wa meli mpya kama tulivyoelekezwa kwa muda, ili kufanya uchunguzi wa kina juu ya mambo hayo. Pia wizara imechuka hatua ya kufunga ofisi ya *ZMA* kama tawi lake liliyoko Dubai, ambayo iliyokuwa ikifanya kazi hiyo ya kuwashawishi wenye meli kusajili kupitia ofisi hiyo. Ofisi ya *ZMA* iliyopo Zanzibar ambayo ndio ofisi kuu iliyokabishiwa kazi hio ndio ulobaki kufanya kazi ya ushawishi ya kusajili meli, ili kupunguza tatizo hilo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini Mhe. Naibu Spika nichukue fursa hii kwa unyenyekevu kabisa nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kukaa na kutuletea jibu ambalo kila mtu yuko kimya na tumepata faida kwa nchi yetu.

Lakini pamoja na hilo, Mhe. Naibu Spika niseme tu kwamba katika taratibu zetu za usajili wa vyombo hivi mimi ikiwa nasajili gari, meli ama ndege nishampa fursa ya kufanya shughuli zake yule mtu akifanya kosa atababombwa yeye huko mbele ya safari suwli langu lipo hapa.

Je, Mhe. Waziri, kwa kuwa vitendo hivyo vimetokea katika nchi yetu na meli zilopeperusha bendera hizo au hiyo zimetoka kwa upande wa meli zilizosajiliwa sehemu ya Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, Zanzibar na Bara.

Ni hatua gani zilizochukuliwa kwa wenye meli hizo ambao wametuingiza katika matatizo ambayo hatukuyategemea, ili liwe fundisho kwa wengine lisitokee katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe Naibu Spika, anachosema Mhe. Mjumbe ni kweli, tumepata hasara na aibu kwa nchi yetu na kikubwa kilichofanyika kwamba meli ile imesimamishwa katika nchi hiyo iliyoko, kwa sababu tulikuwa tumefanya mawasiliano, walipotuletea taarifa na kuhakikishiwa kulikuwa tu na mawasiliano makubwa na kutuhakikishia kwamba kweli hicho kimetendeka.

Sisi huku kwa upande wetu *ZMA* kwa utaratibu wake kukiwa na kitu kama hicho inaifutia meli usajili. Lakini nataka nikubaliane na Mhe. Mjumbe, kwamba hilo halitoshi, isipokuwa tatizo tulilonalo sheria za *ZMA* ziliishia hapo. Sasa kinachofanyika tumeona kosa hilo tunarekebisha sheria ili tuwe na uwezo wa kulipa adhabu zaidi ya hiyo ambayo imefanyika, lakini kwa sasa hatuwezi kwenda mbali ya hapo. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini pia nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa majibu yake ya ukweli na ya uhakika. Lakini pamoja na majibu hayo nataka kuuliza swali moja lenye kifungu (a), na (b), kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, aibu ya kuzuia kwa meli kubwa, lakini pamoja na tatizo hili serikali imejipanga vipi kukabiliana na aibu nyengine inayotarajia kuja hivi karibuni ya mabaharia wetu kukutikana wanachukua dawa za kulevya kwa mujibu wa taasisi ya kushughulikia Mabaharia Zanzibar kwamba idadi yao imeshuka kutoka elfu moja mmoja mpaka mia mbili. Je, hatuoni kwamba nalo hili litaitia doa jengine Zanzibar.

b) Pamoja na kadhia ile ya meli lakini serikali zetu hizi mbili huwa zina utaratibu wa kufanya mazungumzo na kukubaliana. Je, baada ya hatua ile kuna mpango wowote wa pamoja wa serikali mbili hizi, ili kurejesha tena meli zile kusajiliwa hata kama kwa pamoja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Machano Othman Said, swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kutokana na swali lake la mwanzo serikali imejiopanga vipi kwa sababu ya mabaharia wanaokamatwa na madawa ya kulevya, mimi nasema kwamba nalo hilo pia limeshuhulikiwa

a) Mhe. Naibu Spika, hapa ninachozungumzia ni *ZMA*, baharia akienda huko anakwenda kwa utaratibu wa kwake na wala *ZMA* haihusiki likiihusu *ZMA* serikali itaingilia kati. Hata hivyo, ni kweli pia ni aibu kwa Mtanzania kukamatwa na unga, lakini *ZMA* huku haihusiki na hayo, wale wanautaratibu wao tofauti wakwenda kujisajili na kusafiri huko wanako kwenda kwa meli ambazo si za Tanzania, kwa hiyo akikamatwa yeye na unga atajibu yeye binafsi. Lakini ikiwa meli imesajiliwa na *ZMA* sasa hapo ndipo tunapoingia siku tatu kwa sababu *ZMA* ipo chini ya mamlaka yetu.

b) Mazungumzo kukubaliana baina ya serikali ya SMZ na SMT kamati ziliundwa, mazungumzo yamefanyika, jawabu zimepatikana tunasubiri amri ya kupewa ruhusa. (*Makofi)*

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vipengele (a) na (b).

Mhe.Waziri, serikali ilitunga kanuni za kulinda mazingira ya bahari kupitia *ZMA* na kutoa tozo ya *USD* 300 kwa kila meli inayoingia kwenye bahari ya Zanzibar lakini mpaka sasa tunzo hiyo haijaanzwa kutozwa.

a) Ni lini serikali itaanza kutoza tozo hiyo.
b) Je, kwa kuwa sasa ikitokea uchafuzi wa mazingira uliosababishwa na meli iliyoingia na bahari ya Zanzibar hatua gani za kisheria zinachukulia, ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, naomba niwe mkweli wa nafsi yangu kilichonileta hapa ni kuzungumzia meli na tatizo lililojitokeza haya aliyoniuliza ni vitu vyengine tofauti itabidi anipe muda au aulize swali niweze kumjibu kwa uhakika hapa sina suala la hakika kumjibu.

Nam. 130

Matatizo Yanayotokana na Ulemavu au Vifo kwa Wagonjwa

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema mwenye kurehemu aloumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote na kumtakia kheri Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)*, nawatakieni Ramadhani Kareem.

Baadhi ya madaktari hapa nchini wamekuwa wakiajiriwa bila ya kufanyiwa uhakiki wa kina kuhusiana na uwezo wao kitaaluma na kimaadili na hivyo kusababisha vifo au ulemavu ambao ungeweza kuepukwa endapo wangekuwa makini.

(a) Je, upatikanaji wa daktari na *nurse* unategemea elimu yao tu bila ya kufanyiwa utafiti wa kupima imani ya kibinadamu na mambo mengine ya kimaadili.

(b) Je, madaktari kama hao ambao wanafanya vitendo vya unyama kwa wagonjwa ama kwa makusudi au vyenginevyo hawafanyi wajibu wao ipasavyo, wanachukuliwa hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 130 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, hadi sasa wizara yangu haina taarifa yoyote kama kuna baadhi ya madaktari hapa nchini walioajiriwa bila ya kufanyiwa uhakiki kuhusiana na uwezo wao wa wa kitaalamu na kimaadili. Wizara, yangu kama zilivyo wizara nyengine za serikali inatambua uwepo wa Tume ya Utumishi Serikali ambayo ipo kwa mujibu wa Sheria Namba 2 ya 2011 kwamba ina mhakiki mtarajiwa muajiriwa kwa vigezo mbali mbali ikiwemo uwezo alio nao katika nafasi alioomba, pia kipo kitengo cha *GSO* ambacho pamoja na mambo mengine kinathibitisha uhakiki wa muhusika kabla ya kuajiriwa. Hivyo, tunamuomba Mhe. Suleiman Sarahani atupatie ushahidi wa madaktari walioajiriwa chini ya vigezo alivyovieleza katika swali lake, ili vyombo vinavyohusika viwashuhulikie kwa mujibu wa sheria zilizopo.

a) Upatikanaji wa *doctors* na *nurses* hauna tofauti na upatikanaji na mfanyakazi yoyote wa serikali, kwani inaangaliwa fani zinazotangazwa na sifa zinazohusika.

b) Adhabu kwa madaktari ambao hawakufanya wajibu wao inatolewa kutegemea na kuthibitika kwa kosa alilolifanya, kwa uzito wa kosa lenyewe kulingana na usahhidi uliopatikana na kwa kuzingatia sheria kulingana na kosa lenyewe ambalo litatamka adhabu ya kosa hasa kwa kuzingatia kwamba kila kosa lina adhabu yake. Ahsante

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushkuru sana Mhe. Naibu Spika, pia namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, hospitali tusiichukulie kama hospitali, isipokuwa hospitali ni maisha ya mtu anapokuwa tayari uhai wake anauona unalega lega anakwenda hospitali kuurejesha tena na anachukua asilimia 80% ya kupona asilimia 20% ndio yakufa, lakini kumeshajitokeza matukio mengi ya asilimia 80% ya kwamba unakufa kuliko asilimia zile tulizozikusudia kwa hivyo asilimia 20 ndio ya kupona. Sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri kuwa hoja yangu ya msingi niliyomuuliza kwamba. Je, madaktari wako wamefanyiwa uhakiki wa mbinu zote.

Mhe. Naibu Spika, kuwa na vyeti sio *formula* ya daktari kuweza kufanya ile ni kigezo kimoja. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa ushahidi katika masuala ambayo kwamba kumeshatoka makala mengi ya kwamba kuna daktari mmoja alikuwa kila wakati wake basi ukifika ana uwa watu, mpaka ikafanyiwa utafiti ukaonekana mbona huyu kila ikifika wakati wake watu wanakufa kumbe ana *allergy* na watu fulani ya kuwauwa. Sasa hapa kwetu tunakuwa na watoto wanakufa wengi, tunaangalia daktari gani anauwa watoto au watu gani sijui kama inafanyika hiyo au watu wazima kama wanafanya hivyo.

Lakini swali langu Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri pamoja na utaratibu wote aliokuwa kwamba yeye anasema hapana lakini vigezo vya kwetu hapa vimeshakuja, ameletwa mtoto akaletwa pale juu ni mlemavu na baadae akatiwa *drip* ikakaa humo mpaka akakatwa mkono. Sasa, yule daktari ndio kafanyiwa *vetting* ndio vyeti vyake vile Mhe. Waziri hilo kama anataka ushahidi huo ni wa kwanza na wengine walioua hapa nitakuletea

Lakini ya pili umeniuliza wewe hujapata taarifa yoyote, wewe kwa sababu ya sekta hii maalum ya afya umeshawafanyia *vetting* hawa watu ukahakikisha kwamba hawa watu ni wa uhakika, kwa sababu Mhe. Joh'n Pombe Magufuli na Maraisi waliopita wamefanyakazi na watu lakini wamefanyiwa *vetting* zaidi ya watu 11,000/- walikuwa hawafai kufanya *vetting* hiyo kutokana na sababu zao.

Je, Mhe. Waziri tayari ameshawafanyia *vetting* madaktari wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi katoa maelezo mengi lakini sijaona swali naomba anipe swali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Kwa sababu maelezo umeshayapata nakuuliza swali moja ni kwamba:

a) Umenambia kuwa madaktari wako hujapata taarifa ya *vetting* mimi sihusiki kufanya wewe unapopata matatizo ndio unatakiwa ufanye. Je, umeshafanya *vetting* ya madaktari wako ukajua kwamba vyeti *fake* na vilivyo sahihi.

b) Mhe. Naibu Waziri wa Afya, alitaka ushahidi wa kuonesha kwamba huna taratibu ya kwamba lakini ushahidi nakupa, kwamba ndani ya Baraza hili ameletwa mtoto ni mlemavu akawekwa shindano ya *drip* mtoto yule ikawekwa siku mbili mpaka mishipa ikafa akakatwa mkono na wabunge walichangia na Waziri alisema aliomba radhi. Je, ushahidi huo bado daktari huyo bingwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, samahani kidogo hali yangu sio nzuri.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa lakini vile vile nimshukuru sana Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, turejee kwenye majibu ya msingi yaliyotolewa suala la utumishi au watumishi wa serikali. Tunayo sheria iliyopitishwa na Baraza la hili na uko utaratibu wa kisheria ambao watumishi wote wa umma wanapitia katika utaratibu huu, pale ambapo inapatikana tuhuma ya jambo lolote kwa utaratibu kwa mfano katika Wizara ya Afya ziko bodi mbali mbali kwa kila taaluma zinahusika na lalamiko lolote linatokea. Kwa mfano, kama kuna daktari kakosea kuna Bodi ya Madaktari, kama ni *nurses* wamekosea kuna bodi yao, kama kuna wakunga wamekosea kuna bodi yao huu ndio utaratibu wa kisheria uliopo, kama kuna lalamiko lolote kwanza linaanzia huko, na ndio maana hata Mhe. Mahmoud Thabit Kombo aliyekuwa Waziri wa Afya alipotoa kauli juu ya mtoto aliyeopata matatizo basi kwanza alizuhusisha bodi

zinazohusika na mimi nashukuru alipoondoka alikabidhi kazi hio na hatimae na mimi nikachukua wanasheria na nikalipeleka kwa Mwanasheria Mkuu kupata maamuzi ya mwisho.

Lakini cha msingi ni kwamba katika jambo ambalo tumefanikiwa sana Zanzibar tumetoka kutoka madaktari watu kumi na tano elfu kuhudumiwa na daktari moja leo tumefika elfu nane *record* ya dunia inatakiwa tuwe na watu angalau elfu sita sema ni kazi kubwa iliyofanywa na serikali kupata madaktari.

La pili kwamba mtu unamchunguza kwa sababu ya cheti chake ndio utaratibu wa kisheria uliopo, jambo la kwanza ni kuangalia *qualification* zako ulizo nazo, haya mambo mengine ya siri kwamba kafanyaje ndio maana tunazo hizi bodi kuangalia vitendo vinavyotokea kwa kila hatua, ili mtu aweze kufikia hapo. Sasa kusema watu wengi wanakufa kwa siku moja watoto wanaozaliwa Mnazi Mmoja ni watoto mia moja hatujakuta watoto thamanini wamekufa hata siku moja.

Kwa kweli, hii watu mia moja nimekwenda mwenyewe kwa kushuhudia kwa jicho, hatujakuta watu thamanini wamekufa, hiyo ndio takwimu tuliopata sasa hivi kwamba wanakufa asilimia thamanini sasa katika mia moja sijakuta mimi watu wamekufa thamanini.

Nimekwenda Makunduchi tena watu wanazaa vizuri sana pale Makunduchi, nimeshuhudia watoto wanazaliwa kumi na tano hukuti hata mmoja amefariki. Kwa hiyo, sio kweli kama watu wanakufa ovyo hapana na serikali inachukua serikali inachukua tahadhari kabisa kuhakikisha kabisa Wazanzibari hawa wanapata, na ingekuwa *death* hii tunayosema tusingetoka kutoka watu laki tano tukahudumiwa na watu milioni moja na nusu haiwezekani *by all data's* kuna *population* ya watu laki tatu umefikia leo tuko milioni moja na laki tano kama watu wanakufa kwa *rate* hii tunayoambiwa basi hakuna mtu.

Mhe. Naibu Spika, na ukichukua takwimu za hospitali watu wanaopata matibabu ni watu milioni moja na laki moja kwa mwaka ukichukua kwa *average* hiyo ya watu thamanini wanakufa maana yake tumebaki watu laki mbili. Kwa hiyo, nasema hizi *data* ni vizuri tukazitizama vizuri, tukazifanyia kazi vizuri na unapoleta na hoja na sisi tukakujibu vizuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie serikali imejipanga sasa hivi tuna madaktari wengine wako nje wanasoma wanakuja nakubaliano nae kabisa kuwa na cheti na kuwa na *qualification* jambo jengine unaweza ukawa na cheti kizuri, lakini hujafanya *practice* na kwa kweli hili nakubaliana nalo kabisa, na tumewaeleza madaktari wetu, kwamba una *masters* yako ukaitwa *professional* lakini kumbe hujafanya *practice* kwa utaratibu wetu lazima ufanye *practice,* ili tukuone kama kweli ina *qualify* na hilo jambo unalofanya ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na katika jibu mama kakiri kwamba daktari au muuguzi wetu akifanya kosa anachukuliwa hatua. Kwa hiyo, napenda kujua kwa kweli na waziri mwenyewe kakiri kwamba kuna suala la huyo mtoto kukatwa mkono na kawaachia bodi kuchukua hatua.

(a) Nataka nijue ni hatua gani zilichukuliwa na bodi.

(b) Je, wale waliokuwa na makosa walitambulishwa kwamba wanamakosa na hadi leo hii wamechukuliwa hatua gani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nimeelezea hapa baada ya bodi zote mbili kukaa. Kwanza jambo lenyewe limetokea mwaka 2014 ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe wakajua limeanza lini, sio jambo la juzi. Bodi zinazohusika zimefanyakazi yake na waziri akapokea taarifa akanikabidhi mimi taarifa ya bodi, mimi nikawakabidhi wanasheria wangu ndani ya ofisi wakamaliza kazi yao nikampelekea Mwanasheria Mkuu, ili sasa twende kwenye hatua nyengine ya kuiambia serikali na serikali hatimae itoe kauli, huu ndio utaratibu wa kiserikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo mimi baada ya kupokea taarifa kazi ya kwanza ni kuwatafuta wanasheria ndani ya wizara tukawakabidhi taarifa za bodi mbali mbali kila bodi inatoa ushauri wake Bodi ya Madaktari wametoa ushauri wao, Bodi ya Wakunga wametoa ushauri wao, Bodi ya Wauguzi wametoa ushauri wao, tukaona makosa aliyofanya mama mwenyewe mzazi tumeygundu makosa yake, tukasema hebu twendeni kwenye utaratibu wa kisheria, tukawapelekea wanasheria wetu, wanasheria wamemaliza, tumempelekea Mwanasheria Mkuu na *file* liko kwa Mwanasheria Mkuu akimaliza yeye ataishauri serikali hatua gani za kuchukuliwa tutawaelezea wananchi kwa jumla. Lakini nataka kuelewa kwamba tu jambo hili ni la 2014 lisifanywe kama la jana la kwanza.

Lakini la pili ambalo ni la msingi vile vile, kwa kawaida madaktari, ma *engineers* wote wanafahamu kila nchi inakuwa kiwango cha idadi fulani. Kwa mfano, ukichukua Marekani *engineers* mia mbili kwa kila watu elfu moja na kwetu sisi kwa madaktari sasa hivi tuko elfu nane kwa daktari mmoja, sasa ukichukua ile *volume* yake ya kazi anayoifanya na muda anaoutumia kwa kazi halafu unaweza kum-*judge* huyu daktari anafanya kazi yake sawa au si sawa sawa. Pili unaangalia na vifaa anavyotumia vya kufanyia kazi je ana vifaa vya kutosha vya kutosha vya kufanyia kazi yake, tatu unaangaliza mazingira anayofanyia kazi hayo ni mambo ya msingi lazima uyaangalie sasa unapokweda una *condemn* watu bila kuangalia mambo mengine hatutendi haki hata kidogo.

Mimi nakubali kabisa uko uzembe, nakubali kabisa yako maneno ya ovyo kabisa watu watupiwa maneno mabaya nakubali kabisa na nimeyakuta, nimeyakuta mwenyewe kabisa mtu anasema kwa jeuri kabisa hapa Waziri hata akilala hapa ndani ya nyumba tutafanya haya, nimeyakuta. Lakini usimchukulie mtu mmoja anayefanya kosa ukasema watu wote wanafanya makosa, leo nakupeni hizi *data* kuonesha kwamba watu milioni moja wanatibiwa kila mwaka nchini kwetu kama *death* ni hii tunoambiwa basi hakuna mtu aliyekuwa hai hapa na tusingekuwa *one point three million*, kwa hiyo naasema *measure* zipo za kuchukuliwa na mimi nakubaliana kabisa lililotokea hili tatizo nitalifanyia kazi lazima tuangalia ile ya kukatwa mkono kwanza Mhe. Naibu Spika ni kitendo cha mwisho.

Lazima ungalie ilikuwaje mpaka mtoto akafika kukatwa mkono sasa huwezi ku-*jump* kwa kukata mkono lazima uanzie ni sawa sawa na vile lazima tuangalie kama meli watu elfu tatu wamezama si lazima uangalie msingi wake, meli ile ikiwa nzima au mbovu na kadhalika. Kwa hivyo,

unangalia vitu vingi huangalii kitu kimoja tu lazima uangalie msingi wa jambo halafu utoe maamuzi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe.Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika majibu wa msingi Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu, alizungumzia masuala ya ulemavu pamoja na uwezo wa kitaaluma wa madaktari wetu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi zilizochukuliwa na serikali katika kuboresha mazingira. Lakini moja katika mambo ambayo nayatambua sasa hivi kwamba serikali imezuwiya *seminars* pamoja na mambo ambayo ya gharama iliyokuwa si ya msingi ili kuokoa fedha za umma. Sasa swali langu ni moja.

(a) Je, ni utaratibu upi ambao Wizara ya Afya unatumia sasa hivi kuwakutanisha madaktari bingwa pamoja na wale wa kati kati pia katika mandhari amabayo inayopendeza yenye utulivu, ili kuhakikisha kwamba ule utaalamu wao wanaweza kuujadili kwa mazingira ambayo yanayofaaa, kwa ajiliya kuweza kutoa huduma inayostahiki kwa wananchi ambayo ni masuala haya.

(b) Madaktari hawa pia ni binadamu kama sisi sote na wao pia hupata mitihani na changamoto tofauti. Sasa madaktari hao wanapamabana na mambo mengi pale ambapo wanapohitaji na wao msaada wa kuweze kuzungumza na wanapohitaji mazingira ambayo ya kwao pia kimaslahi au ya kwao wenyewe binafsi yaboreshwe au wanapokuwa na matatizo pia ya kiafya.

Je, ni utaratibu upi ambao Wizara ya Afya wameupanga, ili yaweze kufika serikalini au madaktari hawa waweze kupata ule msaada ambao wa *individual* au mmoja mmoja pia, ili serikali iweze kuwasikia na kuwasaidia hasa katika kutoa huduma moja kwa moja ya wananchi.

Naomba majibu yangu nipate yanayostahiki ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwanza nilikuwa nataka nimshukuru sana Mhe. Mjumbe kwa swali lake zuri sana. Kwanza ni kweli kabisa hawa madaktari mbali vikao vyao kama madaktari wanakutana navyo, lakini vile vile walikuwa na hoja kwamba wakutane na serikali kwa ujumla na mimi kwa bahati nzuri nilikutana nao nikawasikiliza shida zao na hatimaye wakatoa ombi tunataka pia tuonane na Mhe. Rais wa Zanzibar, hivyo nataka niwambie rasmi Mhe. Rais wa Zanzibar amekubali kukutana nao na atazungumza nao, kwa utaratibu wa kiserikali wa kuwapa *forum* kukutana nao na tutaimirisha sawa.

Lakini la pili ambacho tunawasaidia tunapata madaktari mabingwa kutoka nchi mbali mbali tunazo *camp* mbali mbali juzi tulikuwa na ma *Spanish* walikuja tulikuwa na ndugu zetu kutoa Saudia walikuja wanapata fursa ya kukaa madaktari kupata taaluma zaidi kwa mabingwa ambao wanakuja, ndani yake mule ndani tunaangalia *ethic* zao. Mhe. Naibu Spika, jana nilikuwa napata taarifa kuhusiana na taratibu ambazo madaktari waliokuja hapa wakagundua kuna kasoro wapi na wapi turekebishe. Kwa hivyo, hayo ni mambo tunayofanya hivi sasa kuangalia sisi

tunayofanya huku ndani na wenzetu wanapokuja nje na taaluma wanayotupa ni vitu gani tuvirekebishe nalo hilo linafanyika hivi sasa.

Lakini suala la maslahi yao ni kweli kabisa na hiyo ndio *forum* ambayo tunataka kukutana nayo, ili wazungumzie maslahi yao ili wakalingishe na watu wengine wanaopata maslahi. Kwa hivyo, mambo yote kwa kweli Mhe. Naibu Spika tunajitahidi sana kuona madaktari wetu mbali na *increment* iliyotolewa na mshahara tuangalie mazingira yao wanayoishi, nyumba za kuweza kuishi madaktari wetu yote hayo ni mambo katika serikali hii tunayaangalia.

Nataka nimshukuru kipekee Mhe. Rais wa Zanzibar sana kabisa kaniongezea bajeti ya wizara hii maradufu kabisa ili iweze kupambana na matatizo ambayo yanatukabili ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 63 nikikazia na 37 kama utanihitaji nisome au niseme nililokusudia nasoma ya 37.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, isome.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu Kanuni ya 37 kwanza.

> Kanuni ya 37 inaeleza hivi:
>
> "Waziri au mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba swali aloulizwa waziri mmoja anaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Naibu Spika, nataka niweke *Hansard* sawa, kwa sababu Mhe. Waziri hakunifahamu, nilichozungumza siyo kwamba watu wanakufa thamanini, nilizungumza imani kwamba anapokuwa mtu yuko hai akapata matatizo ya kuumwa anaende hospitali kwamba kule ndio atapata uhai wake, sasa mtu anapotoka kule akiwa mzima anakwenda kule asilimia thamanini hata kama atakufa atapona. Lakini sasa hivi baadhi ya maeneo mengine mtu yule anapokwenda kule asilimia thamanini anaona atakufa kuliko ile asilimia ishirini siyo kwamba watu wanakufa kwa asilimia mia. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri sijasema kwamba watu wanakufa asilimia thamanini *no,* isipokuwa nilizungumza imani ambayo kutoka na hali ya madaktari wetu hawa wanaofanya na amekiri wanaofanya manyago manyago. Hivyo, namuomba hasa Mhe. Waziri azungumze sana na madaktari wetu kwamba huko ndiko tunakokimbilia.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, mpe majibu sahihi kutokana na swali lake ambalo ameliuliza.

Mhe. Waziri wa Afya: Namshukuru sana Mhe. Suleiman Sarahan Said kwa kutaka kutoa ufafanuzi wa swali lake. Nafikiri nilivyomuelewa ni kwamba kama asilimia thamanini ya watu wanaenda hawana imani na daktari na nikasema kwamba watu milioni moja wanakwenda hospitali na wote hawana imani na daktari hali yetu imekuwa mbaya sana. Lakini katika watu milioni moja wanaokwenda hospitali wakitokea watu asilimia tano, kumi hawana imani ya daktari hiyo kesi ni tofauti, ukichukua ama kufa au kutokuwa na imani yote mawili chukua watu milioni moja wamekwenda hospitali lakini walipokwenda hospitali hawana imani asilimia thamanini ni tatizo.

Kwa hiyo, nakubaliana na yeye kabisa kama unazungumzia suala la imani hilo ni suala mtu mwenyewe, lakini nasema takwimu zinaonesha watu wanaokwenda hospitali na kupata matibabu na kurudi ni kiwango ni kikubwa sana. Sasa, kama kuna mtu moja au wawili ndio hawana imani watakuwa ni wawili watupu hawafikii asilimia hiyo ambayo inasemwa, bado na *maintain* hilo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, lengo na madhumuni yote ya Baraza letu hili ni wananchi kusikia maneno mazuri yanayotoka kwenye serikali maneno yanayotoka kwenye serikali kwamba imani ya wananchi waende hospitali na matatibu mazuri na watafanikiwa. Kwa kweli, nilipata maelezo kutoka na matatizo yalonifikia kama ndio sahihi ya Mhe. Waziri, sina tatizo naye, nashukuru sana Mhe. Naibu Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo katika Baraza hili Tukufu tukiwa salama katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuliongoza vyema taifa letu na kutuletea maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Uongozi wake imara na makini umeiwezesha serikali kutekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020. Hakika mwelekeo huu ndio nguzo ya kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar inayoelekeza nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020. *(Makofi)*

Vilevile, kwa namna ya kipekee naomba kumpa pongezi za dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kutimiza azma yake aliyoahidi wakati wa kuinadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuongeza maslahi ya watumishi wa umma kutoka kima cha chini cha shilingi laki moja na hamsini (150,000) hadi kufikia kima cha chini cha shilingi laki tatu (300,000). *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kuendelea kumshauri vyema Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, nikupongeze wewe Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza, kwa kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Baraza letu la Wawakilishi. Vile vile, ninawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Baraza, kwa kufanya kazi zao kwa uadilifu, umakini na weledi. Kamati hizi zimeweza kutoa ushauri na maelekezo yanayosaidia sana utekelezaji wa majukumu ya wizara na taasisi zetu kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Hassan Hafidh Khamis, Mwakilishi wa Jimbo la Welezo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Mhe.Dkt. Makame Ali Ussi, Mwakilishi wa Jimbo la Mtopepo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kuteuliwa kwao na Mhe.Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni ishara tosha kwamba Mhe. Rais ana imani nao katika kusaidia utekelezaji wa majukumu ya wizara hizo kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii maalumu kuishukuru Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini na Makamo wake Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mwakilishi wa Viti Maalumu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mzuri iliyotupatia wakati wa kupitia Muhtasari wa Taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na Mapendekezo ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika**,** napenda kumshukuru Mhe.nMiraji Khamis Musa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, Makamu Mwenyekiti Mhe. Shaibu Said Ali Mwakilishi wa Jimbo la Chonga, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mzuri waliotupa wakati wa kupitia Muhtasari wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na Mapendekezo ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri Mhe. Khamis Juma Mwalim, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Pangawe kwa kunisaidia vyema kutekeleza majukumu ya Ofisi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki iwapo sitomshukuru kwa dhati kabisa Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Kiongozi wa Utumishi wa Umma Zanzibar kwa maelekezo na ushirikiano mzuri

ulioiwezesha izara hii kutekeleza majukumu yake ya kuwatumikia watumishi wa umma na wananchi kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati na kwa upendo mkubwa niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kuendelea kuniunga mkono na naomba waendelee kunipa ushirikiano. Kwa upande wangu na mimi nitaendelea kushirikiana nao kuhakikisha kuwa maendeleo yanapatikana. Aidha, ninaishukuru familia yangu kwa msaada wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa niwasilishe utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa malengo ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya shilingi 21,563,210,200.00 kwa kazi za kawaida ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2018, kiasi cha shilingi 15,773,157,034.00 kilipatikana kwa matumizi ya kawaida, zikiwemo shilingi 10,211,308,735.00 za mishahara sawa na asilimia 76 na shilingi 5,561,848,299.00 za matumizi mengineyo, sawa na asilimia 69.

Mhe. Naibu Spika, shughuli za maendeleo zilitengewa Shilingi 2,025,382,000.00 na kiasi kilichopatikana ni shilingi 180,000,000.00 milioni kutoka serikalini na shilingi milioni 94,080,000.00 zilipatikana kupitia mchango wa *UNDP* katika utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ruzuku ofisi ilikadiriwa kutumia shilingi 2,245,900,000.00 na hadi kufikia Machi 2018, ofisi imepokea shilingi 1,677,111,683.00 sawa na asilimia 75. Kwa upande mwingine, ofisi ilikadiria kukusanya shilingi 714,639,000.00 ili kuchangia mapato ya serikali. Hadi Machi 2018, fedha zilizokusanywa ni shilingi 446,322,439.00 sawa na asilimia 62 (*tuangalie viambatanisho nam. 1,3 na 4).*

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia Mafungu tisa ambayo ni G01-Ofisi Kuu; G02 Mahakama; G03-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; G04-Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; G05-Tume ya Kurekebisha Sheria; G06-Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; G07-Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; G08-Kamisheni ya Utumishi wa Umma na G09-Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumiahi wa Umma na Utawala Bora maelezo ya kina ya uchumbuzi wa kina kiidara unapatikana kuanzia kifungu cha 16 hadi kifungu cha 60.

Mhe. Naibu Spika, Fungu la G01 linahusu Programu tano ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma; Programu ya Uimarishaji Mawasiliano ya Serikali; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, katika fungu hili la G01 kuna Programu ndogo tisa na hadi kufikia Machi 2018 Programu hizo zilitekeleza yafuatayo: -

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma inatekeleza programu ndogo mbili ambazo ni Maendeleo ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi. Programu ndogo ya Maendeleo ya Rasilimali Watu ina lengo la kuendeleza mipango ya upatikanaji wa watumishi wenye sifa watakaopelekea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo kwa watumiaji wa mfumo wa kieletroniki wa taarifa za watumishi, muongozo wa uandaaji viongozi katika utumishi wa umma na muongozo wa tathmini ya mafunzo yametolewa Unguja na Pemba. Mpango wa miaka mitano wa rasilimali watu wa mwaka 2017/2018 umepitiwa na mpango wa mwaka 2018/2019 umeidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, vikao vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi vimeratibiwa na kusimamiwa ili kujadili masuala ya kiutumishi. Aidha, watendaji wanne wameshiriki Mkutano wa Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma na kupata fursa ya kujifunza na kupata uzoefu wa mbinu za uendeshaji wa shughuli za kiutumishi. Kazi nyengine zilizofanyika ni kutayarisha Muongozo wa tathmini ya mafunzo na kutoa mafunzo katika ngazi ya taifa na ngazi ya mikoa na wilaya.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba, kupitia Programu hii ndogo, ofisi inakamilisha maandalizi ya kuwahamisha rasmi watumishi 9,611 kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka katika Sekta za Elimu (7,922), Afya (1,201) na Kilimo (488), ili kuanzia mwezi Julai 2018, watumishi hao wawe chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Hatua hii inafanywa kufuatia tathmini ya ugatuzi iliyofanywa na kamati tano zilizoundwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, kupitia programu ndogo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi watumishi wa umma wamepangwa katika miundo ya utumishi kwa mujibu wa sifa za kielimu, vyeo na uzoefu wa kazi alionao mtumishi imefanyika. Kazi nyingine zilizofanyika ni marekebisho ya mishahara kwa kada ya maofisa utumishi, pencheni za wastaafu na mazingatio ya pencheni kwa watumishi waliokuwa katika nafasi za uteuzi wa Mhe. Rais. Mapendekezo ya malipo ya posho za safari za nje yametayarishwa na tayari ufumbuzi wa malipo ya viinua mgongo kwa watumishi wa Idara Maalumu za SMZ umepatikana.

Programu ya Uimarishaji wa Mawasiliano ya Serikali

Mhe. Naibu Spika, umuhimu wa kuunganisha mfumo wa malipo ya mishahara na ule wa usimamizi wa rasilimali watu umeelezwa vyema kwenye Mkakati wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma Zanzibar. Katika kipindi hiki, hatua zilizochukuliwa ni maandalizi ya mfumo wa malipo ya mishahara utakaounganishwa na mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu (*an integrated human resource and payroll system*).

Mhe. Naibu Spika, hatua zilizokwisha tekelezwa ni pamoja na kuandaa mfumo wa malipo ya mishahara ambao unaipa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora uwezo wa kusimamia mfumo huo moja kwa moja. Hivi sasa upo katika majaribio kwenye Ofisi

ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora ina lengo la kuimarisha misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa Taasisi za Serikali. Mikutano na semina za kuelimisha masheha, vituo vya elimu na wananchi kwa jumla imefanyika. Jarida la kwanza la Utawala Bora limechapishwa na kusambazwa kwa wahusika mbali mbali. Jumla ya vipindi 28 vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji *ZBC* na vipindi sita kupitia Redio Jamii Mkoani Pemba. Kwa upande mwingine, makongamano ya utawala bora yalifanyika Unguja na Pemba yameleta hamasa kwa wahusika kuzingatia utawala bora katika shughuli zao.

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

Mhe. Naibu Spika, migogoro ya kidini imetatuliwa, kuratibu na kusimamia vikao vya Baraza la Ulamaa, kuendesha vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa mwezi na kujibu maswali ya Dini ya Kiislam ya wananchi. Ziara za misikiti na vyuo vya *Qur-ani* zilifanyika kwa lengo la kuratibu shughuli za taasisi hizo.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetekeleza programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa Masuala ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Uongozi na Utawala imeendesha vikao mbali mbali kama vilivyoainishwa kulingana na majukumu yake. Aidha, semina na mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka, kuandaa mpango wa rasilimali watu, kuandaa mpango wa mafunzo, uingizaji wa taarifa za watumishi katika mfumo wa kielektroniki na mafunzo ya mpango wa urithishaji wa uongozi yametolewa. Programu hii imeendelea kuratibu masuala ya utumishi ambapo hadi kufikia Machi, 2018 ofisi ina jumla ya watumishi 1,280 inayojumuisha watumishi 255 wa idara na watumishi 1,025 wa taasisi za wizara *(tuangalie viambatanisho Nam. 8(a) na (b)).*

Mhe. Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa kupitia Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ni pamoja na kuandaa taarifa za utekelezaji za 2017/2018 pamoja na kuandaa mpango wa mwaka 2018/2019. Mapitio ya sheria ya adhabu na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai yamekamilika na sheria hizo tayari zimepitishwa Baraza la Wawakilishi. Sera ya Msaada wa Kisheria imepitishwa rasmi na rasimu ya sheria yake ipo katika maandalizi. Maofisa Mipango wamejengewa uwezo wa uchambuzi wa sera, maandalizi ya mpango na bajeti, ufuatiliaji na tathmini na umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi.

Mhe. Naibu Spika, shughuli za utafiti zilizotekelezwa ni pamoja na utafiti wa uhakiki wa mali za wakfu, utafiti mdogo uliofanywa kwa lengo la kupata taarifa zitakazosaidia utaratibu wa kuanzisha '*Law School in Zanzibar'* na Tathmini ya Mwenendo wa Utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria. Aidha, imefanyika tathmini na ukaguzi wa mifumo na vifaa vya TEHAMA kwenye taasisi 17 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina lengo la kutoa huduma za ofisi, kusimamia watumishi na kuratibu shughuli za Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2018 ofisi inaendelea kuwa kiungo muhimu cha shughuli za wizara kisiwani Pemba kwa kuratibu shughuli za kitaifa, kazi za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na kufuatilia masuala ya kiutendaji kwa idara na taasisi za wizara na hatimaye kutoa taarifa wizarani.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilikuwa ikisimamia pia utekelezaji wa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa na Ofisi ya Hakimiliki. Mabadiliko ya muundo wa wizara yaliyofanyika hivi karibuni, yamepelekea Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kupelekwa katika Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale na Ofisi ya Hakimiliki imepelekwa katika Wizara ya Vijana, Utamaduni Sanaa na Michezo.

Taasisi Zinazopokea Ruzuku

Mhe. Naibu Spika, Fungu la G01 lina taasisi tatu zinazopokea ruzuku ambazo ni: Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Chuo Cha Utawala wa Umma na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Utekelezaji wa majukumu katika taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Naibu Spika, katika urithishaji wa mali za marehemu waislamu, jumla ya tirka 1,073 zimefunguliwa, tirka 639 za mirathi zenye thamani ya shilingi 16,589,178,708 zimefungwa na warathi kupewa haki zao. Aidha, Kamisheni imetoa ushauri wa kisheria kwa kesi 61, imetatua mizozo 26 na 61 kupelekwa Mahakamani kwa kutolewa hukumu.

Mhe. Naibu Spika, tathmini ya mali, kumbukumbu na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inafanyika na iko katika hatua za mwisho. Kodi ya shilingi 287,233,100.00 ya nyumba na shilingi 4,930,000.00 za mapato ya mashamba imekusanywa. Vile vile, Zakka na misaada ya kheri yenye thamani ya shilingi 396,885,000.00 imekusanywa na kugawiwa kwa wanufaika. Sala na Baraza la Idd el Hajj kitaifa limeratibiwa na kufanyika Fumba Wilaya ya Maghribi 'B'. Kati ya Mahujaji 1,906, wa Tanzania nzima, Mahujaji 1,077 walisafirishwa na taasisi za Zanzibar. Kwa upande mwingine, waraka wa kuundwa Mfuko wa Hijja umewasilishwa Wizarani kwa taratibu za kisheria.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Programu ndogo ya Chuo cha Utawala wa Umma ina lengo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma. Mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa watumishi 1,144 kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali. Mafunzo hayo yalihusu masuala ya itifaki, mikopo na vyama vya ushirika kwa watumishi wa Chuo Cha Utawala wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya maadili ya kazi yametolewa kwa watumishi wapya 3,902 kutoka Wizara na Taasisi za Serikali zikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *SUZA*, Shirika la Umeme *ZECO* na *ZURA*. Watumishi tisa wameshiriki mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa lengo la kuimarisha rasilimali watu ya Chuo cha Utawala wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kimejiandaa kutoa shahada ya kwanza katika fani za Menejimenti ya Rasilimali Watu; Uhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka; na Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia. Ili kufanikisha hatua hiyo, serikali inaandaa utaratibu wa kukijengea uwezo Chuo hicho cha *IPA* ili kiweze kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi zaidi.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma ina lengo la kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Jumla ya fomu za viongozi 1,631 zilipokelewa na kusajiliwa sawa na asilimia 99 ya shabaha iliyopangwa ya kupokea fomu za tamko la mali na madeni 1,650. Orodha ya viongozi waliowasilisha fomu imechapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali (Tangazo Nam. 8 la Februari 2018).

Mhe. Naibu Spika, uhakiki wa taarifa za mali na madeni za viongozi wa umma umeendelea ambapo jumla ya viongozi wa umma73 walifanyiwa uhakiki wa taarifa zao Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, taarifa za mapato na matumizi kwa fungu G01 zinapatikana katika Viambatanisho Nam. 1,3&4.

G02 – Mahakama(maelezo zaidi yanapatikana kuanzia kifungu cha 61 hadi kifungu cha 75)

Mhe. Naibu Spika, ili kufanikisha jukumu la upatikanaji wa haki na uwajibikaji, Mahakama imesikiliza kesi za madai na jinai pamoja na rufaa za Mahakama Kuu. Hali ya usikilizaji wa kesi katika ngazi mbali mbali za Mahakama ni kama inavyoonekana katika viambatanisho. Uchambuzi huo, unaonesha kuwa Mahakama imepokea na kusajili jumla ya mashauri 8,956 kutoka Mahakama zote kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2018 ambapo idadi ya mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 6,274 sawa na asilimia 70. (Viambatanisho Nam. 6(a), (b) na (c) vinatoa ufafanuzi zaidi).

Mhe. Naibu Spika, Mahakama tayari imeanza kuchukua hatua za ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu. Hatua hizo ni pamoja na kufuatilia upatikanaji wa hatimiliki ya

kiwanja, kupata Mshauri Elekezi na kutayarisha eneo la kiwanja. Hatua iliyofikia sasa ni kwamba Mshauri Elekezi amekamilisha michoro ya jengo hilo na yupo katika hatua ya kutayarisha "*Bill of Quantities*" (*BOQ*). Aidha, ofisi yangu inaishukuru serikali kwa kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Mahakama ya Mwanakwerekwe.

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (maelezo zaidi yanapatikana kuanzia kifungu cha 76 hadi kifungu cha 83)

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa miswada sita ya sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa na hatimaye kupitishwa. Miswada hiyo imetiwa saini na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na sasa ni sheria kamili. Ofisi pia imeandaa Kanuni 12 zinazotokana na Sheria tofauti kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi. Vile vile ofisi imeandaa matangazo ya kisheria 51 yanayohusu mambo mbali mbali ambayo yalihitaji kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Mhe. Naibu Spika, ofisi imeendelea kuishauri serikali juu ya masuala ya mikataba ambapo jumla ya mikataba 258 ilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri. Aidha, Hati za Maelewano (MoU) 56 zinazohusu Sekta ya Elimu, Afya, Ujenzi, Biashara, Uchumi, Kilimo na Uvuvi zilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri. Ofisi imesimamia jumla ya kesi 85, katika kesi hizo kumi zimefikia hatua ya kutolewa uamuzi ambapo, nane serikali imeshinda na kesi 75 zinaendelea.

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Mhe. Naibu Spika, ofisi ina lengo la kuendesha na kusimamia kesi za jinai kiraia na kukuza mipango na uendeshaji wa ofisi. Kati ya kesi za jinai 2,205 zilizofunguliwa katika Mahakama za Unguja na Pemba, jumla ya kesi 1,068 zimetolewa uamuzi, sawa na asilimia 48.

Mhe. Naibu Spika, katika kukuza mipango na uendeshaji, ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi saba katika kada ya sheria ngazi yashahada ya uzamili. Kati ya hao sita wanaume na mmoja mwanamke. Jumla ya wanasheria kumi walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ambayo yameongeza ujuzi na taaluma ya kutekeleza vyema majukumu ya kazi.

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria(maelezo zaidi yanapatikana kuanzia kifungu cha 86 hadi kifungu cha 89)

Mhe. Naibu Spika, tume imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kukamilisha mapitio ya sheria tano, ambazo ni Sheria ya Kamati ya Uongozi Nam.10/1986, Sheria ya Jumuiya Nam.6/1995, Sheria ya Msimamizi wa Mirathi Sura ya 23/1925, Sheria ya Udhibiti wa Kodi Sura ya 98/1957 na Sheria ya Kuhifadhi Utamaduni wa Taifa Nam.1/1973. Aidha, mapitio ya Sheria ya Mahakama Kuu Nam.2/1985 na Sheria ya Mahakama za Chini Nam.6/1985 yamefanyika kwa hatua ya kwanza na yataendelea kwa hatua ya pili katika mwaka 2018/ 2019.

G06 –Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(maelezo zaidi yanapatikana kuanzia kifungu cha 90 hadi kifungu cha 93)

Mhe. Naibu Spika, ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuimarisha uwezo wa watumishi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi kama vile ukaguzi wa mazingira, (*Environmental Audit*) ukaguzi wa kompyuta, ukaguzi yakinifu (*Value for Money*) na ukaguzi wa aina nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya ukaguzi wa hesabu unaozingatia viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa, mafunzo ya mabadiliko ya teknolojia katika mifumo ya uhasibu na ukaguzi na mafunzo ya mabadiliko ya bajeti kwa wakaguzi kutoka katika mfumo wa vifungu '*Line Items'* kwenda mfumo unaozingatia matokeo (*PBB*) yametolewa.

G07 – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi(maelezo zaidi yanapatikana kuanzia kifungu cha 94 hadi kifungu cha 101)

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uzuiaji wa vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ina lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya kuchukua hatua za kinga dhidi ya rushwa na kufanya uchunguzi wa vitendo vya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa elimu juu ya rushwa na athari zake inawafikia wananchi, ofisi imeanzisha huduma ya kupiga simu bure (*toll-free113*) ili kurahisisha utoaji wa huduma zake na kuwafikia wananchi katika maeneo yao. Hatua hii inasaidia sana katika kuiwezesha jamii kuripoti vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa wakati, kwa faragha na kujiamini zaidi hasa kwenye matukio ya ghafla yanayotokea katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, ofisi imeadhimisha siku ya kuzuia rushwa duniani ambayo ilijumuisha taasisi zote zinazosimamia maadili ya utawala wa umma. Katika kuadhimisha siku hii, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar imefanya makongamano yaliyowahusisha Vijana, Wakuu wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma, Waandishi wa Habari na Wananchi wa Wilaya ya Mkoani Pemba.

G08 – Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeendelea na ziara za ukaguziwa Taasisi za Umma. Ziara hizo zimeanza na zitaendelea katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na zimejumuisha Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya Unguja na Pemba. Vile vile, ziara hizo zitafanyika katika Ofisi za Tume nne za Utumishi za Zanzibar, ambazo ni Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi na Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ. Katika kushughulikia masuala ya Watumishi wa Umma, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imepokea na kuyatolea uamuzi Malalamiko manane na rufaa tatu za watumishi.

G09 – Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Naibu Spika, jumla ya nafasi za ajira 2,481 zimetangazwa katika wizara na taasisi mbali mbali kupitia *ZBC Redio* na Televisheni, kufanyiwa usaili kwa nafasi hizo na kutolewa kibali cha ajira kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, tume imewaongezea muda wa utumishi watumishi 24, watumishi 29 wamebadilishwa kada, na watumishi watatu wamepandishwa cheo. Pia tume imeidhinisha ajira ya mkataba kwa watumishi 13, likizo bila ya malipo kwa watumishi watatu, watumishi 32 wamestaafu kazi kwa hiari, watumishi 381 wamestaafishwa kazi kwa kufikia umri wa lazima na watumishi tisa wamestaafu kazi kwa maradhi.

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa kuchukua nafasi hii kutoa maelezo ya muelekeo wa programu zinazosimamiwa na ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejipanga kutekeleza vipaumbele vifutavyo:-

i. Kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Tunguu na jengo la Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar;
ii. Kuwezesha shughuli za serikali na utoaji wa huduma kufanyika kielektroniki;
iii. Kuendelea kutayarisha miongozo ya utumishi wa umma na kusimamia utekelezaji wake;
iv. Kutekeleza Programu ya Mabadiliko katika Sekta ya Sheria na Mabadiliko ya Utumishi wa Umma;
v. Kuimarisha usimamizi wa misingi ya utawala bora; na
vi. Kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Ofisi ya Mufti wa Zanzibar na Mahakama ya Kadhi.

Mhe. Naibu Spika, vipaumbele hivi vitaendana na Malengo Makuu ya Taifa (Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar – MKUZA III) pamoja na Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu na Sera za Kisekta. Pia, vipaumbele hivi vimezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015-2020, Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi 2010-2020 na Hotuba za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein wakati wa kampeni za uchaguzi 2010 na 2015.

Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na Utawala wa Sheria;
ii. Kuimarisha Miundombinu katika Sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
iii. Kuweka Miundo ya Taasisi na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa;

iv. Kuimarisha usimamizi wa masuala ya dini;
v. Kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;
vi. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika shughuli na utoaji wa huduma; na
vii. Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili katika utendaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jumla ya Programu kuu 13 na Programu ndogo 24. Kati ya programu hizo, zipo programu kuu tano na programu ndogo tisa zinazosimamiwa na kutekelezwa kupitia idara zilizo chini ya Katibu Mkuu; na programu 8 kuu na 15 ndogo zinatekelezwa na taasisi zinazojitegemea. Programu hizo zote zimegawika katika sehemu mbili kuu; ambazo ni utekelezaji wa majukumu ya msingi pamoja na shughuli za uendeshaji wa ofisi. Maelezo kamili ya mwelekeo wa programu hizo ni kama ifuatavyo:-

G01 – Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora(maelezo zaidi yanapatikana kuanzia kifungu cha 114 hadi kifungu cha 138)

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma inatekelezwa na programu ndogo mbili, Miundo na Mifumo ya Taasisi na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 programu hii itafanya yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Rasilimali Watu imepanga kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano 2017/2022, kuratibu na kusimamia vikao vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Wizara na vikao vya Maafisa Wadhamini wa Wizara za SMZ. Katika kuimarisha uwezo na uzoefu wa kiutendaji, ziara za kimafunzo na kuhudhuria mikutano ya kikanda na kimataifa itazingatiwa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa fursa zaidi za mafunzo kwa watumishi wa umma. Vile vile, mafunzo kwa maafisa utumishi juu ya Sera na Sheria za Utumishi wa Umma yatafanyika pamoja na kuendesha mafunzo kwa watumishi wanaotarajiwa kustaafu.

Mhe. Naibu Spika, programu ndogo ya Usimamizi wa Miundo, Mifumo na Maendeleo ya Watumishi imepanga kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa utoaji huduma kwa mteja katika Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nakutoa elimu ya upimaji utendaji kazi kwa wizara, mamlaka na taasisi zinazojitegemea.

Mhe. Naibu Spika, programu imeandaa mafunzo kwa watumishi wa umma juu ya masuala yanayohusu Sheria na Kanuni za Utumishi, kufanyia mapitio na kurekebisha viwango na taratibu za malipo ya posho katika Wizara na Taasisi za Serikali kulingana na miongozo iliyotolewa katika Sera za Malipo ya Watumishi wa Umma.

Programu ya Uimarishaji wa Mawasiliano ya Serikali

Mhe. Naibu Spika, ili kuwezesha dhana ya Serikali Mtandao ifanye kazi ilivyokusudiwa, afisi imejipangia kuanzisha dirisha la pamoja la mawasiliano ya serikali pamoja na kusimamia uanzishwaji wa tovuti zilizo hai katika taasisi za umma. Aidha, afisi imepanga kutengeneza mfumo wa usimamizi wa masjala (*registry management system*) ambao unahusu taratibu zitakazorahisisha mawasiliano ya barua ndani ya utumishi wa umma, na mfumo wa kumbukumbu na maombi ya vibali vya watumishi wa umma kusafiri nje ya nchi. Vilevile, Idara ya Serikali Mtandao itaratibu maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma. Kupitia hotuba hii ninazishauri Wizara na Taasisi za Serikali kuitumia afisi yetu ya Serikali Mtandao kwa kupata miongozo juu ya matumizi ya mifumo ya kielektroniki wanayotaka kuitumia katika shughuli na huduma zao wanazotoa kwa umma.

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika, pogramu ya Usimamizi wa Utawala Bora na Haki za Binadamu imepanga kuendelea kuinua uelewa wa jamii katika masuala ya utawala bora, kufanya kongamano la kitaifa la utawala bora, kutayarisha jarida la utawala bora na kufanya tathmini juu ya jinsi ambavyo wananchi wanaelewa dhana ya utawala bora.

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

Mhe. Naibu Spika, afisi imepanga kukamilisha Muundo wa Ofisi ya Mufti na kuimarisha idara na vitengo vyake ili vikidhi mahitaji ya jamii na viendane na technolojia ya wakati tulionao. Aidha, kuimarisha shughuli za utoaji taaluma na miongozo ya dini ili kushikamana na maadili ya Kiislamu na kuwajengea uwezo viongozi wa kiislamu katika majukumu yao ya msingi na usuluhishi.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uongozi na Utawalaimepanga kutengeneza Kituo cha Kuhifadhia kumbukumbu tuli za afisi, kuendelea kuwajengea uwezo watumishi 15 kwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 160 kwa mafunzo ya muda mfupi na yale ya ndani ya afisi (in house training) ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, Idara imepanga kuimarisha usalama wa majengo, watumishi na wataka huduma kwa kuweka mfumo wa *CCTV Camera* na upimaji wa afya za watumishi, kuimarisha matumizi ya miongozo ya kiutumishi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na ununuzi wa vifaa vya Ofisi na kutoa huduma za Uendeshaji wa afisi.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu ya Mipango, Sera na Utafiti, afisi itaendelea kuratibu mipango, taarifa za utekelezaji na kufanya mapitio ya utekelezaji wa sera na sheria zinazosimamiwa na afisi, ikiwemo Sera ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sera ya Msaada wa Kisheria, Sera ya Nyaraka, Sera ya Mafunzo, Sera na sera ya lipo na Sera ya Serikali Mtandao. Aidha, Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria, Mabadiliko katika Utumishi wa Umma na ule wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi itaendelea kufanyiwa kazi. Misingi ya ufuatiliaji na tathmini na suala la kukusanya na kutumia takwimu sahihi ni miongoni mwa

mambo ya kipaumbele. Aidha, Idara itaratibu tafiti katika Sekta za Utumishi wa Umma, Katiba, Sheria na Utumishi wa umma.

Mhe. Naibu Spika, programu ya kuratibu shughuli za Afisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Pemba imepanga kuendelea na kuratibu shughuli za afisi, kutoa huduma za uendeshaji wa ofisi, kusimamia watumishi wa umma kwa kuwajengea uwezo zaidi na kuondokana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea. Programu hii pia imepanga kutoa elimu dhidi ya mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia, rushwa na uhujumu wa uchumi na kusimamia dhana ya Utawala Bora pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wa Ofisi Kuu Pemba.

Taasisi Zinazopokea Ruzuku

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Naibu Spika, Program hii imepanga kuimarisha utoaji wa huduma za mirathi, ustawishaji wa mali za wakfu na amana na uratibu wa shughuli za Iddi, Hijja na misaada ili zikidhi mahitaji ya wakati tulionao. Aidha, imelenga kuimarisha zaidi mawasiliano, mazingira ya kazi na ufanisi wa watendaji.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kimepanga kuandaa na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma na watumishi wa sekta binafsi, kuandaa na kutoa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wanaoingia katika ajira kwa mara ya kwanza, kufanya tafiti katika utumishi wa umma na kutoa ushauri elekezi na kuandaa na kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wa umma na wananchi wengine.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imepanga kupokea, kuhifadhi na kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma, kufanya uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa viongozi wa umma, kuelimisha viongozi wa umma na wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili, kuadhimisha Siku ya Maadili Duniani, kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo na kushiriki katika mikutano ya kimataifa, kikanda na kitaifa kuhusu maadili na uadilifu.

Mhe. Naibu Spika, ili kuziwezesha programu zilizochini ya Fungu G01 kutekeleza majukumu yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 8,909,000,000.00 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 3,225,800,000.00 kwa matumizi ya mishahara, shilingi 2,283,500,000.00 kwa matumizi mengineyo, shilingi 2,349,700,000.00 ni ruzuku na shilingi 1,050,000,000.00 kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. Naomba pia Baraza lako likubali Fungu G01 lichangie shilingi 50,589,000,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

(Mchanganuo wa Idara na Taasisi za Fungu G01 unapatikana katika viambatanisho 2,3, na 5).

G02 – Mahakama

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki, Mahakama imepanga kuendelea na jukumu lake kuu la usikilizaji wa kesi na utoaji maamuzi kwa wakati, kuhakiksha mfumo wa kisasa wa kuendesha na kurikodi kesi unaimarika na kuendelea kujenga na kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 6,725,200,000.00. Kati ya fedha hizo Mahakama imepangiwa kutumia shilingi 5,611,400,000.00 ambapo shilingi 4,096,300,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,515,100,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 5,000,000,000.00 zimepangwa kutumika kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi 659,910,000.00 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ya Kadhi imepangiwa kutumia shilingi 1,113,800,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka serikalini. Kati ya fedha hizo shilingi 878,800,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 215,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. *(angalia kiambatanisho nam. 2,3 na 5).*

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Mageuzi ya Utoaji Huduma za Sheria itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuishauri serikali masuala ya kisheria ikiwemo kuandaa mikataba ya kitaifa na kimataifa, kutayarisha miswada ya sheria, kusimamia mashauri ya madai kwa niaba ya serikali na kuandaa hati na nyaraka za kisheria. Aidha, inatarajia kuanza rasmi kupeleka wanasheria katika Afisi ya Pemba mara baada ya kukamilika kwa utaratibu wa ajira.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 2,027,400,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 730,200,000.00 mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,297,200,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. *(Tuangalie kiambatanisho nam. 2).*

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai imepanga kuendesha na kusimamia kesi za jinai, kukuza mipango na uendeshaji wa Afisi na kukiendeleza Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti. Aidha, afisi imejipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria mpya ya adhabu na sheria ya mwenendo wa jinai ili kujenga uelewa wa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 2,705,100,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,586,400,000.00 kwa matumizi mengineyo na shilingi 1,098,700,000.00 kwa matumizi ya

mishahara na stahiki za watumishi. Aidha, shilingi 20,000,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka serikalini kwa Kituo cha Mafunzo ya Sheria. *(angalia kiambatanisho nam. 2).*

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria za Zanzibar imepanga kuzifanyia mapitio sheria tano, Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai Sura 8/1917, Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana namba 2/2007, Sheria ya Mahusiano Kazini namba 1/2005, Sheria ya Ajira namba 11/2005 na Sheria ya Watu Wenye ulemavu (Haki na Fursa Sawa) namba 9/2006. Aidha, utafiti na uchambuzi wa Matumizi ya Sheria za Zanzibar utafanyika na kuandaa ripoti, sheria zitatafsiriwa kwa lugha nyepesi naelimu kwa umma itatolewa.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,045,200,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 304,700,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 740,500,000.00 kwa matumizi mengineyo. *(angalia kiambatanisho nam. 2).*

G06 – Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu ya Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma, afisi itaendelea kukagua hesabu za serikali na taasisi zake zote kwa kutumia viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa, sambamba na kuimarisha uwezo wa watumishi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 3,022,200,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 1,472,200,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,550,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 50,954,000.00 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya serikali. *(angalia viambatanisho nam. 2 na 3).*

G07 – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imepanga kuendelea na shughuli za uchunguzi wa makosa mbali mbali ya rushwa, kukamilisha Mpango Mkakati wa Mamlaka, kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa mamlaka.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,590,800,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 876,000,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi, shilingi 614,800,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 100,000,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka serikalini *(angalia kiambatanisho nam. 2).*

G08 – Kamisheni ya Utumishi wa Umma

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kusimamia Utumishi wa Umma kwa kufanya ziara za ukaguzi na ufuatiliaji wa shughuli za Taasisi za Umma na kuzishauri taasisi hizo juu ya namna bora ya kutekeleza shughuli kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma. Aidha, mapitio ya miongozo ya kuandaa Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumishi yatafanyika. Ofisi itachapisha na kusambaza Matoleo, itaandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka 2017/2018 na kuishauri Serikali juu ya njia za kuimarisha Utumishi wa Umma ili kuleta ufanisi.

Vile vile, itapokea na kushughulikia rufaa na malalamiko, ya watumishi, Mamlaka za Nidhamu na Mamlaka za Rufaa na kuyafanyia kazi Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumishi kadiri yatakavyopokelewa. Kamisheni pia itafanya tathmini ya uwezo wa kiutendaji ili kubaini uimara na udhaifu wake, pamoja na kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa kazi za kamisheni ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kamisheni.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 1,033,000,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 380,200,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 652,800,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo *(angalia kiambatanisho nam. 2).*

G09 – Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini imepanga kuandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, kuendelea kusimamia haki na nidhamu za watumishi serikalini ikiwa ni pamoja na kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi, kusikiliza rufaa za watumishi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa tume, kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kutoa nyongeza za muda wa utumishi, likizo bila ya malipo, kustaafisha kisheria watumishi serikalini na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wa Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Naibu Spika, ili kuiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi 529,200,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 189,100,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 340,100,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. *(angalia kiambatanisho nam. 2).*

SHUKURANI

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, kwa mara nyengine naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Naomba niwashukuru kwa dhati wahusika na washirika mbali mbali wa maendeleo kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala

Bora ambao umerahisisha utekelezaji wa malengo tuliojipangia. Miongoni mwao ni Jumuiya ya Ulaya (*EU*), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (*UNDP*), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (*UNFPA*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuzuia Uhalifu na Madawa ya Kulevya (*UNODC*), Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (*AAPAM*), Benki ya Dunia, Afrika Muslim Agency na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Benki ya Maendeleo ya Kiislam (*IDB*), Mamlaka ya Wakfu wa Uturuki, Wizara ya Awkaaf ya Algeria, Serikali ya Saudi Arabia, Taasisi ya *Red Crescent* ya Uturuki, Taasisi ya *World Monument Fund*, Taasisi zinazosafirisha mahujaji na taasisi za misaada ya kheri Zanzibar. Aidha, tunawashukuru *Save the Children*, nchi ya China, India, Korea, Japani, Indonesia, Uingereza, Marekani, Afrika ya Kusini, Oman, Uturuki na Misri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namshukuru kwa moyo wangu wote Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Khamis Juma Mwalim, Katibu Mkuu Ndugu Yakout Hassan Yakout, Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma, Ndugu Seif Shaaban Mwinyi na Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Katiba, Sheria na Utawala Bora Ndugu George Joseph Kazi, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya afisi yetu katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mhe. Jaji Mkuu, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mufti wa Zanzibar, Kadhi Mkuu, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Mkurugenzi wa Mashtaka, Wenyeviti, Makamishna na Wajumbe, na Watendaji Wakuu wa Tume zinazosimamiwa na afisi, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa utendaji na ushirikiano wao wanaonipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya uwaziri kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, afisi pia inatoa shukrani kwa vyombo vinavyosimamia Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wao mwema. Vile vile, tunatoa shukrani za dhati kwa Chama cha Wanasheria Zanzibar (*ZLS*), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (*ZLSC*), Chama cha Wanasheria Wanawake (*ZAFELA*), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (*TAMWA*) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar. Aidha, shukrani zetu ziwaendee masheha na wananchi wote kwa jumla. Mwisho navishukuru sana vyomba vyetu vya habari kwa kazi nzuri walioifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yanayohusu shughuli za afisi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla naomba niwashukuru wote walioisaidia Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Shukrani zangu za dhati ziwaendee pia watumishi wote wa umma kwa kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, napenda kuwahakikishia washirika wetu wote kwamba, afisi itaendelea kuthamini kwa dhati michango yao ya hali na mali pamoja na ushirikiano wanaotupatia kila tunapowahitaji. Hatuna cha kuwalipa zaidi ya kusema ahsanteni sana. Tunawathamini sana na tunashukuru wote. Kwa niaba ya Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala

Bora na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tunaomba mzipokee shukrani zetu, ahsanteni na Mungu awabariki. *(Makofi)*

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumalizia hotuba yangu hii, naomba nikumbushe kuwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jukumu la kuhakikisha kuwa huduma kwa wananchi, upatikanaji wa haki kwa wakati, utawala bora na masuala ya dini yanasimamiwa ipasavyo. Kwa mnasaba huo, Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria, Mkakati wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma na Mkakati wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ni nyenzo muhimu zitakazotuwezesha kufikia malengo ya MKUZA, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu Duniani.

Mhe. Naibu Spika, naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora jumla ya shilingi 27,587,100,000.00 kwa matumizi ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, shilingi 15,126,000,000.00 kwa matumizi ya mishahara, shilingi 11,411,100,000.00 kwa matumizi mengineyo na shilingi 1,050,000,000.00 kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. Naomba pia Baraza lako likubali Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ichangie shilingi 761,453,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *(angalia kiambatanisho nam. 2&5).*

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

HAPA TABLE ZAKE

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Naibu Spika, naafiki

(Hoja imetolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa, nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Makame Ali: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma hotua ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusiana na Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Tisa, Mkutano wa Kumi kwa lengo lilelile la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, Mhe. Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa ufanisi na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha demokrasia katika chombo hiki muhimu cha wananchi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu hali inayopelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman pamoja na Naibu wake Mhe. Khamis Juma Mwalim pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja Afisa Mdhamini Pemba bila ya kuwasahau watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Nadir Abdul – latif Yussuf	Mjumbe

4.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
5.	Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	Mjumbe
6.	Mhe. Ali Khamis Bakar	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
8.	Nd. Ali Alawy Ali	Katibu, na
9.	Nd. Haji Jecha Salim	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo mfupi sasa naomba nichukue fursa hii adhimu kutekeleza jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako Tukufu moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum inatoa pongezi kwa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuiwezesha Mahakama ya Kadhi katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kuipangia ruzuku yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa Sheria mpya ya Mahakama ya Kadhi inatekelezwa ipasavyo. Vile vile, Kamati inapongeza mazingatio yaliyotolewa kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuiwezesha kufanya kazi kama tume nyengine za aina hiyo. *(Makofi)*

Pia, kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanapatiwa mafunzo yanayohusiana na kazi na majukumu yao mara tu wanapoajiriwa na wakati wakiwa kazini kama ilivyo katika Kanuni za Utumishi wa Umma, ili kuwawezesha kumudu majukumu yao.

FUNGU G01: OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina jumla ya Programu kuu tano (5) na Programu ndogo kumi (10), ambazo katika mwaka wa fedha 2018/2019 inategemea kuzitekeleza licha ya kuwepo kwa changamoto mbali mbali ambazo zinarudisha nyuma jitihada zao, miongoni mwa changamoto hizo ni uhaba na ubovu wa baadhi ya afisi zake kama vile majengo ya Mahakama mbali mbali Unguja na Pemba, uhaba wa vyombo vya usafiri na uhaba wa vitendea kazi katika sehemu mbali mbali.

Aidha, Kamati inashauri kwa mwaka wa fedha 2018/2019 serikali kuelekeza juhudi katika kuhakikisha wizara hii imepatiwa vyombo vya usafiri na majengo ya kisasa ya afisi ingawa juhudi hizo zimeanza kuonekana kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena, kamati inaiomba serikali kufanya juhudi za pekee katika kupatiwa *vote* (fungu) lake kwa Afisi ya Mufti Zanzibar kama zilivyo taasisi nyengine za serikali licha ya changamoto mbali mbali zinazoelezwa ambazo kimsingi kwa serikali hazileti athari yoyote.

FUNGU G02: MAHAKAMA

Mhe. Naibu Spika, Mahakama ni miongoni mwa mihimili mikuu ya nchi inayotarajiwa kuimarisha na kuongeza upatikanaji wa haki, kuheshimu utawala wa sheria, kuzingatia haki za msingi za binadamu na ushirikishwaji wa shughuli za demokrasia nchini pamoja na kujenga

misingi imara ya Utawala Bora. Aidha, katika kuhakikisha kuwa sekta ya sheria inaimarika nchini, mambo mbali mbali yanafanyika ikiwemo kuandaa miongozo ya mahakama na sera ya matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa kesi ambapo tayari imeanza kutumika.

Aidha, kamati inapongeza juhudi za ukarabati wa majengo ya mahakama pamoja na matayarisho ya ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Tunguu ambayo yamefanyika, hatua ambazo zinaashiria kuongezeka kwa upatikanaji wa haki nchini. Vile vile, kamati inatoa pongezi kwa afisi ya Mahakama kwa kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Mahakama ya Mwanakwerekwe ambalo lilikuwa katika hali mbaya.

Mhe. Naibu Spika, kamati katika vipindi tofauti wakati wa ziara zake za ufuatiliaji wa shughuli za wizara inazozisimamia, ilitembelea baadhi ya Mahakama Unguja na Pemba na kukutana na changamoto nyingi ikiwemo ubovu wa majengo katika Mahakama ya Wete, Konde, Mfenesini na Mkokotoni. Vile vile, changamoto nyengine kubwa ni ukosefu wa vyombo vya usafiri pamoja na kukosekana kwa makabati ya kuhifadhia nyaraka ambapo katika baadhi ya Mahakama nyaraka zimekutikana zikiwa zimeanza kupotea na kuharibika kwa kuliwa na mchwa au kunyeshewa na mvua na kupelekea kuharibika kwa nyaraka hizo muhimu.

Hata hivyo, kamati inashauri katika mradi mkubwa wa mahakama ambao unatarajiwa kutekelezwa katika kujenga Mahakama Kuu Tunguu kuanzia Bajeti hii ya mwaka 2018/2019, serikali pia ifikirie mpango wa kujenga upya Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba iliyopo Wete au kufanyiwa ukarabati utakaonyanyua hadhi ya mahakama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati inashauri katika bajeti hii ya 2018/2019 Ofisi ya Mahakama kuhakikisha wametumia vyema rasilimali walizonazo katika kuendeleza ukarabati wa majengo yao hususan Mahakama ya Konde Kisiwani Pemba na Mahakama ya Mkokotoni Kaskazini Unguja.

Aidha, kamati imeridhishwa na programu zote zinazotarajiwa kufanywa na Mahakama katika mwaka wa fedha 2018/2019. Hata hivyo, Kamati inatoa msisitizo zaidi kwa Mahakama kuzingatia utatuzi wa changamoto zake ambazo zinawakabili katika kujenga mazingira rafiki ya kazi kwa watendaji wake pamoja na kushughulikia tatizo la uhaba wa vyombo vya usafiri kunakopelekea kutotekeleza vyema majukumu yao.

FUNGU G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake, kuandaa Miswaada, Kanuni na matangazo ya kisheria pamoja na kuiwakilisha serikali Mahakamani kwenye kesi zote za madai. Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika mwaka wa fedha 2018/2019 imedhamiria kutekeleza programu kuu mbili (2) ambazo zimewekwa, ili kuimarisha maendeleo ya Haki na Sheria Nchini.

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar imeweka program ndogo ya Kutoa Ushauri wa Kisheria, Kutayarisha na Kusimamia Mikataba ya Serikali; programu

ambayo kimsingi utekelezaji wake unatimiza lengo kuu la kuanzishwa kwa afisi hii katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, kamati inasikitika sana kuona zipo baadhi ya aasisi za serikali huandaa mikataba kutoka hatua za awali hadi kukamilika kwake bila ya kuishirikisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu na hatimaye hufika pahala wakashindwa katika utekelezaji wa mikataba hiyo na hivyo kuisababishia hasara kubwa serikali kutokana na ubovu wa mikataba hiyo na vile kupelekea wananchi kupoteza haki zao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika utekelezaji wa programu hii, kuhakikisha imewatia hatiani wale wote wenye kusimamia au kuratibu utengenezaji wa mikataba mibovu katika taasisi za serikali ili kudhibiti upatikanaji wa hasara usiotarajiwa lakini vile vile kupelekea baadhi ya wananchi kupoteza haki zao.

Aidha, Kamati inaipongeza sana Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kutekeleza ipasavyo majukumu yake, na inaishauri afisi hii kuhakikisha kuwa imeandaa utaratibu maalumu wa kuiwasilisha Miswada Baraza la Wawakilishi na utaratibu huo utatekelezeka endapo itaandaa mpango maalumu wa kuzitaka wizara na taasisi zinazodhamiria kutoa miswaada kutayarisha miswada yao mapema na kwa kufuata maelekezo kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili kuepusha matatizo ambayo hupelekea kukosa ubora kwa miswada hiyo na vile vile kukosa muda wa kutosha katika uandaaji wake inapofika Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa.

FUNGU G04: OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka miongoni mwa majukumu yake ni kuendesha mashtaka Mahakamani, kutoa ushauri wa kisheria na maelekezo juu ya haki za jinai. Afisi hii inatarajia kuongeza upatikanaji wa haki, kuheshimu utawala wa sheria, kukuza haki za binadamu na kukuza ushiriki wa kidemokrasia nchini. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imedhamiria kuendesha kesi za Jinai, kusimamia kesi za jina pamoja na kuendesha operesheni maalum dhidi ya Makosa ya Udhalilishaji na Dawa za Kulevya katika kuhakikisha program zote hizi zinahitaji fedha za kutosha kwa ajili ya kufikia malengo waliyokusudia.

Aidha, kamati inaipongeza kwa dhati Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa juhudi zake za kuiwakilisha serikali katika kesi za jinai na kupelekea kupungua kwa mrundikano wa kesi Mahakamani hususani kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto, ambazo katika kipindi cha hivi karibuni matendo hayo yameongezeka mara dufu. Vile vile, kamati inaishakuru sana Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuona iko mstari wa mbele katika kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na kutoa msaada mkubwa wa kisheria katika kuhakikisha wamewatia hatiani wale wote wenye kujishirikisha na matendo hayo maovu.

FUNGU G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ina jukumu kuu la kufanya mapitio ya sheria nchini ambapo imedhamiria kuzifanyia sheria mbali mbali mabadiliko, ili ziendane sambamba na mabadiliko ya mazingira na wakati.

Kamati imeridhishwa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kazi nzuri wanazozitekeleza katika kipindi hiki ambapo baadhi ya sheria zimeshafanyiwa mapitio na kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa, kwa hakika tume imefanyakazi nzuri sana katika mwaka wa fedha 2017/2018.

FUNGU G07: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI (*ZAECA*)

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ni Taasisi yenye jukumu la kuhakikisha makosa yanayohusiana na rushwa na uhujumu wa uchumi yanapungua nchini. Aidha, mamlaka hii inatarajia kuhakikisha kwamba Mfumo wa Utawala Bora na Muundo wa Serikali unakuwa wazi na wenye uwajibikaji na kupingana na vitendo vya rushwa. Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa ambazo zinarudisha nyuma juhudi za watumishi wa afisi hii Unguja na Pemba.

Hata hivyo, kamati inashauri kupitia bajeti hii, serikali kuhakikisha inasaidia juhudi za Taasisi ya *ZAECA* kwa kupatiwa vyombo vya usafiri hususani Afisi za Pemba ambazo zinatumia gari moja tu Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limekua changamoto na hivyo kuathiri utendaji wao na kukosa ufanisi katika maeneo yao ya kazi.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri mamlaka hii kuhakikisha kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ihakikishe inatumia vizuri fedha itakazoidhinishwa katika kuielimisha jamii, ili iweze kusaidia kupunguza tatizo la rushwa na uhujumu wa uchumi ambao ni adui mkubwa wa haki, utawala bora na maendeleo ya nchi. Aidha, kamati inaipongeza taasisi kwa wazo lao la kujenga afisi mpya ya Makao Makuu ya Taasisi hiyo.

FUNGU G08: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Utumishi wa Umma miongoni mwa program zake ni Usimamizi wa Utumishi wa Umma na Usimamizi wa Nidhamu na Maadili ya Utumishi wa Umma. Aidha, kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya baadhi ya watumishi wa Umma kushindwa kuzielewa kikamilifu Kanuni za Utumishi na hivyo kupelekea kupotea kwa nidhamu za kiutumishi katika maeneo yao ya kazi, hali ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa uwajibikaji wao kazini.

Sambamba na hayo, kamati inashauri kupitia bajeti hii, Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuaanda utaratibu maalumu juu ya ufuatiliaji na usimamizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

FUNGU G09: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Mhe. Naibu Spika, Kwa kuwa, Tume ya Utumishi Serikalini ina wajibu na jukumu la kusimamia watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na tume nyengine za kiutumishi, kamati inaomba kuzidi kusimamia watumishi wa serikali katika kuhakikisha wamepata haki zao zote za msingi sambamba na kuimarika kwa maslahi yao ya msingi. Vile vile, kamati inashauri tume hii kusimamia kikamilifu na kuona kwamba watumishi wa serikali

wanapatiwa fursa zaidi za kujiendeleza kielimu kwa misingi kwamba elimu bora ndio msingi wa maendeleo katika taasisi yoyote katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Pia, Tume ya Utumishi Serikalini inalo jukumu la kusimamia uajiri kwa watumishi wapya wakati serikali itakapoona ipo haja ya kufanya hivyo. Hivyo, kamati inaishauri tume inapotangaza nafasi za ajira kwa kuzingatia vigezo ilivyoweka kisheria, basi izingatie sana muda, kwani baadhi ya wakati hutoa matangazo ya ajira na waombaji kuomba kwa wakati mahususi lakini majibu kwa waombaji hao huchukua muda mrefu sana kiasi kwamba hufikia huwakatisha tamaa wale waliwoomba nafasi hizo. Hivyo, Kamati inaishauri, Tume ya Utumishi Serikalini, endapo itatangaza nafasi za ajira wazingatie muda wa tangazo hilo na wakati ambao majibu yatatolewa bila kupoteza muda.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu kwa niaba ya kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu. Aidha, kamati yangu inawaombea Waislamu wote wa Zanzibar na Ulimwenguni kote kwa ujumla mfungo mwema wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, tunamuomba Mwenyezi Mungu aujaalie uwe mwezi wenye kheri na baraka nyingi kwa Waumini wote wa Dini ya Kiislam. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika, mwisho kabisa, kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie bajeti hii na hatimae waidhinishie Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya kamati yangu naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Utawala Bora na Idara Maalum. Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (*PAC*)): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kusoma maoni ya kamati ya juu ya hotuba uliyozungumza Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2018/2019. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba Mbingu na Ardhi kwa kutujaalia uzima na afya na kutuwezesha kuendelea kujadili bajeti za wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na leo hii tukiwa tunajadili bajeti ya nne kati ya Wizara kumi na nne zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, shukurani zangu za dhati zimwendee Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na watendaji wengine wa wizara hii pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia wakati kamati hii ilipokuwa inachambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya *PAC*, kwa umahiri na umakini wao mkubwa wa kuyachunguza na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Pongezi na shukrani hizi pia ziende kwa Makatibu wa Kamati hii kwa ushauri na maelekezo yao ya kitaalamu yaliyowawezesha Wajumbe wa Kamati kutekeleza jukumu lao hili la kupitia bajeti ya ofisi hii kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu wao huo, kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya *PAC* kama ifuatavyo:

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamu Mwenyekiti.
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Mjumbe
4. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
7. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
8. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Naibu Spika, Kiujumla Kamati ya *PAC* imeridhika na utendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ingawa ofisi hii ndio kwanza imekamilisha ukaguzi kwa mwaka 2015/2016 wakati tupo katika mwaka 2018/2019.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* imediriki kulisema hili kwani wakati inatekeleza majukumu yake hupata wakati mgumu wa kufuatilia ripoti hizo hususan kwa kuwa mapato na matumizi yanayofuatiliwa ni ya miaka ya nyuma sana na asilimia kubwa ya wasimamizi wa fedha hizo ama wameshafariki au hawafanyi tena kazi katika taasisi hizo, kitendo hiki hupelekea kamati hii kupata taarifa ambazo hazina uhakika.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kasoro hiyo Kamati ya *PAC* inaiomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuzidisha juhudi ya kutekeleza jukumu lake hilo la msingi ili iweze kufanya ukaguzi ambao hautopishana sana na mwaka wa fedha husika.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, Kamati ya *PAC* inaendelea kushangazwa kwa kuwa kwa kipindi kirefu sasa Ripoti za Ukaguzi wa Miradi na Programu za Maendeleo, zikiwemo za ujenzi hazijawasilishwa Barazani. Hali hii inaipa wasiwasi sana kamati hasa kwa kuwa fedha nyingi za umma zinaendelea kutumika katika miradi hiyo bila ya wasimamizi wa serikali kupata fursa ya kuzikagua.

Mhe. Naibu Spika, hivyo, Kamati inaiomba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya juhudi maalum za kuhakikisha kuwa ukaguzi wa Miradi na Programu za Maendeleo

zinakamilishwa na Ripoti zao kuwasilishwa Barazani kama matakwa ya Katiba na Sheria yanavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* inaishauri Ofisi ya Mkaguzi kuendelea kuyafanyia ukaguzi Mashirika ya Umma kila mwaka kwani imebainika kuwa baadhi ya mashirika hukaguliwa kwa mkupuo kwa kisingizio kuwa Mashirika hayo hayana fedha za kulipia ada ya ukaguzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla naomba sasa nielekee moja kwa moja kwenye shughuli inayotukabili kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati ya *PAC* ilipokuwa ikichunguza na kupitia Fungu la Ofisi hii (G 06), ilibaini mambo yafuatayo ambayo yalikubalika kufanyiwa marekebisho:

i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi iingiziwe shilingi 994,954,000 badala ya 1,667,387,000; na
ii. Programu Ndogo ya Udhibiti na Ukaguzi Pemba iingiziwe shilingi 672,433,000 badala ya kutotengewa fedha kama ilivyoainishwa hapo awali.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* ilipendekeza hili baada ya kugundua kuwa katika vitabu vya bajeti vya mwaka wa fedha 2016/2017 na mwaka 2017/2018 vimeonesha kuwa Programu Ndogo ya Udhibiti na Ukaguzi Pemba inapaswa kutengewa fedha.

Mhes. Naibu Spika, kamati imeshtushwa na kiasi kidogo cha fedha za mapato kilichokusanywa na Ofisi hii, kwani Ofisi ya Mdhibiti ilikadiriwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kukusanya jumla ya shilingi 84,555,000, hata hivyo, hadi tunaipitishia bajeti ofisi hii iliweza kukusanya shilingi 22,000,000 sawa na asilimia 26 tu.

Mhe. Naibu Spika, kiwango hiki cha mapato ni kidogo sana, hivyo, Kamati ya *PAC* inaziomba Taasisi zote za Serikali ambazo zimeshafanyiwa ukaguzi kulipa ada ya ukaguzi kwa wakati ili Ofisi hii iweze kufikia malengo yaliyopangwa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya *PAC* inaipongeza serikali kwa kuiongezea fedha za matumizi Ofisi ya Mdhibiti katika mwaka ujao wa fedha ambapo kwa upande wa matumizi ya mishahara na maposho jumla ya shilingi 381,236,565 zimeongezeka.

Mhe. Naibu Spika, ni matarajio yetu kuwa kiwango hicho cha fedha kilichoongezeka kitakuwa ni chachu ya kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti kuongeza idadi ya wakaguzi kwa kuajiri watendaji hao na kuweza kufanya ukaguzi kwa wepesi na kutoa angalau ripoti mbili ndani ya mwaka mmoja.

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (*PAC*), imeyaridhia na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa upekee kabisa, naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu, kwa utulivu wao waliouonesha wakati wote nilipokuwa nawasilisha hotuba hii. Ni matarajio yangu kuwa, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza wameifahamu vyema bajeti ya Ofisi hii na watatoa michango yao yenye tija kwa manufaa ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wananchi wote kwa ujumla.
Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwasilisha ripoti ya kamati naomba na mimi unipe muda kidogo nichangie ya kwangu mimi mwenyewe binafsi kama Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe,

Mhe. Naibu Spika: Nimekuruhusu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru na Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kunijaalia nguvu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ikiwa leo ni mwezi mosi Ramadhani nitamuomba Mwenyezi Mungu sana anijaalie ulimi mwepesi, ili yale nitakoyoyasema isiwe kero kwa wenzangu watakaoweza kunisikiliza.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu nitakwenda katika suala zima katika ukurasa wa kumi masuala ya kidini. Kwanza ifahamike kwamba sasa hivi imekuwa ni bajeti yangu ya tatu katika chombo hichi kila nikisimama nazungumzia hali halisi ya malalamiko ya wananchi wangu au waajiri wangu wa Jimbo la Jang'ombe juu ya kadhia yao ya Msikiti wa Shurba, Mhe. Makamu wa Rais ambaye Mtendaji Mkuu ametoa maelekezo, nimejaribu kuyafanya kwa asilimia tisini, lakini mpaka dakika hii sijapata mustakabali mzima juu ya kadhia ile pale.

Kwa wananchi wa Jang'ombe kama mimi mtumishi wao walifikia kunitamkia kwamba hivi sasa wako tayari waanze kugawana majengo ya serikali aidha wengine wende *morchary* wengine wende jela kwa kadhia nzima ya msikiti ule pale wa Jang'ombe msikiti wa Shurba ambao umejengwa kwa majili ya mbadala ya Msikiti wa Hidaya ule uliozama pale. Kwa mfano, tukitilia maanani hata warka wa msikiti ule wa mwanzo kuanzia maombi ya kiwanja mpaka ujenzi ule unasomeka Hidaya.

Lakini cha kustaajabisha baadae warka ule umekwenda kubadilishwa umetiwa ilo jina Masjid Afraa, ambao wale wasimamizi wa msikiti ule pale hawana taarifa hizo. Inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nakutana na waziri anayehusika si mara moja si mara mbili si mara tatu akanipa maelekezo nikayafanya, lakini mpaka dakika hii bado hajatoka mustakabali juu ya nini kifanyike juu ya kazia ile pale ya msikiti ule pale wa Jang'ombe.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Makamu wa Rais namheshimu sana nakuthamin sana pamoja na maelekezo yake ninayafuata, lakini baadhi ya wetendaji wanatuangusha katika hilo. Kwa kweli, sikusudii kusema maneno makali, lakini inabidi tuzungumze ili tuone namna gani wale wananchi wetu wa Jang'ombe tuone haki yao ile wameipata. Imefikia hatua kipindi hichi hata wale vijana ambao waliokuwa wanasoma chuo mle ndani wamefukuzwa ni wananchi wa Jang'ombe, Kidongochekudu, Jang'ombe na Urusi, hawa ni wapiga kura wangu wazee wao na mimi kama mwana-Jang'ombe ni ndugu zangu inasikitisha hali ya juu.

Kipindi kilichopita nilisema humu laitani ingelikuwa msikiti ule ni wa Makunduchi, basi ingekuwa tatizo lishatatuliwa lakini kwa kuwa msikiti ule ni wa Jang'ombe bado mpaka dakika hii tunaendelea kulia. Mhe. Naibu Spika, nitaendelea kulia mpaka Mwenyezi Mungu atakaponiondosha duniani au atakaponitoa ndani ya Baraza hili sitonyamaza, haki yetu Jang'ombe kama Jang'ombe tupatiwe juu ya msikiti ule pale.

Msikiti ule inasemekana kwamba kuna mtu mjenzi aliachiwa kujenga msikiti ule ndio alihodhi yeye baada kuona kwamba mbele kuna mardi biashara inampatia yeye chejio, na baadhi ya watu wangu wamekuwa wanasema kwamba hata kuna mpango wa mrungura kutoka au rushwa kwamba ili haki icheleweshe kwa wananchi wa Jang'ombe lakini iko siku itafika. Nimesubutu kusema haya kwa sababu roho inauma na inaumiza sana kila siku panda shuka kupitia Ofisi ya Wizara ya Ardhi na Ofisi ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu kadhia ile ya msikiti wangu wa Jang'ombe, nishakwenda si mara moja si mara mbili na wazee wa msikiti ule pale lakini mpaka dakika hii ninavyozungumza bado haki ile ya Jang'ombe haijarudishwa.

Pamoja na agizo kuzungumza na mwenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Sheni akaniambia kwamba kashampa maelekezo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora mwambie mmalize, lakini mpaka leo hii haijamalizika tatizo nini na kumekwamba wapi. Mhe. Naibu Spika, naomba sana katika hili sitokuwa tayari kuliwachia fungu la Diwani lipite hivi bila ya mustakabali wa mahsus kuhusu msikiti wetu wa Jang'ombe tunayo haki basi tupewe haiwezekani ule msikiti uvunjwe tutafutiwe mfadhili mpya aje atujengee msikiti wenye hadhi na sisi.

Nilitaka niseme hilo kwanza wakati pili nikiendelea katika ukurasa wangu wa kifungu 51 suala zima la chuo cha *IPA* awali ya yote nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar jana tu….

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Abdalla Maulid Diwani, tunao utaratibu hapa wa kupishana kwa sababu tunaanza saa tatu tunamaliza saa tisa na nyinyi nyote mnafahamu kwamba kuwepo hapa kwa muda wa masaa mengi kiafya sio sahihi kabisa. Kwa hivyo, tuwe na utaratibu huo wa kupishana hasa katika mwezi huu wa Ramadhani kwa hivyo, naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma aweze kuja kuendelea na shughuli yetu hii ya leo.

(Hapa Mwenyekiti, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea namuomba Mhe. Abdalla Maulid Diwani aendelee.

Mhe. Abdalla Diwani: Ahsate sana Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa naendelea kwenye kifungu 51 Chuo cha Utawala wa Umma *IPA*. Nimesema namshukuru sana na nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa majaliwa aliyoweza kutuchaguliwa ndugu yetu Dkt. Mwinyi Talib kuwa Mkuu wa Chuo kile pale hongera sana Mhe. Rais wa Zanzibar, najua siku zote Mhe. Rais wa Zanzibar katika uteuzi wake hafanyi makosa, anamini kwamba vijana sasa tumeweza na nikweli tutakudhihirishia kwamba tunaweza ili ujenge imani zaidi na sisi. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo siku mbili tu zilizopita imekuja kadhia ya kusimishwa udahili hivi vyuo na hili suala linakuwa lina muda mrefu mara kwa mara kila mwaka sijui tatizo nini. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuweke wazi kidogo, ili wale wanafunzi wetu tunaowapeleka pale wasiwe wanahangaika kwa sababu wapo chuoni mara inakuja taarifa inaletwa kwamba wanafuta udahili wa vyuo hivi wakati watu washatumia gharama zao wazee wao washawasomesha pale pesa nyingi zimekwenda, lakini najua kwa serikali ninaimani inaweza ikakaa ikatatua mara moja suala hilo naipongeza sana katika hicho.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nende katika fungu jengine la Mkurugenzi wa Mashtaka, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Mkurugenzi wa Mashtaka malalamiko ya wananchi wetu ni ucheleweshaji wa majalada kupelekwa mahakamani, imekuwa kadhia ya mda mrefu sana kesi zinachelewa kupelekwa mahakamani. Kwa hivyo, polisi akishakamata akishamaliza kupeleleza ili isithibitishwe kesi inapelekwa kwa *DPP* athibitishe kesi apeleke mahakamani kitendo cha pale mpaka kujiridhisha yeye inachukua siku nyingi sana inacheleweshwa kuna mlongolo wa kesi nyingi sana ambazo mpaka dakika hii hazijenda mahakamani na tunaamini kwamba kila mtu anapotafuta haki yetu itabidi akimbilie mahakamani kwa kutafuta haki yake.

Lakini inapocheleweshwa haki inabidi kuweza kuleta mazingira mengine ambayo inafanya watu kukosa imani na nchi yao hata na serikali yao kwa hiyo ningeomba tu ili kidogo tufanye haraka yanapopelekwa majadala kutoka polisi kwa ajili ya ku-*form frame* kesi pale, basi ifanyike haraka iwezekanavyo kuweza kupelekwa watu wakapata haki zao za msingi sina matatizo nayo sana.

Katika suala zima G6 Mdhibiti na Mkakuguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nimetaka niseme hilo kwa sabaubu ya matatizo ya kila siku ya *CAG*, kwamba ana uhaba wa wafanyakazi, ukaguzi hauendi kwa wakati. Lakini cha kustaajabisha ana watendaji ambao kawasomesha kwa gharama nyingi sana, ni *specialist* hasa wa mambo fulani fulani ya kuweza kutusaidia hata sisi *PAC*.

Leo hii anawahamisha watu wale au wanahamishwa watu wale wanapelekwa Idara ya Wanawake na Watoto sehemu ya *Social Service*, wakati huku wanahitajika zaidi. Kwa mfano, hapa naomba nimtaje mtu mmoja anaitwa Ramadhan Iddi ambaye ni *specialist* ambaye amesoma *electronics IFMS* ni pekee ambaye ana uwezo wa kuingia katika mtandao wa *IFMS* kutusaidia katika masuala ya ukaguzi hata kuwasaidia wenyewe *CAG*, yule mtu anakwenda kumuondoa anampeleka Idara ya Wanawake na Watoto katika kitengo cha *Social Service*, kwa kweli inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuona yeye mwenyewe anasema ukaguzi haukukamilika kwa sababu anakosa wataalamu, lakini leo wataalamu anao anawapeleka Idara ya Wanawake na Watoto, pana kitu gani hapo. Lakini sio hicho tu kuna baadhi ya wafanyakazi watatu sasa hivi wana barua ziko kwenye meza ya *CAG* wanaomba uhamisho waondoke katika Ofisi ya Mdhibiti kwenda kufanyakazi sehemu nyengine. Je, kulikoni? Ni wataalam, maafisa waandamizi ambao tunawajua wana uwezo mzuri na wanatusaidia sana, leo hii wanataka kuhama katika kitengo kile kuna tatizo gani. Mhe. Waziri nakuamini sana katika hicho, nafikiri uliangalie hili kwa kina kabisa, wale watu ambao kwenye kuhitaji tunapoteza pesa nyingi sana kuwasomesha wa kutusaidia katika masuala haya ya kitaalamu basi wabakie katika maeneo yao, ili wapate kumsaidia waziri anapokwenda na wapate kuisaidia serikali yao katika mustakabali mzima wa kufanyakazi zetu hizi za Baraza la Wawakilishi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele vile vile nimejaribu kupitia vitabu nimekuta G2, Mahakama Kuu, ukurasa mapato hayaonekani sijui ilikuaje. Nafikiri kwenye tabu kubwa lile ukiangalia ukurasa wa mapato mle haupo kwenye Mahakama. Sasa ningeomba sijui ilikuaje au kuna tatizo gani hata ikawa hivyo kwenye ukurasa wa G01 16.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kitabu kikubwa hiki nimekuta kwamba kifungu cha G3 Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, muhtasari wake hauna mnyumbuliko wa yale mahesabu ya *CAG* hayamo kwenye kitabu kikubwa, sijui mapungufu hayo ilikuaje au namna gani au tutayapata wapi. Namuomba Mhe. Waziri atuambie ili tujuwe je, yamefanywa hayo kwa bahati mbaya tu pengine watu wamepitikiwa au namna gani tujuwe.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hata katika fungu la G3 la AG muhtasari uliowekwa sio muhtasari wa AG. Katika buku kubwa ukiangalia G3 sio muhtasari wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, imewekwa ofisi nyengine kabisa sio ya Mwanasheria Mkuu. Sasa changamoto kama hizo na vinaletwa vitabu kama hapa tunaposoma, tukiangalia tunaona mbona yanafanyika makosa ambayo hayapaswi kufanywa na maafisa kama hawa ambao wanaleta watu wazima na akili zao, ningetegemea makosa yale pengine yafanywe na watoto wa darasa la tatu, la nne na la tano ingekuwa hatukosowi. Lakini leo watendaji wakuu ambao tunawaamini wanatuletea vitabu hapa Barazani halafu vikawa na makosa kama yale ya kitoto.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na siungi mkono hoja hii mpaka pale Mhe. Waziri wa ofisi hii atakaponipa majibu mazuri juu ya mustakabali wa Msikiti wangu wa Jang'ombe Shurba hapo nitakuwa tayari. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, atafuatiwa na Mhe Suleiman Sarahan Said na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi na wenzangu wote tuliokuwepo hapa kuingia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, na tutakiane kheir Waislamu wote kuendelea na swaumu zetu ili tuwe katika muelekeo mzuri huko tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Majaji wetu, Mahakimu wetu, Wakuu wa Idara na vitengo mbali mbali pamoja na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya juu ya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika utawala bora kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa dhati kabisa utawala bora ni mwelekeo mzuri katika jamii, na bila ya kuwa na utawala bora basi hatufiki tunakokwenda. Kwa hivyo, suluhisho na maelekezo mema ndio utawala bora, ndio maana katika wizara hii kuna mambo mengi, kuna viongozi wa

dini, kuna viongozi wa Mahakama, kuna viongozi wa mambo ya rushwa na wengineo wengi ili kuhakikisha kwamba tunaelekea katika mwelekeo anaoutaka Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitamke rasmi kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asili mia mia moja sina tatizo. Kwa hivyo, taasisi yoyote nitakayokuwa sikuichangia hapa, nitakuwa nimeshaiunga mkono wasiwe na wasi wasi, lakini nitatoa ushauri kwa baadhi ya maeneo kama ulivyo wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti. kubwa ninaloliomba kulisema tu kwamba Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, suala hili ni kubwa, ni muhimu na ndio maana ukifika wakati fulani, ukifika mwaka unaotakiwa uende ukajisajili ni lazima uende uthibitishe vielelezo vyako kwamba umo katika maadili yanayotakiwa. Kwa sababu bila ya kuwa na taarifa rasmi basi kunaweza kutokea matatizo baadae ukajiingiza. Kwa hivyo, nawapongeza wenzetu hawa Viongozi wa Tume ya Maadili na watendaji wote, kwa kazi nzuri wanazofanya za kuwahakiki wale viongozi katika muelekeo bora wa shughuli zao na ukweli wao. Kwa sababu ukisema kweli utakuwa umefanikisha, ukisema vyenginevyo itakuwa umeingia kasoro maadili yako yamepungua. Kwa hivyo, niwapongeze wenzetu hawa kwa kazi nzuri wanayoendelea nayo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, Mahakama zetu, Mahakama ni sehemu moja wapo ya kupata haki kwa mwenye kufuatilia shughuli zake kimahakama. Lakini niipongeze sana wizara kutokana na Mahakama zetu hizi zinajitahidi kufanya kazi zao kadiri ya uwezo wao. Ombi langu naziomba Mahakama zetu ziongeze bidii katika kutafuta haki kwa watu wetu, lakini tuwe waadilifu zaidi, sio tuwe waadilifu tuongeze uwadilifu kwa sababu ndio uongozi bora na utawala bora, ili kupata haki kwa wakati na wananchi wetu waondokane na msongamano wakati mwengine wa maneno ya ovyo. Watu wengi wanalalamika wanacheleweshewa kesi zao, lakini kesi zina matatizo yake kwa sababu kesi bila ya shahidi huwa ni matatizo. Kwa hivyo, hili naunganisha tu kwamba ni vyema Mahakama zetu wale mashahidi wetu wafanyekazi vizuri ili tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti, lakini zaidi niseme kwamba kesi za udhalilishaji ambazo kuna Mahakama zetu hapa ambazo zinafanyakazi vizuri na zinaendelea vizuri. Pia nimpongeze Mwenyekiti wa Mahakama hizi anabidii na anajitahidi sana kutokana na shughuli zake mbali mbali, tunampongeza kwa dhati na kwa moyo wetu wote, hasa katika mazingira mbali mbali tunayokutana katika mambo haya ya udhalilishaji katika sehemu mbali mbali.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi pamoja na Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii tumeshirikiana naye katika sehemu mbali mbali. Tunampongeza kwa uwezo wake wote aliojaliwa na Mwenyezi Mungu na amzidishie kuelekeza mema juu ya kuondoa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, tunazo Mahakama nne. Tunayo Mahakama ya Vuga ya Watoto, Mahakama ya Mahonda, Mahakama ya Chake Chake na Mahakama ya Wete. Kwa hivyo, tunaomba waongezewe wafanyakazi, yaani Mahakimu au Majaji, lakini tunasema waongezewe watu hao kwa ajili ya kuendelezwa haraka kesi ili haki ipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, pia sio vibaya kutoa ushauri. Ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mahakama zetu ili zende vizuri basi tuwe na watu wakalimani wa lugha mbali mbali. Kwa mfano, anakwenda kwenye Mahakama mlemavu wa aina mbali mbali, kama wa kusikia au hawezi

kusema, lakini pakiwa na mkalimani basi atawasaidia watu wale ili kupata haki zao. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa makusudi iwatafute wakalimani ambao watasaidia katika Mahakama mbali mbali wananchi wetu ambao wanasumbuliwa kwa hali moja au nyengine kutokana na mazingira yao ya maumbile walivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu. Hilo, Mhe. Mwenyekiti, litaleta faraja. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, tukiri kwamba Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ana kazi nyingi na ana kazi nzito. Kwa hivyo, niombe shughuli zake hizi apatiwe watu wa kutosha, wenye fani na kwa sehemu mbali mbali ili kazi ziende vizuri. Tunaamini Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu zetu za kazi kuna mawizara, mashirika ya umma na mengineyo basi bila ya kuwa na wanasheria basi hatufiki wakati umebadilika sasa hivi. Wanasheria ni sehemu moja ya kuelekekeza mambo ambayo yanatakiwa katika sehemu hiyo.

Kwa hivyo, wanasheria ni muhimu na ningeomba wizara kwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria tukaongeza kwa bidii wanasheria katika sehemu mbali mbali za wizara, maidara na taasisi nyengine. Mhe. Mwenyekiti, leo tunaamini kwamba tuna migogoro mingi ya ardhi, kuna migogoro hata katika maskuli, makambi yetu, vituo vya afya na kwengineko, wanasheria wanahitajika kusaidia katika maeneo yale ili haki zao wapate watu wale kuendelea na kazi zao.

Vile vile, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, nampongeza kwa dhati kutokana na kazi zake nyingi anazofanya hasa tukizingatia kwamba sisi hatuwezi kufanya ziara katika kamati yetu bila ya kushirikiana na yeye kwenda kusikiliza lolote juu ya matatizo ambayo yanatokana na hali iliyotokea katika nchi yetu ya udhalilishaji, nampongeza. Lakini narudia lile lile Mkurugenzi wa Mashtaka ni sehemu moja, lakini wale walengwa wenye matatizo yao ni sehemu ya pili.

Kwa hivyo, akishapelekewa mashtaka moja, mbili, tatu basi yeye apate watu wa kutoa ushahidi inapopelekwa Mahakamani, ndio maana anakaa na kesi mpaka anakata tamaa na kwa mujibu wa taratibu zetu kila kitu kina muda wake, ikifika muda ah! Suala au udhalilishaji huu mimi naona hauna mashiko mfano, au hauna ushahidi anaachia atalaumiwa Mkurugenzi wa Mashtaka kumbe sio yeye. Hivyo, ni vyema kwamba tusomeshwe wananchi wote pamoja na mimi, taaluma ni muhimu, narudia kila wakati lugha hii, bila ya taaluma kumfikia mtu wa chini kabisa mtu wa kijijini basi shida hii bado itaendelea na maskini atapata lawama mkurugenzi bila ya kutegemea. Kwa hiyo, nampongeza Mkurugenzi wa Mashtaka na ofisi zake zote Unguja na Pemba, wanafanyakazi nzuri na anajitahidi kwa moyo wake wote na bahati nzuri yeye ni mwalimu, kwa hivyo anajua shida ya kazi hizi zinavyokwenda. Kwa hivyo, namtakia heri na aongeze bidii katika shughuli zake za kila siku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Naipongeza idara yetu hii kwa kazi zake nzuri na wanafanyakazi kwa bidii, lakini nakuja kidogo Mhe. Mwenyekiti, serikali ina kitengo hiki kinachofanyakazi kwa nchi nzima na inafanyakazi kwa mtu yeyote wa chama chochote, lakini wakati wa siasa huwa kuna mashaka kidogo nazungumza leo. Siipendi rushwa na ninailaani kwa nguvu zangu zote, lakini viongozi wanaoandamwa katika nchi hii, kuanzia Rais, Mbunge, Mwakilishi, Diwani wa Chama cha Mapinduzi ndio ataandamwa, hawa vyama vyengine hawafuatiliwi kwa nini?

Kwa hivyo, naiomba idara hii muhimui na nimesema inafanyakazi zake kililahitaala na wanafanyakazi zao nzuri, lakini ukifika wakati waangalie kuanzia chama chochote, ikiwa chama hicho kakianzisha Shihata au nani nacho kiangaliwe, ikiwa chama hicho kakianzisha Machano Othman kiangaliwe, sio CCM wanaandamwa kupita kiwango, kumbe majasusi wale wabaya wa rushwa wamo katika vyama vyengine wameka kimyaa na wao wanacheka wanasema ah! Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuelekee huko wakati ukifika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme tu kwa ufupi kwamba kwa muelekeo wangu natoa ushauri ufuatao. Mhe. Mwenyekiti, tukiri kwamba wizara hii ni kubwa na ina mambo mengi, wizara hii ina majukumu mazito kwa kila sehemu. Kwa hivyo, niiombe serikali na niwaombe wajumbe wenzangu tuichangie wizara hii, tumpe imani waziri na watendaji wake wote, lakini pia tumpe ushauri inapostahiki.

Kwa kweli, napenda tu kama limetokea tatizo wakati wowote basi nitamfuata waziri yeyote wizara sio nyumbani, nitamfuata kuna moja, mbili, tatu ili tumpe muongozo, kwa sababu mtu mmoja hawezi kufanya kitu bila ya kupata ushauri na sisi bahati nzuri hapa sote ni washauri wa wizara zote. Kwa hivyo, kila mtu ana haki tumpelekee matatizo, maelekezo. Mimi nasema tu kwamba kama lipo langu ambalo limenikaa basi nitamfuata waziri wakati wowote au Naibu Waziri au Katibu Mkuu na huo ndio utaratibu mzuri, hata Mwanasheria au kuna Hakimu fulani, lakini hatuingilii mambo ya Mahakama, kama kuna ushauri tu, ushauri lazima tutoe tusikilize kuna nini, lakini hatuingilii maamuzi ya Mahakama wala shughuli zao za kawaida.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba baada ya hayo mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele, naipongeza wizara hii pamoja na watendaji wao wote, hasa tukizingatia kwamba ndiko haki zetu tunakozipata pindi tukikutwa na shida. Kwa hivyo, niombe tu kwa nia njema kabisa naikubali kwa asilimia mia moja sina tatizo. Ahsante, Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nakushukuru Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said, atafuatiwa na na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Simai Mohamed Said ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumshukuru Mhe. Waziri kwa kitabu chake ambacho amefafanua mambo mengi sana na leo sitokuwa nje sana ya kitabu chake zaidi ya kuwa nimesikiliza sana maoni yake.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na suala la ukurasa wa 16 ambapo kuna urithi. Katika kifungu cha 44 kwenye masuala ya kuimarisha kazi na kusimamia mali za wakfu, amana, mirathi kwa Waislamu, sala, mabaraza na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, urathi unafanyika na upo wa mambo mengi. Ukienda kwenye serikali upo kwa kutumia vigezo ambavyo vitafanyika kama ni kwa Waislamu au kwa mambo mengine ukuhitaji msaada wa kisheria kutoka serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala la mirathi limekuwa na mashaka makubwa sana katika nchi yetu. Kwanza imeonekana ukidai mirathi kama vile wewe ulikuwa unamsubiri baba

yako afe au mama yako afe. Hili ni jambo ambalo Mtume wetu Muhammad (*SAW*) ametusema kwamba baada ya maiti kufa basi watu wasikae muda mrefu waweze kugawana hizi mali zao ili kuepuka mengi ambayo Mtume aliyasemea hapo.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo tulilonalo sisi ni kwamba urathi hasa kwa watu ambao wamedhibitiwa sana na upande wa baba kama mababa wadogo, urathi ule mara nyingi unatumiwa na wazazi wale na watoto wanakosa haki zao. Kwa kweli, suala hili Mhe. Mwenyekiti, tukisema tuliachie liendelee kama lilivyo lina ushahidi wa kutosha kuna ule upande wa kutoa vibali katika kudhibiti ardhi katika suala ambalo wamesema limewashinda sana ni urathi.

Mhe. Mwenyekiti, urathi unakuwa na matatizo sana katika jamii yetu huwezi kusimama ukadai mirathi yako, mambo mawili utapata ama utakwenda maji wewe uache watu au *otherwise* wewe utakuwa si mtu kudai haki zako. Naiomba serikali kwa wale watu wote ambao wameshakufa na katika hasa kupitia mlango wa Ofisi ya Mufti basi zitoke elimu zaidi za kuweza kutoa hii mirathi, kwa sababu wao huwa hawajijui katika umri huu kwamba wanakula mali za yatima na mambo mengine. Lakini wao wanachoona ni kwamba wamedhibiti hicho kitu sasa ningeomba sana hili suala likaweza kusaidia katiaka masuala haya. Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa niseme hili ili Mhe. Waziri nalo alitilie maanani ili kuweza kuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee katika ukurasa wa 12. Kuna suala la udhalilishaji katika kifungu cha 33. Mhe. Mwenyekiti, bado nalizungumzi suala la Ofisi ya Mufti kwamba ni bora ajitahidi sana kufanya ziara katika maeneo mengi ambayo yanahusu hasa vyuo vya *Qur-ani*. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kitabu ni aibu kuona katika ukurasa huu, unasema vitendo vya udhalilishaji katika Madrasa za *Qur-ani* vimekuwa vikiripotiwa mara mara.

Mhe. Mwenyekiti, katika jumla ya udhalilishaji basi kama na Vyuo vya *Qur-ani* ambavyo vinaongoza maadili mema kwamba vimo hasa hawa walimu wetu. Kwa hivyo, hili suala Mhe. Waziri alichukue aliangalie kwamba huku tunakokwenda kuwapeleka watoto wetu kumbe ndio tunawapeleka kwenye moto zaidi kuukanyaga, sasa sijui tuelekee wapi? Sasa Mhe. Waziri ningeomba suala hili aikabidhi Ofisi ya Mufti, ili liweze kuendana na shuguli hii. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti sitaki niliseme sana lakini kwa suala hilo nitaangalia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee katika ukurasa wa 10 na 11. Mhe. Mwenyekiti, amezungumzwa Mufti sana katika ukurasa mzima ukiwa na kifungu cha 28,29 na 30. Anazungumzwa Mufti kazi zake na mambo mengi aliyonayo. Mhe. Mwenyekiti, Mufti ni mtu mkubwa sana ana sekta za dini nyingi sana, huyu Mufti kadiri tutakavyokuwa tunamzungumza ana Kitengo Maalum, naweza kusema kwamba asilimia ya Waislamu wote kwa upande wa Zanzibar anawashughulika yeye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika utafiti wangu nilioufanya bado haja ya kukidhi haja katika matumizi yake bado anapangiwa, ningemuomba akafanya jihada zake akampa *Vote* yake yote ya matumizi yake akajipangia mwenyewe na sisi tukapata kumlaumu Mufti kwamba bado kazi hii inatakiwa, lakini kama tutakuwa bado tunamnyima haki zake, basi lawama atakuwa anatutupia upande mwengine kwa sababu hajipangii nini ambacho anakifanya, na Mufti katika pande Unguja na Pemba wote wapo katika vitengo vyake. Lakini ukisema Mufti ni sekta nzima ya kimufti. Kwa hivyo, nazungumzia kwamba wapewe *Vote* yao waweze kuji-*control* na kuweza

jipangia mambo yao ili lile jambo, kwasababu wale ni watu dini wanajua wafanye nini ukarabati wao. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa niseme hilo na Mhe. Waziri nalo alichukue ili tuweze kuangalia hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kwenye Sheria za Mahkama. Mhe. Mwenyekiti, Mahkama zetu na sisi wenyewe na dini zimechanganyika, sote ni Waislamu wengi sana, Mahkama zinasheria nzuri lakinki kuna na Wizara za Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, tunawapa tatu sana watu katika sheria zetu za kuhukumu sana mambo ya ndoa, mambo ya sheria za watoto, mambo huyu atakwambia hili, huyu atakwambie lile.

Namuomba Mhe. Waziri hizi Sheria za Mapenzi, Sheria za Watoto, Sheria za Wanawake na mambo mengine wakayaweka wazi sana kuelekea upande mmoja, ama waendelee kukaa na dini, ama kwenye serikali, lakini *otherwise* tunapelekea kwenye dini, tunapeleka kwenye serikali, huyu akishindwa kwenye dini anakuja kwenye serikali, akishindwa serikali anakwenda kwenye dini, sasa mimi ningesema mfumo mmoja. Kwa kuangalia kesi zetu za mapenzi basi uangalie mfumo huo huo kama ni wa dini tuende huko huko serikali ijuvue kwenye masuala haya ili suala lipate ufumbuzi. Mhe. Mwenyekiti, na hilo nimwambie Mhe. Waziri ili aweze kuliangalia kwa mfumo wake.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena katika masuala ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, Mahkama ya Ardhi ni Mahakama kama Mahkama nyengine lakini Mahakimu wa Mahkama ya Ardhi ni Mahakimu wale wale wanaotoka katika Mahkama hizi kubwa. Mhe. Mwenyekiti, Mahakimu hawa kweli wanafika wakati wanakosa haki zao. Kwa kweli, inafika wakati wanashindwa kuboreshwa kiutaalamu, semina na kila kitu, wanaokana kama tayari wamekwenda Wizara ya Ardhi ambako siku kwenye Mahakama. Sasa naomba sana hawa ni Mahakimu au ni kama Majaji kama Majaji wengine ambao wote tunawategeme mpaka mazingira yao ya kuhukumu kesi. Mhe. Mwenyekiti usishangae akahukumu kesi chini ya muembe.

Mhe. Mwenyekiti, hawa naona niwatete, vitengo vyote ambavyo, na vitu vyote ambavyo vinastahihiki kupewa Majaji wa Mahkama ya kesi hi huku za jinai basi na hawa washughulikiwe katika maelekezo hayo hayo wawe katika orodha, kama watu wanapelekwa semina, watu wanapelekwa mafunzo watu wanapelekwa katika mambo chungumzima, basi na hawa nao wapewe.

Mhe. Mwenyekiti, nisimame hapa hapa katika kuzisifu mahkama zetu, nimshukuru sana Mhe. Waziri kweli ana wigo mkubwa katika mahkama zetu, mahakama zimeleta upeo mkubwa na majaji wetu wamepanua wigo sana wa kuhukumu kesi, na sasa hivi taratibu nyingi zimeondokana na kesi za kukata rufaa za kipumbavu, kwa sababu mahakimu wamejiweka wazi kwamba hawana shida ya rushwa, hawana shida ya matatizo, ubakishwe ubinaadamu kama ubinaadamu na mambo mengine yanapitikia lakini wanajitahidi kuendelea na uadilifu. Nawasifu sana Waheshimiwa majaji kwa kweli nao wanajitahidi katika sekta zao.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala jengine la mambo ya ajira. Mhe. Mwenyekiti, ajira tunazifahamu sana, lakini ninachokizumza kwamba nashangaa huku nje mitaani utakuta watu wanavyo vyeti vyengine vichafu kwa jinsi vile vyeti walivyonavyo. Ukija kwenye mashirika

unasikia au katika mawizara unasikia kuna nafasi hazina watu. Sasa humu katika kitabu kila kitu nimeona kwenye *target.*

Lakini Mhe. waziri sijamuona *target* au sijaangalia vizuri, mbona hajaniandikia kunionesha ana-*target* ya kuajiri watu wangapi mpaka mwaka 2018/2019? Tukajua watu wangapi ana- *target* ya kuajiri, kwa sababu bado utakuta katika mashirika na mawizara kuna nafasi. Kwa hivyo, ningeomba atupe maelekezo kwamba alikuwa ana-*target* ya kuajiri watu wangapi na mpaka mwaka 2020 atawaajiri watu wangapi, ili tuweze kujua kipimo cha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie katika jambo hili nitamuomba sana Mhe. Waziri kesi za misikiti, kesi za vyuo vya uongozaji limekuwa tatizo kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, waziri ukitaka usitake hili suala uliangilie, misikitini huko kuna mambo, watu wanapigana, watachinjana. Kwa kweli, sijui ni kitu gani, nafikiri wewe kwa sababu ni mtaalamu unajua, lakini kesi za misikiti zimekuwa nyingi, ambapo zamani kulikuwa na heshima ya Sheikh, siku hizi wanatukanana, wakipiganana. Sasa uziingize kwenye bajeti yako misikiti na vyuo uweze kuvitambua vizuri na uweze kuwa unaweza kuwa-*control* vinginevyo itakuwa sekta moja tumeiwacha nje.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niangalie katika ukurasa wa 47. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa huu unazungumzia suala la Mkurugenzi wa Mashtaka. Lengo na madhumuni makubwa ambayo Mhe. Rais wetu Abeid Amani Karume wa kwanza wa Zanzibar, nia yake ya kuwafunga watu jela ilikuwa sio, isipokuwa nia yake ilikuwa ni Chuo cha Mafunzo cha kwenda watu kule kujifunza, kwa sababu ya matatizo waliyonayo huku wasiibe tena wanaporudi na kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, tumeondoa ile dhana ya Chuo cha Mafunzo tumeipeleka jela, ukifika kule utakiona cha mtema kuni, sio kwamba unakwenda kufundishwa. Kwa hivyo, ningeomba katika sekta hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka, wana nafasi kubwa ya kwenda kwenye semina za watoto wetu wanaotoka chini kuanzia vyuo, mashule na vitu vyengine ambavyo watoto wasiyakaribie haya makosa na waweze kuwapa utaalamu zaidi, kuliko kuzisubiri kesi wakazipeleka pale kwa kwenda kuhukumiwa.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri hii Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iendeleze semina zao katika vyuo kwenye mafunzo mbali mbali, ili kujenga uwiano mzuri wa kuwapata hawa vijana wazuri wanaokuja, badala ya kuwasubiri waje wafanye makosa halafu tuje tuwahukumu. Ningeomba sana na hili likawa katika sekta hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki kwenye ukurasa wa 48, katika Udhibiti wa Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, bado tuna tatizo la kutokufika kwa wakati katika masuala yetu. Sisi tunapohitaji tunahitaji kujadili kitu cha mwaka 2016/2017 na 2017/2018 ambavyo *front* yetu hapa mbele. Lakini ukijadili kitu cha 2015/2016 au 2014/2015 inakuwa kidogo kile kitu kimeshapitwa na wakati na matokeo yake hata tukikifanyia kazi kinakuwa hakina maana tena. Pengine mkurugenzi keshakufa na watu waliofanya hawapo tena, sasa unakwenda kuwahukumu nini zaidi ya kuwaonea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninachokizungumza kukosekana kwa ripoti na ukaguzi katika majengo mengi na matatizo yaliyotoka. Nitatoa mfano, tuna jengo lile pale Tibirinzi la Wizara ya Fedha na Mipango, ninakuja kuambiwa ngoja uletewe ripoti na mpaka leo ripoti haipo, mkaguzi na

mkagua serikali. Kwa hivyo, waliopo hawapo tena, ukienda kumuhukumu unamuonea, hata mambo ya Mwenyezi Mungu Mhe. Mwenyekiti, anakuambia mtu akifanya kazi mlipe kabla jasho halijakauka. Lakini hata kama mtoto kakosa ukiletewa jioni, kama umetoka Mhe. Mwenyekiti, kwenda nyumbani ukaletewa kesi ya mtoto usimpige tena, mwambie yule dada anayemlea kwamba akifanya kosa basi mpige hapo hapo, sio umsubiri mpaka akisha sahau unakuwa unamuonea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nilikuwa nazungumzia kwamba madeni haya na matatizo yanayotoka yaletwe kwa wakati na kusimamia, kwa sababu taasisi husika iwepo katika muda ule. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hapa hatujaona matokeo yoyote ambayo mambo mengi ambayo juzi tu hapa kulikuwa na Skuli ya Madungu pale imepukutika yote, mikataba mibovu. Lakini hao hao ukiwaambia wanakuambia kanuni, sheria imetubana na kitu gani kimetubana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ana wanasheria wengi, ana Mwanasheria Mkuu mtoto mbichi kabisa, *young* kabisa ana uwezo mkubwa sana na ana timu kubwa sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na wasomi wa hali ya juu. Kwa hivyo, ajaribu kuipitia mikataba, ajaribu kuangalia ili atuokoe katika serikali yetu, tumemuamini na tunamuamini sana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nashauri sana Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ambayo Mhe. Mwanasheria Mkuu amsaidie Mhe. Waziri ni kuiangalia mikataba katika hali ambayo vyovyote vile itakuwa lazima ni kuiokoa au ni kuziokoa fedha za serikali ili zisipotee kirahisi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumzia masuala ambayo yanaleta ....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakukumbusha una dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, sawa. Bado naizungumzia sheria nakuja, lakini nimeshaliomba sana, lakini bado Mhe. Waziri kama sheria sijui kama ataipataje. Nalizungumzia sana suala la magereza, kufungwa sio kumaliza maisha, unaweza kufungwa ukiwa na kosa na unaweza ukafungwa usiwe na kosa, pia kuwa mahakamani sio kuwa unajua sheria na matatizo mengine yanatokezea kwa bahati mbaya.

Kwa hivyo, namuomba sana sheria za jela kwa kesi maalum zitapungua. Mhe. Mwenyekiti, nazungumza tena unafungwa ukijua nimeonewa, ukijua sikufanya kosa lakini ndio umefungwa, unafungwa kwa kujua nimefanyakosa. Lakini wewe unaondoka jela. Mtu kumfunga ndani peke yake inatosha kuwa ni jela, wale wafungwa kule ukiwaachia kwamba wao wapewe na matrekta kulima kwa mikono basi. Mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, ukimtoa mtu jela basi hata mama watoto hamtaki tena yule mume keshavunjwa kila kitu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninachokuambia kwamba zitolewe siku maalum, naomba tena kwa Chuo cha Mafunzo, sisemi magereza ya Zanzibar mama watoto akacheze na baba kule jela, ili mradi warudishe hadhi ya watoto na kuzungumza mambo yao. Mhe. Mwenyekiti, kumfunga mtu miaka 10 uende ukamuone tu, hivi sivyo. Siku moja apewe chumba ajitanafasi, tutaondoa mambo ya UKIMWI na tutaondoa matatizo yote. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman Sarahan Said. Nilimuita Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf lakini simuoni. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohamed Said, atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, lakini niendeleze kukuomba radhi wewe pamoja na Wajumbe wako wa Baraza hili la Wawakilishi tukufu, kuwa bado kifua changu hakiko sawa, kwa hivyo nikikohoa bado sina nia mbaya yoyote kwa sababu ni kifua changu kinauma na pia nina mafua. Kwa hivyo, niwaombe na wasikilizaji pia nitajitahidi niweze kuchangia ipasavyo na wapate kusikia yale ambayo nakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ambapo mimi nikiwa mtetezi wao na msemaji wao hapa. Pia niendeleze kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti waliosoma hotuba zao leo asubuhi, walitoa mawazo na mambo ya bajeti mengi ambayo naamini tumeweza kuyapata na kuweza kuyachangia.

Mhe. Mwenyekiti, pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu, kwa jinsi walivyokuwa na mahusiano mazuri kwa kupitia mimi mwakilishi wao na wizara hii. Shukrani hasa ziende kwa Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wake wote pamoja na Mwanasheria Mkuu, na viongozi wengine wote katika wizara hii, ambapo mimi mwenyewe nimekuwa na mahusiano mazuri na tunaweze kuwasiliano pale ambapo wanahitaji msaada kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu, kwa hivyo nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitarudi kidogo katika hoja zangu za miaka miwili ambazo nilichangia nyuma huko. Kwanza ni suala la *E-Government*, moja Mhe. Waziri atakapokuja atueleze mpango mkubwa wote wa *E-Government* serikali tumefikia wapi, kwa sababu suala moja ambalo linanisumbua sana, sijui makubaliano yakoje lakini ukiangalia kwa utaratibu ndani ya wizara zetu, hata ukiangalia tovuti pamoja na *Email* za Waheshimiwa Wajumbe, bado wapo viongozi au Wakurugenzi na Makatibu Wakuu na wengine watendaji wanatumia *Emails* kama za *Hotmail*, *Yahoo* na *Gmail*. Sasa hebu Mhe. Waziri utakapokuja utueleze mpango mkuu wa suala la *E-Government* kuhusu mpango wowote mnaokwenda nao pamoja na huu mkonga wenyewe tuliokuwa tunauzungumza miaka ya nyuma, tunaelekea wapi sasa hivi tupo pazuri baada ya yote yaliyotukuta huko nyuma kuingia mkataba na *Zantel*. Matumizi yake hasa *E-Government* tunaelekea wapi, maana yake hiyo *E-Government* ni kutumia *electronic* na mambo yote.

Mhe. Mwenyekiti, pili ni suala la Ofisi ya *CAG*. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nipongeze kwamba tumeanza kuona mabadiliko katika Ofisi ya *CAG*. Nimshukuru sana na nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar hivi karibuni kwa kumchagua Mwenyekiti. Lakini, bado nilikuwa napata hofu kwa sababu niliongelea kwa sauti mwaka mmoja nyuma, kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018 juu ya mapungufu yaliyokuwepo katika Ofisi ya *CAG* katika suala zima la kufanya *auditing* katika taasisi na mashirika ya serikali. Sasa moja ambalo lililokuwa linampata yeye ni kutokuwa na watendaji wa kutosha, na alikuwa anachukua wafanyakazi au anaingia ubia na kampuni za nje.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kumlaumu *CAG* na siwezi kunyooshea mkono moja kwa moja wizarani, kwa sababu mamlaka haya ya kuteuwa mwenyekiti ili *CAG* apate watendaji ipasavyo yako chini ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Sasa niombe tu kwamba tayari Mwenyekiti wa Bodi ameshapatikana na bodi ipo. Sasa wachagamke haraka sana yapelekwe majina katika wizara husika, ili *CAG* aweze kwenda na *race* ambayo tunaitaka.

Hivi leo Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwa utaratibu tunaongelea sisi tuko mwaka 2018/2019 tunapitisha bajeti hapa leo. *CAG* ndio kwanza amekamilisha ukaguzi wa mwaka 2015/2016, sasa hiyo ripoti itakapokuja huku mpaka tuje kuichangia sisi tunaweza kuondoka. Kwa hivyo, tujitahidini sana kwamba *CAG* apate nguvu zote zile anazizihitaji, ili twende sambamba na wenzetu kule Tanzania Bara wanavyofanyakazi na nchi zetu za jirani.

Natambua kwamba *resource* tulizokuwa nazo katika serikali yetu ni chache lakini kwa mujibu wa katiba *CAG* ni taasisi muhimu na yeye apate awe *equipt*, ili wananchi wafaidike na taarifa ambazo wanazostahiki kuzijua ili na sisi tunapochangia jambo, unachangia jambo siyo wakati mwingine mtu ambayo tayari kama ametenda kosa au amefanya sahihi kama tunampongeza au tunamkamata kwa makosa aliyoyafanya basi iwe ipo katika kipindi ambacho kinastahiki.

Lakini leo *CAG* yupo 2015/2016 sisi tupo 2018 kwenda 2019 sasa hivi, kwa hivyo ilikuwa inahitajika hapa hivi sasa awe tayari yeye yupo katika 2016/2017 anaingia tena 2017 kwenda 2018 huku tukiondoka sisi tunakuwa tupo sambamba.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nataka nitoe ushauri ambao niliuzungumza katika miaka ya nyuma naamini Mwanasheria Mkuu ananisikia.Ukienda katika bajeti kuu ya serikali katika vipaumbele tunaangalia suala la utalii, lakini tunapoongelea kama kipaumbele ni utalii ina maana kila *ministry* iko-*concern* itakuwa imejipanga kuhakikisha kwamba suala la utalii wao wanali-*capture* katika huko kipaumbele cha serikali kwa namna gani.

Ushauri wangu katika wizara hii ni *issue* ya usalama wa wageni wetu wanaokuja, mbali na wanaokuja kwa ajili ya kutalii au kutembea lakini wale pia wanaokuja kama kwa biashara. Jana serikali walikuwa na wageni wanafungua ofisi nilimuona Mhe. Waziri wa Nchi alikuwa Mgeni Rasmi wanayo kampuni kutoka China wamefungua ofisi yao na hawa ndio watakaojenga bara bara ya kutoka Bububu kuelekea Mahonda mpaka Mkokotoni. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye utalii ukiangalia kuna wageni wanaokuja kwa ajili ya biashara lakini pia kwa ajili ya kutembea hii ndiyo *concept* kwa ajili ya makubaliano yanavyohusiana na Umoja wa Mataifa. Sasa tunapoangalia usalama wa wageni tunaangalia usalama wa watalii pamoja na sasa wanaokuja kwa ajili ya biashara, ina maana wanaweza kuwa ni wafanya biashara au wawekezaji lakini pia wanaweza kuwa wawekezaji chini ya *World Bank* au taasisi kubwa ambazo wanafanya mikataba na serikali.

Kwa hivyo, hao wanapoingia mikataba na serikali usalama wao, wakati mwingine unapopata matatizo kuna umuhimu sasa na sisi pia tukawa na mahakama zetu za wageni kama za kitalii, tayari kule Arusha nimeona zimezinduliwa karibuni na Mhe. Rais John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amezindua. Sasa tunapokuwa *Tourism Court* maana yake nini? Ina maana hata kama mgeni kafanyiwa uhalifu wa aina yoyote leo, anapoondoka ule ushahidi tunakuwa tayari tuna tunampeleka mtu Mahakamani anapohukumiwa tayari inakuwa kila kitu Jaji amejiridhisha.

Mhe. Mwenyekititi, kwa mfano hili gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 16/05/2018 na Mhe.Waziri ningeomba ulitafute hili lilikuwa la Jumatano nafikiri ilikuwa ni jana, ukiangalia mbele hili Gazeti la Serikali linasema "Polisi Walaumiwa Kuvuruga Kesi za Udhalilishaji" ukurasa wa mbele Mhe. Mwenyekiti, halafu kwenye ukurasa wa pili linasema "Mahakama Yamchomoa Aliedakwa na kete 668". Sasa ukienda humu ndani anasema kuhusu hii habari ya kete 668. "Lakini siku ya tukio mtuhumiwa alikuwa dukani kwake Mtemani baada ya askari Polisi kudai wamepata taarifa za uwepo wa unga nyumbani kwake walifika dukani hapo na kumchukua bila kufata utaratibu, na baada ya kufanya upekuzi Hati ya Upekuzi haikujazwa kitu kilichopatikiana".

Sasa, hapa najenge hoja mbili kwa wakati mmoja, moja ni Ofisa ya ambayo tayari Mhe. Abdalla Maulid Diwani amezungumza kuhusu kesi kutopelekwa mahakamani juu ya ofisi ya *DPP*, lakini pia utaratibu ambao ulotumika na majeshi au wapiganaji wetu Polisi ili katika ukamataji mzima katika *process* yote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunaponyoosheana mikono baina ya jeshi letu la Polisi pamoja na Ofisi ya *DPP* na wakati tupata taarifa kama hizi kama hapa Mahakama haijakosea utaratibu haujafuatwa lakini *DPP* unapotaka kumnyooshea mkono ofisi yao wamechukua ile kesi wameipeleka Mahakamani wakijua pengine kama watashindwa. Kwa hivyo, lazima tujenge mahusiano mazuri baina ya *DPP* lakini pia na Jeshi la Polisi, tumepitisha hapa sheria juu ya *Cyber Crime* tayari imeshapitishwa kuna mambo mengi yeshapitishwa.

Lakini, ukienda huko polisi wenyewe uwezo wao wa kukaa kukamata na kufanya na kufanya, je kama wanazo fedha na nyenzo za kutosha? Maana yake tunaangalia mamlaka mbili tofauti hapa pana Serikali ya Jamhuri ndiyo inayosimamia ulinzi na usalama wa wananchi. Kwa hivyo, Jeshi la Polisi ni Muungano lakini Mahakama zetu wanategemea Polisi hao hao, sasa lazima tuangalie katika jinsi ambayo tunawawezesha vipi ili Polisi wawe na uwezo katika *process* nzima ya kwenda kukamata na kufanya utaratibu wote kwa pamoja.

Kwa mfano, leo ukiangalia katika hii habari ya mtu mwenye kete 668 anasema hapa " ... mara baada ya uamuzi huo upande wa mashtaka ukiongozwa na Mwanasheria wa Serikali bwana Ramadhan Suleiman kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka umedai kutoridhishwa na

maamuzi ya Mahakama na utakata rufaa, ambapo itatoka indhari ya mdomo na mtuhumiwa ametakiwa ajidhamini kwa shilingi 1,000,000" hili nanukuu Gazeti la Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa lazima tujitahidini sana kwa upande wa serikali kujenga ukaribu baina ya wizara, *DPP* na Jeshi la Polisi. Lakini katika mpango wote huo ambao tunazungumza katika ofisi pia nikirudi katika ofisi ya *CAG* naomba sana warudishiwe basi hao watu, ili waweze kufanya kazi zao kwa umakini.

Lakini kwenye nimalizie tu kwenye lile suala la *Tourism Court,* hili Mhe. Mwenyekiti tayari nchi nyingi za Afrika wameanza kwenda nalo na litatusaidia sisi katika kuujenga uchumi wetu na pia katika kujitangaza na kwa hali tunayokwenda utalii utakuja kusimama kwa upande mkubwa sana katika uchumi wa nchi hii.

Sasa usalama wa wageni, usalama wa wawekezaji, usalama wa mali zao pia. Kwa hivyo, hakuna njia yoyote nyingine isipokua ku-*speed up the process* na kama utaangalia kwenye *statistic* za uhalifu wa miaka mitano mpaka kumi juu ya wawekezaji pamoja na wageni, basi kama utatafuta mtu ambae amefungwa ni wachache sana, leo wapo pale mjini wanatembea pia wanafanya uhalifu anapita mtu ana chupa anatia ndani kama ya dawa anamgonga mgeni anamwambia "sikiliza umenivunjia dawa yangu nataka unigaiye dola tano au kumi" anayefanya namjua ameshakamatwa mara nyingi anajulikana na hasa mjini ukitembea mpaka Jeshi la Polisi wanamjua, lakini anawekwa ndani wiki moja wiki ya pili anatoka.

Kwa kweli, hakuna utaratibu mzima wa kukamata na kuweza kuwadhibiti, kwa hivyo, mtu mmoja anatia jina baya serikali na wananchi na anafika pahala anatoa lugha chafu kabisa, kwa sababu hakuna njia za kumkamata na kumdhibiti anafika pahala anawaambia kwa niaba ya Wazanzibari *go back home* maana yake nenda nchi yako ulipotoka, *this is not your country* hii siyo nchi yako. Sasa, hivi leo unapomwambia mtu hii siyo nchi yako wakati sisi tunakaribisha wageni kosa analo nani? Ni sisi au yule mgeni aliyekuja? Tuamueni moja kama tunafanya kazi ya kuweza kuwalinda wageni tunyooshe moja kwa moja tuone mpaka mwisho na tuhakikishe kwamba tunawalinda wageni.

Kwa hivyo, naomba sana Mwanasheria Mkuu pamoja na Mhe. Waziri tufanye utaratibu wa kuanzisha *Tourism Court*, nawapongeza sana mmeanza kujenga mahakama nzuri sasa hivi mnajenga majengo mengi nimeona kule Mahonda, Tunguu tayari mnaendelea kwa *speed* na nimpongeze pia rafiki yangu Mhe. Mwanasheria Mkuu pia nimepata nafasi ya kumtembelea ofisi yake ni nzuri kabisa, kwa hivyo majengo yenu mengi mnajenga ni mazuri na kasi hii kisheri muiangalie pia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nataka niligusie la mwisho ni *issue* ya sadaka, najua kwamba sadaka haiko chini ya mkono wa kiserikali au wa kisheria. Lakini utaratibu niombe tu Mhe.

Waziri unapopata nafasi ya kuzungumza watu wanapotoka katika mwezi huu mtukufu wananchi wanapotoka kutoka sehemu tofauti kwa malengo ya kwenda kutoa sadaka, basi wanapoingia katika vijiji vyetu maeneo yote wasifanye zogo na kuwadhalilisha wananchi, wakati mwingine wanaingia unakuta watu wanakimbizana akinamama na kanga zao, mtu anatarajia leo atapata chakula anakimbizana alimuradi inakuwa wakati mwingine ule mpango unakuwa hauko mzuri.

Unapoingia kwenda kutoa sadaka hatukatai naamini ni jambo zuri na tuwaombe wananchi wetu waendelee kufanya, lakini si vibaya kama kuna uongozi wa vijiji, kuna Kamati za Maendeleo, kuna Wawakilishi, kuna Wabunge kuna Masheha basi wakahusishwa, ili yule mtu anapotaka kupeleka sadaka yake akaweka utaratibu mzuri kuliko unapoingia katika kijiji unasababisha zogo watu wanakimbizana inakuwa wakati mwingine haileti sura nzuri katika jamii na wale wananchi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, muda wangu umekwisha? Naona kama unaniangalia niendelee? Samahani Mwenyekiti naomba niendelee basi.

Lakini pia katika suala la ajira za wananchi. Mhe. Mwenyekiti, naomba upande mmoja mimi katika jimbo langu la Tunguu Wilaya ya Kati tuna majimbo matatu, tuna Jimbo la Chwaka, Jimbo la Uzini lakini pia na Jimbo la Tunguu. Naomba sana Mhe. Waziri apite aangalie katika utumishi huu tunaopata sisi katika maeneno yetu pia unaendana na huduma za wananchi, hasa katika jiografia hasa jimbo letu la Tunguu. Kwa mfano, katika kisiwa cha Uzi ukiangalia tunajua kuna mashirika hayako chini yake yeye lakini huduma za wananchi kutokana na mazingira ya visiwa kama kwa upande wa Mhe. Haji Omar Kheir lakini kwa upande wake yeye naamini Jimbo la Tumbatu na kisiwa cha Tumabatu wao wako mbele zaidi kimaendeleo kuliko kisiwa cha Uzi, kwa sababu wa umahiri wake mwenyewe anavyohangaika na kuwasaidia wananchi.

Kwa hiyo, naomba kwa jicho la huruma katika usimamizi wa watendaji lakini pia upande wa sekta ya afya pamoja na umeme pia, kwa mfano wakihitaji huduma za umeme, umeme ukikatika, waya zikifanya matatizo hawana watu najua kazi hizi ziko chini ya *ZECO* lakini ni vizuri pia Mhe. Waziri ukipata nafasi ukawatembelea, kwa sababu kisiwa hiki pia na wao wana haki ya kufurahi juu ya serikali yao, na mara nyingi kutokana na mazingira yao pia watendaji wanakuwa wanakusahau. Na unapopata fursa ya kwenda basi na rafiki yangu Mwanasheria Mkuu pia na yeye mchukue, ili aweze kutusaidia na tuweze kupata maendeleo haraka katika Jimbo letu la Tunguu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo leo Mhe. Suleiman Makame Ali amenifundisha maneno mazito leo ameniambia kule Pemba wana maneno wanasema hivi "Kumpa anaekupa hujatupa umeweka, ukimpa asiyekupa kuntupa" maana yake umetupa sasa mimi nasema leo sijatupa naweka kwa Mhe. Waziri kwa hiyo mimi sitopiga buti namuhakikishia naunga mkono hoja mia juu ya mia na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote wengine waunge mkono bajeti hii wampitishie Mhe.Waziri wampitishie bajeti yake bila ya kupiga buti kwa sababu ya usimamizi

wake ameonesha tofauti katika mwaka huu na mwaka wa jana amekuwa karibu na sisi sana Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza hili kwa hivyo. Kwa upande wa Jimbo letu la Tunguu naunga mkono hoja kwa asilimia juu ya mia na nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu na niwaombe tena Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama nimekohoa sikuwa na nia njema. Ahsante sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuichangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Mwalimu wangu Mhe. Haroun Ali Suleiman katika Wizara yake ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii nimpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu na Watendaji wote walio katika taasisi zake kwa kuiandaa ripoti hii ya bajeti ambayo kwa kweli imekaa vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nizipongeze kamati zote mbili ambazo zimewasilisha ripoti zao katika kuunga mkono na kutoa ushauri na mapendekezo juu ya ripoti hii ikiwemo Kamati ya Sheria Utawala Bora na ile Kamati yangu ya *PAC*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze pia Wajumbe walionitangulia kwa michango yao mizuri, baada ya hayo nielekee katika michango yangu. Lakini kabla sijenda ndani zaidi shukurani za pekee sana na pongezi nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa uamuzi wake wa kuweza kumteua Mwenyekiti wa Bodi ya *PAC* kutokana na umuhimu wa Bodi hiyo, nina imani sana kwamba baada ya uteuzi huo, yale mambo ambayo yalikwama kwa wenzetu wa Ofisi hii ya Mdhibiti ya uajiri wa wafanyakazi basi hivi sasa yatakwamuka ili kuweza kuona kwamba ofisi hii inapata Watendaji wa kutosha ambao wanaweza kusukuma gurudumu la maendeleo katika suala zima la Udhibiti na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, niwapongeze sana wenzetu wa kamisheni hii kwa utendaji wao wa majukumu mbali mbali kuweza kusimamia mali za Wakfu, kuweza kusimamia Mirathi, kuweza kusimamia Sala za Iddi lakini vile vile kusimamia masuala mazima yanayohusiana na Hijja na Mwenyezi Mungu atuwezesha wale wale ambao tuliokuwa hatujahiji basi atupe *taufiq* ya kuweza kutia nia hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo katika masuala ya kusafirisha mahujaji yamezuka makundi mbli mbali yenye lengo la kusafirisha Mahujaji katika nchi hii ukiacha ile Kamisheni yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mahujaji wengi wanapata usumbufu wengine wanashindwa kusafiri dakika za mwisho kabisa kutokana na mipangilio mibovu ya baadhi ya makundi hayo, lakini vile vile wengine wanapata usumbufu wanapokuwa kenye Hija zao juu ya huduma mbali mbali za baadhi ya makundi. Mhe. Mwenyekiti, niombe sana kwanza tuweze kuangalia kama haya makundi tunayasajili hapa Zanzibar basi tuweze kuwa na vigezo vizuri mpaka pale tutakapojiridhisha kwamba hili kundi lina uwezo kweli wa kusafirisha Mahujaji, kwa sababu inavyojionesha kuna baadhi ya makundi inaonekana yapo kibiashara kuliko kiimani. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri katika vigezo vya kuweza kuyasajili makundi haya basi suala hili liangaliwe, ili kuweza kuwafanya Waislamu wawe na moyo zaidi wa kusafiri kwa sababu wengine hawa ni Wastaafu pesa zao walizostaafu ndizo ambazo zinawawezesha kwenda Hijja sasa unapomkosesha katika mwaka ule aliotia nia basi inakuwa vigumu sana kuweza kusafiri katika mwaka mwingine na pengine Mwenyezi Mungu akachukua uhai wake kabla ya huo mwaka mwingine.

Mhe. Mwanyekiti, nikitoka suala la Hijja nielekee zaidi sasa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kwanza niipongeze ofisi kwa shughuli zake mbali mbali na mimi nina uhakika sana kutokana na Mwanasheria Mkuu na kazi zake basi ofisi hii inafanya kazi vizuri, na tayari amesifiwa hapa na Mhe. Sarahani Suleiman Said sina wasi wasi sana isipokuwa nizungumze mambo mawili katika ofisi hii. Ofisi hii ina jukumu la kuweza kuwathibitisha wanasheria mbali mbali ambao wamo katika taassisi mbali mbali za serikali, lakini serikali wakati mwengine inashitakiwa sasa kuna baadhi ya wanasheria ambao wamethibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wanamsimamia mtu binafsi kwa kesi ambayo serikali imeshitakiwa. Sasa hapa kidogo pana wasi wasi kama kuna wanasheria wawasimamie watu binafsi wakati wanasheria wale tumewaajiri ki serikali pale ambapo serikali inashitakiwa Mhe. Mwenyekiti Wanasheria wa aina hii mimi nimuombe sana Mwanasheria Mkuu awaangalie. Nimuombe sana Mwanasheria angalia Wizara ya Ardhi kuna Mwanasheria ambaye amemsimamia mtu binafsi wakati serikali imeshitakiwa, sasa sijui kimaadili kama mtu kama huyo tunamkubali.

Mhe. Mwenyekiti, nikibaki hapo hapo katika Ofisi ya Mwanasheria katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana 2017/2018 kulikuwa na takwimu ambayo ilikuwa inaonesha kanuni mbali mbali ambazo zimeshatayarishwa au zimetungwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mshangao mkubwa sana katika ripoti hii ya mwaka huu sijaona takwimu ya namna hiyo, sijui kama Mwanasheria kasahau lakini kuna kanuni ambazo zishapelekwa kwake zilizotayarishwa, lakini kama hakuna kanuni ambazo kwa mwaka huu zimetayarishwa Mhe. Mwenyekiti hili ni tatizo. Kwa kweli, Baraza hili na sisi ndiyo masuuli wa kuweza kutunga

sheria tumepitisha sheria nyingi, kutoka Baraza hili na hata lililopita sasa kama kuna hali ya kuzorota kwa kanuni au kutayarisha kanuni katika sheria mbali mbali ambazo zimetungwa Mhe. Mwenyekiti hii ni hatari.

Kwa mantiki hiyo, bila kanuni maana yake huwezi kuandaa miongozo na bila kanuni maana yake utekeleza wa sheria mbali mbali basi unakuwa mgumu sana na wakati mwingine unaweza ukawa unaleta migogoro. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kuweza kulisimamia hili, kuweza kuona kwamba sheria mbali mbali ambazo tunazitunga basi zinatungiwa kanuni, ili kuweza kurahisisha kuweka miongozo lakini vile vile sheria hizo ziweze kutekelezeka, lakini vile vile hata kamati yangu ya kanuni iweze kufanya kazi Barazani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi katika fungu N0. 7 ukurasa wa 30 hadi 32. Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii ni muhimu sana katika mustakbala mzima wa maendeleo ya nchi hii inafanya kazi kubwa sana, inatoa huduma mbali mbali inafanya makongamano, inatoa mafunzo, inatoa uelewa na kwenye kitabu hichi inaonekana kwamba kuna tuhuma 151 ambazo zimeripotiwa kwao, katika tuhuma hizo 151 kuna majalada 39 ambayo yapo kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (*DPP*). Niwapongeze sana kwa hilo. *(Makofi)*

Vile vile, imeokoa karibu shilingi milioni 169 hii ni hatua kubwa sana kwa taasisi. Lakini wasi wasi wangu katika utekelezaji wa majukumu yake taasisi hii ni kudhorota kwa kesi kwenda Mahakamani, nafikiri tokea taasisi hii iundwe na hata ile ripoti ya mwaka jana sijaona kama kuna mtu ambae ametiwa hatiyani kutokana na makosa ya rushwa au kuhujumu uchumi, au matumizi mabaya ya mali ya umma au matumizi mabaya ya ofisi za serikali. Kwa kweli, hapa nina wasi wasi mkubwa na kuna baadhi ya kesi watu wanakamatwa *redhanded* hapa ndio wasi wasi wangu, kwamba kuna mkwamo gani kwa taasisi hii kushindwa kuwafikisha hawa wahalifu mahakamani na huku wanaendelea kuhujumu uchumi.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri aitazame vyema hii taasisi najua anaimarisha hivi sasa kuna mpango wa kuwajengea ofisi. Lakini lengo kubwa zaidi ni kukomesha hali ya rushwa, uhujumu uchumi na matumizi mabaya ya mali ya umma, pamoja na matumizi ya ofisi za serikali. Sasa kama hakuna watu ambao wanaingia hatiyani tunabaki tu na *files* katika Afisi ya *DPP* hii ni hatari sana hali hii inaweza kutufikisha pabaya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nifikie hapo nimalizie hapo kwa sababu michango mingi itatolewa na wenzangu. Naipongeza sana kwa mara nyengine ofisi hii kwa kazi zake nzuri na ripoti yake nzuri, niwaombe wenzangu kuweza kuichangia hotuba hii na wampe moyo sana Mhe. Waziri, ili hotuba hii iweze kupita bila ya tabu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni naiunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi sina budi kurudisha shukurani zangu nyingi kwa Mwenyezi Mungu kunijaalia siku hii ya leo ya Alhamis Mwezi mosi Ramadhani tukakutana hapa tena, ni bajeti au hotuba iliyopata baraka ya kwanza ya mwezi wa Ramadhani. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuwatakia Waislamu wote duniani Ramadhani Kareem na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuifunga Ramadhani na atukubalie funga yetu, Mwenyezi Mungu tunakuomba utukubalie funga yetu tunayoifunga.

Lakini pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana na kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake wa busara, makini na uliojaa hekma kila siku nikisimama hapa nasema kwamba uongozi wake na busara zake ndio zilizoweza kutufikisha hapa leo tulipo, bila ya hekima na busara yake tusingekuwepo leo japokuwa kila kitu Mwenyezi Mungu mwenyewe anakipanga, lakini asbabu ya binaadamu ipo na asbabu ya kuwa utulivu na amani tulionao na yeye kachangia kwa kiasi kikubwa kukosekana na kuwa yeye kuwa na busara kama alivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu narudia tena kusema tusingefika hapa. Tumuombe Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na ampe maisha marefu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu leo nitaanza kujikita moja kwa moja na ukurasa wa 11 katika Programu ya Usimamizi wa Masuali ya Dini, kama tunavyojua Ofisi ya Mufti ndio tuliyoikabidhi jukumu hili mwenzangu Mhe. Suleiman Sarahan Said kazungumza mengi kuhusiana na hili lakini na mimi nina mchango wangu ambao nataka Wazanzibari wausikie kuhusiana na hili.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kunukuu kifungu cha 29 kinasema hivi:

> "Katika kuendeleza jitihada za kuwa na takwimu sahihi za idadi ya hali halisi ya misikiti na madrasa hapa Zanzibar, Ofisi ya Mufti imesajili madrasa 104 na misikiti 61 ya Unguja na Pemba na ukaguzi umefanyika katika Vyuo vya *Qur-ani* 58 na misikiti 50 na mashauriano kuhusu changamoto yamefanyika, ambapo ushauri ulitolewa kuhusiana na maendeleo ya taasisi hizo".

Mhe. Mwenyekiti, nina ushauri na naomba Ofisi ya Mufti aupokee na auangalie na uzito wake, tumekuwa na utitiri wa misikiti inayojengwa katika nchi yetu kila kona unayopita leo kuna msikiti, kila pembe unayopita leo kuna msikiti, hatusemi kwamba misikiti isijengwe, isipokuwa tunasema kwamba misikiti ijengwe lakini kwa utaratibu. Hata hiyo enzi ya Mtume Muhammad (*S.A.W*) msikiti tulipewa maelekezo kwamba ujengwe pale itakaposikilikana adhana. Sasa leo anatambiwa ameratibu misikiti 60 hiyo mimi nataka niulize hii misikiti ni yote kama alivyosema na kwa nini hiyo mingine hawajairatibu wakaijua ilivyo ni mingapi.

Kwa hiyo, natoa ombi kwa Ofisi ya Mufti kwamba tuangalie ujenzi wa misikiti kwa sasa na tuweke utaratibu kwa kudhibiti ujenzi wa misikiti, kwa sababu ujenzi wa misikiti ni moja kati ya inayosababisha mizozo, kwa sababu leo kiongozi na msimamizi wa misikiti akiona kama mimi jambo hili sikulitaka basi anaanzisha msikiti wake, anachukua waumini watano, sita, kumi, kumi na tano anakwenda kuanzisha msikiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika jimbo langu pale kwa hesabu ya haraka haraka pale mjini pale pana misikiti zaidi ya minane au kumi au misikiti minane inayosaliwa Ijumaa, hivi tujiulize hakuna amali nyengine ya *khairat* nyengine zaidi ya kujenga misikiti. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Ofisi ya Mufti pamoja na serikali kuanzia sasa ushauri huu naomba uzingatiwe kwamba ujenzi wa misikiti uwe chini ya Ofisi ya Mufti na itoe vibali kwa ujenzi wa misikiti mipya, jambo ambalo litatupunguzia mizozo katika misikiti yetu. Badala yake wale watu wanaotaka kujielekeza kutenda mema tuna mambo mengi, tunavyo vyuo hapa walimu wetu wa vyuoni hawana maposho wale wanaotaka kusaidia mambo ya *khairat* ni vyema wakajikita wakasaidia vyuo vya *Qur-ani* kuliko kuendelea kujenga misikiti ambayo tunayo mingi na waumini ni hao hao kila siku. *(Makofi)*

Kwa hivyo, jambo hili nilikuwa naliona la kwanza lizingatiwe Ofisi ya Mufti itoe vibali na ione kama kweli iko haja ya mahala pale kujengwa msikiti. Vile vile, kwa wale wanaotaka kuelekeza katika mambo yao ya *khairat* tuna nafasi ya kuchimba visima na kuviendeleza visima vilivyopo pia ni jambo la *khairat*, wajielekeze katika kuchimba visima jambo ambalo litasaidia wananchi pamoja na serikali yenyewe na mambo ya *khairat* yake na thawabu zake na ni sadaka yenye kuendelea nayo yatajitokeza na atapata fungu lake kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka niende katika ukurasa wa 12 unaozungumzia mitaala, kama nilivyozungumza kwamba vyuo vya *Qur-ani* ni muhimu katika dini elimu ni muhimu katika dini. Kwa hivyo, naipongeza sana ofisi hii kwa kuandaa utaratibu wa kuanzisha mtaala, ili vyuo vyote viwe vinaendana na ikiwezekana wafanye mitihani kwa vyuo kwa ngazi zote, hili jambo litasaidia sana katika kupata elimu kwa watoto wetu watajua vipi wanakwenda na tutapata njia ya kuwapima elimu waliyoipata katika vyuo tofauti. Hivyo, nachukua fursa hii kuipongeza sana Ofisi ya Mufti kwa kuanzisha utaratibu huo na nawaomba waendelee na isiwe katika maandishi tu iwemo katika vitendo tuione kwamba kwenye mwaka huu imeanza na inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ndio nataka nijikie katika Chuo cha Utawala wa Umma, chuo hichi wanasema wametoa mafunzo kwa watumishi wapya na mimi napenda ninukuu kifungu cha 52 wanasema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kifungu cha 52 kinasema hivi:-

> "Mafunzo ya maadili ya kazi watumishi wapya wametolewa kwa watumishi 3902 kutoka wizara na taasisi za serikali ikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Afisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *SUZA*, Shirika la Umeme *ZECO* na *ZURA*".

Leo asubuhi nililisikia swali la Mhe. Suleiman Sarahan Said na jinsi ilivyompasa Mhe. Waziri wa Afya ajibu atoe maelezo ya kina juu ya utumishi wa Wizara ya Afya. Mhe. Mwenyekiti, nataka niulize kwa nini Wizara ya Afya sikuwaona au haya mafunzo Wizara ya Afya hayakupelekwa. Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho namuomba aniambie kuhusiana na Wizara ya Afya, katika hao mliowapa mafunzo Wizara ya Afya mmewapelekea.

Kwa sababu leo mimi ni imani yangu naamini kwamba watu wa Wizara ya Afya ndio wanaotakiwa wafundishwe maadili zaidi kulikoni sehemu nyengine yoyote kwa sababu hawa wanadili na jamii, tena jamii ambayo wanakwenda pale wakiwa wagonjwa wanataka huduma, wanataka kunyenyekewa wanataka kupewa mambo yote yanayostahiki mgonjwa, lakini leo tumeshuhudia kwamba unaweza ukenda hospitalini muuguzi au nurse akamjibu neno analolitaka ambalo halimridhishi yule mgonjwa kinyume na matarajio kama alivyosema Mhe. Suleiman Sarahan Said pale.

Kwa hivyo, kupewa elimu hii kwa watumishi wa taasisi za serikali nilikuwa napendelea mimi na nashauri kwamba elimu na mafunzo ya maadili yaelekezwe sana Wizara ya Afya, kwa sababu Wizara ya Afya inalalamikiwa hata sisi waheshimiwa tunalalamika sana kuhusiana na watumishi wa Wizara ya Afya kutokana na huduma, hii zamani ilikuwa ina ukosefu wa nidhamu na maadili huwezi kufanyakazi ikawa na mwelekeo mzuri. Lakini mafanikio ya kazi yanapatikana pale panapokuwa na nidhamu na maadili ya kazi yakawepo ndipo tunapopata mafanikio makubwa katika kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa niingie katika Mahakama tumeiona Mahakama ilivyo Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Mahakama wana kazi kubwa Mahakama ni watu tunaowategemea baada ya mtu kufanywa aliyofanywa, kila mtu mwenye matatizo yake anakimbilia Mahakamani. Lakini leo tunakuta Mahakama nikiiona hapa na nikiitizama hapa katika bajeti yao wamepangiwa matumizi ya uendeshaji wa ofisi shilingi bilioni 1,515,100,000/= ruzuku bilioni 1,113,800,000, vipi kwa mwaka Mahakama zote tulizozisajili na tulizonazo Zanzibar kuanzia Mahakama ya Rufaa mpaka Mahakama za Mwanzo wanaweza kuendesha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwamba watumishi wa Idara ya Mahakama, Majaji, Mahakimu kuwa kuanzia Mahakama ya Mkoa hadi chini waangaliwe upya, leo tukiangalia pale Mhe. Mwenyekiti, *OC* ndogo hata zile pesa za kuwaita mashahidi saa nyengine zinakosekana tunasema hakuna kesi bila ya ushahidi, shahidi ukimwita huna pesa hakufuati akijua yeye anakwenda kule hana hata nauli hakufuati, matokeo yake kesi inakosa ushahidi inatupwa, wananchi wanalalamika hawajatendewa haki. Tatizo ni kwamba shahidi hakutaka kwenda kwa sababu anajua mimi uwezo wa kwenda kutoa ushahidi pengine katoka Konde kwenda Wete shilingi elfu nne ya kwenda na kurudi hana.

Kwa hivyo, naomba sana suala hili liangaliwe na waongezewe *OC* hawa katika Idara ya Mahakama kwa ajili ya kuweza kuwaboresha kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. Sambamba na *sitting* hawa ni watu muhimu na ndio pale tunapowakosesha *sitting allowance* za kutosha ukakuta saa nyengine mtu binaadam roho anakwenda anaingia katika mkono ambao hakuutegemea kutokana na hali yake ilivyo. Kwa hivyo, niwasihi tu na niwaombe sana kwamba suala hili la Mahakama liangaliwe upya na lipewe kipaumbele wa kibajeti wa aina yake.

Lakini nikitoka kwenye Mahakama nataka atakapokuja Mhe. Waziri aniambie Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwenye ripoti yake kidogo alinifilisi wala si kidogo, kwa sababu nilitaka nijue kwanza ripoti ya miradi mbali mbali inayotekelezwa lakini ambayo ripoti zake tokea mimi niingie hapa Barazani mpaka leo haijaja.

Kwanza nilikuwa napenda nizungumzie ripoti ya mkaguzi ya *CAG* inayohusiana na Mkonga wa Taifa, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje aniambie ripoti hii ya ukaguzi ya Mkonga wa Taifa italetwa lini hapa Barazani tutaiona na sisi tokea siku tulipoingia hapa hatujaiona, hatujaisikia sambamba na miradi kama ule Mradi wa Ujenzi Kiwanja cha Kufurahishia Watoto cha Kariakoo na kile cha Tibitinzi kilichoko Pemba na miradi mingine mikubwa ya serikali ambayo inatekelezwa, atakapokuja naomba Mhe. Waziri unihafamishe na wala sina dhamiri ya kumzuilia bajeti kwa sababu ni mwalimu wangu namheshimu namuogopa. Lakini na atakapokuja hapa namuomba hili anielezee ili na sisi kiu yetu ipungue kwa kujua lini mambo haya tutayapata, ripoti hii itafika ambayo tunaisubiri kwa hamu sana.

Mhe. Mwenyekiti, tukenda kwenye Tume ya Utumishi tuliangalia na atumeona jinsi gani miradi ya maendeleo kwenye Mahakama, narudia tena kidogo sikumalizia pale kwenye Mahakama kwamba hawa kwenye ujenzi wa Mahakama ya Tunguu wamepanga shilingi bilioni 5. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana najua Mhe. Rais mwenyewe analo na Mhe. Mwenye jimbo kalizungumza vya kutosha, isipokuwa nakazia pale kwamba miradi kama hii ipewe kipaumbele cha aina yake, ili iweze kutekelezeka kama ilivyo.

Lakini, nilikuwa pia nimeona kwenye mchanganuo wa kimahakama kuhusu kesi za madai ambazo kama Mahakama ya Vuga kwa mwaka huu wanasema kwamba 2017/2018 kesi 98, lakini zilizotolewa aumuzi ni tano. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Mahakama Kuu nafahamu pamoja na matatizo yaliyopo lakini kuna kesi nyingi ambazo zipo Mahakama Kuu hazijapata uamuzi mpaka leo. Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu nakumbuka kuna kesi sipendi nizitaje hapa lakini wenyewe watu wa Mahakama Kuu wanazijua tokea mwaka 2013 ambazo ziko Mahakama Kuu kwa maana ya kuu nafikiria tayari watakuwa wameshanifahamu tokea mwaka 2013.

Kutokana na hali hiyo, naiomba sana Mahakama Kuu kesi hizi wazitolee uamuzi, ili wale wananchi wajijue vya kwenda wajuwe vya kuishi. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kupitia hotuba hii Mhe. Waziri, wewe ndio mwenye wizara tuwaombe watu wa Mahakama Kuu hasa zile za Rufaa, kesi zilizokuwepo kwenye Mahakama Kuu ya Rufaa na zitolewe uamuzi, zirahisishwe kutowa uwamuzi. Haiwezekani kwamba Mahakama Kuu ina rufaa ya mwaka 2013 iwe mpaka leo iwe haijapatiwa ufumbuzi Mhe. Mwanasheria Mkuu unanitizama lakini huo ndio ukweli, zipo kezi ambazo mimi nazifahamu kutoka 2013 zinahusu jimbo langu mpaka leo hazijatolewa. Kwa hivyo, nakuombeni sana mzitolee uamuzi, ili wale wananchi wajue aliyepata au aliyekosa ajue.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni kuhusiana na Ripoti za Mkaguzi na Mdhibiti wa Mkuu wa Hesabu za Serikali, tulikuwa tunawaona wenzetu Bara inapokuja ripoti ikamgusa mtu au taasisi ambayo imepata hati chafu, taasisi ile inachukuliwa hatua haraka iwezekanavyo. Kwa kweli, tumemsikia mwenyewe Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Joseph Pombe Magufuli jinsi walizozifanish zile idara ambazo wamepata zimepata hati chafu, lakini leo sisi kwa masikitiko kuna taasisi ambazo zimepata hati chafu kutoka ripoti ya 2014/2015, lakini mpaka leo hatuoni kwamba kuna hatua yoyote japo kwa hatua ya awali. Hivyo, naomba na sisi taarifa zile tukazipata ili na sisi tusiweze kuhoji jambo jengine, lakini vyenginevyo itakuja taarifa na sisi tutapata nafasi ya kuhoji, je utekelezaji yale ya awali umekuwaje jambo lile si zuri kujadiliwa kila wakati Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba ni vyema na busara kabla ya kuja kwa taarifa au ripoti yengine ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Serikali, tupate muendelezo wa ile ripoti matokeo yaliyotokea kwenye ile ripoti iliyotanguliya kabla ya kupokea ripoti nyengine si vizuri sisi tunajiuliza ah! Ripoti ya mwaka 2014/2015 imekuja na imetajwa moja, mbili, tatu lakini na leo inakuja hii bila ya kuona matokeo ya ripoti iliyotangulia.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna imani sana mimi mwenyewe nina imani sana na Ofisi ya *CAG* kama anafanya kazi zake vizuri, lakini hili tatizo la kutokuwa na ripoti ya utekelezaji kwa zile ripoti zilizotangulia ni jambo ambalo linatuweka katika njia panda. Kwa hiyo, naomba sana kwamba jambo hili liangaliwe na lichukuliwe hatua.

Mwisho naona nataka kunamwia lakini nazungumzia Idara ya Utumishi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, idara hii kama tunavyofahamu ni muhimu, tena ina majukumu mengi. Mhe. Waziri, tunaiomba idara hii kwa wale watumishi wa umma ambao, wamekutwa na matatizo katika ripoti zao za ukaguzi, haraka iwezekanavyo wachukuliwe hatua za kinidhamu kama inavyoelekeza kwa mujibu wa Kanuni ya kuanzia 48 hadi 53 juu ya adhabu, ambazo wanapewa watumishi pale wanapokwenda kinyume na wanavyovunja Maadili wa Utumishi wa Umma.

Kwa kweli, bila ya kuwa na msimamo kama huu Mhe. Waziri, kila siku watumishi wetu wataendelea kurejea makosa yale yale, kwa sababu wanaamini kwamba hataweza kuchukuliwa hatua kama zilivyoelekezwa. Lakini, sheria pamoja na kanuni zipo, ziko wazi na ukizisoma utaziona. Kwa hiyo, nakuomba sana Mhe. Waziri wewe ndio mwenye wizara na hizi taasisi ziko chini yako na utakapokuja unambie kwamba ni watumishi wangapi waliochukuliwa hatua za kinidhamu baada ya kuonekana au kupatikana na matatizo katika taasisi zao au hakuna mtumishi aliyepatikana na makosa baada ya kufanyiwa hiyo *vetting*.

Baada ya haya Mhe. Mwenyekiti, sina shida leo ya kuzuia shilingi wala kufanya lolote kwa Mhe. Waziri, mwalimu wangu namheshimu, nampenda na nasema naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Lakini namuomba Mhe.Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe majibu ya masuala yangu niliyoyauliza. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma akifuatia na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma ajiandae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu kabisa nikaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri ambaye ni Mwalimu wangu Mhe. Mwalimu Haruon Ali Suleiman, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba na Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa bajeti hii ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, sina mambo mengi katika hotuba hii, kwa sababu kwanza tunawapongeza kuanzia Mhe. Waziri pamoja na timu yake yote kwa uchapaji kazi nzuri, lakini vile vile kuwa wasikivu kwa yale yote ambayo kila mwaka huwa tunajaribu kuwashauri. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti kimsingi kwa mwaka huu kwa hotuba hii, nitakuwa sina mambo mengi.

Isipokuwa nilikuwa nataka nianze kutoa pongezi kwa upande wa Mahakama kwa kweli Idara ya Mahakama inafanya kazi nzuri, namshukuru sana Mhe. Jaji Mkuu pamoja na Majaji wa Mahakama Kuu pamoja na Mahakimu kazi wanafanya nzuri. Lakini zaidi kwa jinsi walivyoandaa programu ya uboreshaji wa majengo yao, kwa kweli tunawapongeza sana angalau sasa hivi wale Mahakimu wetu wameanza kupata ladha ya kuhukumu kesi, kwa sababu kwa kweli Mahakimu wetu hawa ni watu ambao au Majaji wetu ni watu ambao wanastahiki heshima kubwa ndani ya serikali yetu. Kwa hiyo, kupitia programu ya ujenzi au ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa kweli tunafarijika sana na tunaomba waendelee na mtindo huo huo. Sasa bado kuna baadhi ya Mahakama yengine hali zake za majengo hazijakuwa vizuri, lakini tunaamini ndani ya programu hii wataweza nazo kuziboresha.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hii ya Mahakama kuna maombi mawili moja kwamba ukiacha Mahakama zetu hizi ambazo zipo katika ufumo wa Mahakama lakini tuna Mahakama ya Ardhi, ambayo kwa mujibu wa sheria tulizozitunga kwamba sasa hivi kuna Mahakama ya Ardhi za Wilaya lakini vile vile na za Mikoa. Kwa kweli ni jambo ambalo nnalosikitika na hili namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe ufafanuzi kuhusu stahiki za Mahakimu wetu wa Mahakama za Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa tunaye Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi, kwa mujibu wa *status* yake ana hadhi ya sawa sawa na Hakimu wa Mkoa, lakini kimsingi mpaka sasa hivi zile stahiki zake za kushika nafasi mpaka hii leo bado hajazipata. Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti nitakuja kuzuia fungu mpaka nihakikishe kwamba, Hakimu wetu huyu au Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi anapatiwa stahiki zake, kwa sababu hawezekani yeye anawasimamia mahakimu wengine katika kutoka haki hasa katika migogoro ya ardhi, lakini yeye mwenyewe anasimamia haki, lakini yeye mwenyewe haki zake mpaka leo hajazipata. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi alipwe haki zake lakini vile vile, pamoja na *arrears* ya tangu alipokamata au aliposhsika ile nafasi.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika hapa hapa Idara ya Mahakama kuna suala zima la mafunzo, hawa Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi na wao vile vile ni Mahakimu ambao wametoka huko huko Mahakamani, lakini tangu kupelekwa kule ardhi wamekuwa kama watoto wa kambo, yaani hawajijui, kwa sababu kule walipo ni taasisi ya kiraia, kule waliko hakuna sheria wala kitu chochote, wao ndio wamepelekwa kule kwa ajili ya kusimamia haki za wananchi. Lakini yanapotokezea mafunzo ya Majaji au Mahakimu wao nafasi zile hawapelekewi sasa Mhe. Mwenyekiti ulimwengu wa sasa hivi kila siku dunia inabadilika, sheria zinabalika kwa hivyo, zinapobadilika sheria Mhe. Mwenyekiti na wale Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi na wao wanatakiwa wawe *updated* vile vile, wapate yale mafunzo pamoja na Mahakimu wenzao ili wanapohukumu zile kesi kwa kweli na nao waweze ku-*cop* kwa mujibu wa mabadiliko ya sheria, lakini vile vile, kwa mabadiliko ya mambo mbali mbali ya kidunia.

Sasa nilikuwa naomba sana katika Idara hii ya Mahakama mambo hayo mawili suala la stahiki la Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi pamoja na *arrears* zake toka siku aliposhika nafasi, lakini vile vile suala la mafunzo au yakupatiwa semina pamoja na *incentives* nyengine ambazo mahakimu wengine wanazipata.

Mhe. Mwenyekiti hilo nimejaribu kuliogelea sana, kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia masuala ya ardhi, naona jinsi wanavyofanya kazi nzuri sana, lakini kwa kweli unapokuja kwenye maslahi pamoja na *incentives* nyengine kwa kweli wanakuwa wako nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, naipongeza sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kweli sasa hivi tunashukuru, hata yale mambo yalikuwa yanakwenda ndivyo sivyo katika taasisi zetu mbali mbali, kwa kuwa sasa hivi mikataba yote lazima ipitie kwa Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo, tunashukuru sana na tunaona ni namna gani serikali yetu ilivyokuwa makini katika kusimamia haki za wananchi pamoja na maslahi ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia katika G04, limeangalia Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka tunampongeza sana bosi wetu wa zamani ambaye ametulea ametufundisha kazi hapa Barazani, ambaye sasa hivi ni Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kweli kazi kubwa anafanya. Lakini kitu ambacho nnachosikitika kwenye ile *column* yake yeye kuna *paragraph* mbili tu sasa sijui Mhe. Waziri alikuwa na uhaba wa karatasi au vipi, kwa kweli *paragraph* mbili kwa Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kwa majukumu na kazi nyingi anazozifanya nafikiri hakutendewa haki. Lakini pamoja hayo tunampongeza sana kwa kazi nzuri ambazo wanazozifanya.

Sasa, naomba katika G08 Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, kamisheni hii siipongezi na siipongezi kwa sababu bado tuna mgogoro wa kimaslahi baina ya Baraza la Wawakilishi na Kamisheni hii ya Utumishi wa Umma, bado tunadai na Mwanasheria Mkuu tunamtaka hili aendele kutusikiliza. Kwa hivyo, tunaomba kufanywe marekebisho ya Katiba ya Zanzibar kuhakikisha kwamba Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi inakuwa huru haisimamiwi na taasisi nyengine yoyote, kwa sababu Baraza la Wawakilishi ni muhimu na muhimili hautakiwi uwe chini ya muhimili.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kifungu hichi cha Kamisheni ya Utumishi wa Umma, hata wakati wa kupiga zile kura hata sauti yangu utoisikia, kwa sababu wanaisimamia kinyume cha taratibu za utawala bora tume mbili za utumishi, Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi na Tume ya Utumishi ya Idara Maalam. Kwa kweli, bado suala langu hili nitaendelea kupambana nalo Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi inatakiwa ile mwamvuli wowote ambao uko juu yake, hiyo inatoa *separation of power*, lakini hapa hakuna *separation of power*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika Tume ya Utumishi Serikali, Mhe. Mwenyekiti hapa kuna maneno kidogo. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tukiangalia kuna wataalamu wetu wengi ambao wana sifa ambazo sifa zile zilikuwa zinastahiki wapate stahiki fulani, lakini mpaka leo maombi yamepelekwa kupitia idara mbali mbali na taasisi mbali mbali mpaka katika mashirika ya serikali, lakini bado stahiki zao zimekaliwa na Tume ya Utumishi Serikalini. Kwa hivyo, tunaomba sana, Mhe. Mwenyekiti hawa ndugu zetu au vijana wetu wanasoma wanakwenda vyuoni wanatia mpaka mikuu kwenye mabeseni kwa ajili ya kusoma, sasa leo wanapofika pahala wameshapata ajira wanafanya kazi nzuri na elimu wanazo maslahi yao kuweza kukaliwa kwa kweli sio jambo sahihi.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti yale maombi yanayotoka katika mashirika mbali mbali ya serikali lakini vile vile, na taasisi mbali kuhusu stahiki za watendaji wetu naomba sana wazikalie kikao nawatengeneze hasa programu, kwa sababu kuna njengine zimeshapelekwa

zaidi ya mwaka mmoja, lakini jawabu hakuna. Kutokana na hali hiyo, inawarejesha nyuma watendaji wetu hasa katika suala zima la uwajibikaji na uchapaji wa kazi katika taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tunaona katika baadhi ya mashirika binafsi watu wanaekewa *perfomance contract* mtu anaambiwa ukifanya kazi hivi vizuri utapandishiwa *bonus* au kama mfano mabenki wanaambiwa mkiweza kuzalisha au mkiweza kuleta faida ya kiasi fulani basi gawiyo asilimia fulani mtapatiwa nyie. Sasa na hawa watendaji wetu pamoja kwamba hawafanyakazi pengine katika maeneo ambayo yanazalisha sana lakini ule uwajibikaji wao na utaalamu wao na sifa zao tunahisi waweze kupatiwa hayo maslahi yao.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, bado tunao watumishi ambao wameshastaafu wanaendelea kupapigwa mikataba mara mbili, mara tatu kwa kweli hili suala halipendezi wala halifurahishi. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hii Tume ya Utumishi Serikalini kuna vijana wengi sasa hivi tunashukuru serikali yetu tumeanzisha vyuo vikuu, vijana wengi wanasoma kuna wengine wamewapelekwa nje ya nchi wanasoma basi wapewe hizi nafasi tena wale wengine wapumzike. Sasa hili Mhe. Mwenyekiti, ikiwa serikali yetu itatengeneza utaratibu wa kuwatengenezea mafao yao wakati wa kustaafu hakuna mtu atakayeendelea kung'ang'ania kutaka kufungiwa mikataba ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hili pengine linatokana pengine labda na maslahi tunayowapangia baada ya kustaafu yanakuwa madogo, ndio mara nyingi watu wanaendelea kung'ang'aniana mikataba lakini wengine wanakosa ajira ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie la mwisho Ofisi ya *CAG*. Mhe. Mwenyekiti Ofisi ya *CAG* ni ofisi kubwa sana, unaweza ukasema ni nusu ya muhimili kwa sababu hii haitakiwi kuingiliwa ingiliwa na mamlaka jengine yoyote. Lakini, Mhe. Mwenyekiti naomba sana hii ofisi ili iendelee kuwa na heshima zake kuna baadhi ya mambo madogo madogo na manunguniko madogo madogo haya ni vizuri yakawekwa sana, ili heshima ya ofisi hii iendelee kuwa nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya changamoto ambazo zinazojitokeza na nitaomba Mhe. Waziri ukija uje ututolee maelezo, ofisi hii mimi nnavyojua kwa muda mrefu ina upungufu wa watumishi ndani ya taasisi ile, lakini leo tunaambiwa kuna watumishi ndani ya ofisi hiyo hiyo wamehamishwa wamepelekwa katika idara nyengine za serikali. Sasa je, leo kama sisi wenyewe tunahitaji kuwaajiri watu kwa mkataba kwa ajili ya kutusaidia kazi, lakini leo sisi wenyewe tunapunguza watu tunawapeleka kwenye sehemu nyengine.

Kwa hiyo, hapa nadhani lazima tujaribu kupaangalia vizuri pia naomba sana Mhe. Waziri eneo hili nitakuja kupiga buti vile vile, katika maeneo ambayo napunguza asilimia ishirini katika bajeti hii na eneo hili nitapunguza, ili tuweze kupata maelezo ya kina, tuambiwe sababu ya *transfer* ya watu hawa wakati ofisi yenyewe inahitaji watumishi wa kuweza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, haya waliyoyazungumza wenzangu na mimi nitakuwa nayaunga mkono kwa sababu Kanuni zetu hazitutaki kurejea rejea, lakini ofisi hii kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti hii ni nusu ya muhimili inatakiwa iwe na heshma kubwa sana. Kwa mfano, hata Mhe. Waziri mwenyewe anatetemeka unapogusa Ofisi ya *CAG*, kwa sababu hata na yeye hatakiwi kutia

mkono kule. Lakini, kama itakuwa kuna taarifa kidogo hazipendezi itabidi Waziri akaingilie mamlaka ambayo kidogo Kikatiba pia inakuwa sio nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hayo yalikuwa ndiyo ya kwangu katika hotuba hii. Lakini vile vile samahani Mhe. Mwenyekiti, najua nimebakisha dakika zangu tano nilikuwa nataka nizungumzie Chuo cha Utumishi wa Umma ambacho na mimi kwa bahati nzuri nilipita pale na nashukuru haya mengi ninayoyasema hapa niliyapata kupitia pale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa nilizokuwa nazo kwanza tulikuwa tukipiga kelele sana kwamba kile chuo angalau kianzishe *degree*, kwa taarifa niliyoipata sina uhakika lakini Mhe. Waziri atakuja kunieleza kwamba tayari chuo sasa hivi kinatoa *degree*, kwa sababu kulikuwa kuna wale wanafunzi walikuwa wanasoma *International Relation* walikuwa wanalalamika kwamba wanasoma wakishakufikia *diploma* wanashindwa kupata *degree* inabidi waende Bara, nafikiri sasa hivi tayari.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya wanafunzi ambao walisoma pale waliingia wakapata *certificate* pia wamepata *diploma*, tunaambiwa wanazuiwa wasisome *degree*. Sasa, hii Mhe. Mwenyekiti kama wao wenyewe wamewasomesha wakawapa *certificate*, wakawapa *diploma* leo kwa nini wanawazuia wasipate *degree*. Kwa hiyo, hili namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anipe maelezo ya kutosha, ili vijana wetu hawa wasibakie mtaani wakajikunja, wakajikunyata mikono.

Baada ya hayo machache, namalizia kwamba tumepata taarifa kwamba jengo linavuja. Kwa kweli, hili naomba sana Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* vile vile na *CAG*. Mhe. Mwenyekiti, tunayo majengo mengi ya serikali hivi sasa ambayo yamejengwa kwa gharama kubwa na majengo ya kisasa, lakini yanavuja inakuwa ni aibu kubwa kwa nchi yetu. Kutokana na hali hiyo, hatujasikia mkandarasi yeyote akachukuliwa hatua au *consultancy* ambaye aliyekuwa anasimamia ule ujenzi. Miongoni mwa majengo hayo kwa taarifa tuliyokuwa nayo ni Chuo chetu cha Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, hili namuomba Mhe. Waziri alifuatilie na kama kuna mtu ambaye hakuwajibika vizuri katika kazi yake naomba asimamie vizuri pamoja na hatua za kisheria zichukuliwe.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hotuba hii kwa asilimia thamanini na asilimia zangu ishirini nazibakisha baada ya maelezo kwa Mhe. Waziri, Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Matar atafuatiwa na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mchana huu kunipa fursa hii niweze kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi nitoe shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kila hali. Pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake katika kukitayarisha kitabu hichi, pamoja na kamati ambayo imetoa maoni yao, naomba sana yazingatiwe maoni ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nina masikitiko kidogo kwa mwalimu wangu katika kuandaa kitabu hiki, kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mara nyingi anatukosoa katika lugha juu ya kuienzi lugha yetu ya Kiswahili kwa haya baadhi ya maneno aliyotumia kwa nini anatumia maneno kama haya *program* na yeye huwa anakataza kabisa kuchanganya changanya maneno, lakini na yeye kayarudia sijui kwa nini, baada ya hayo tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu upo katika ukurasa wa 6 Programu ya Usimamizi na Utumishi wa Umma kifungu 21. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Kifungu cha 21 kinasema kwamba:

> "Programu ndogo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi ina lengo la kuimarisha mfumo wa miundo ya kiutumishi na maslahi ya watumishi. Kazi ya kuwapanga watumishi wa umma katika miundo ya utumishi kwa mujibu wa sifa zao za kielimu, …"

Mhe. Mwenyekiti, hapa nina hoja zangu kwa Mhe. Waziri, hivi ni sababu gani, mwaka jana nilizungumza suala hili na leo nalirudia tena, kuhusu wasaidizi wahasibu waliokuwepo Pemba kupata stahili zao. Jambo ambalo kuwa lilizungumzwa hapa mwaka jana na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ambaye anasimamia wahasibu amelikubali na afisi yake tayari imepelekewa kupitia tume, lakini hadi leo watu hawa hawajapata stahili zao. Kwa kweli, kama ni mhasibu wa taasisi ile ile ya serikali wenye sifa moja kwa nini maslahi wapitane.

Mhe. Mwenyekiti, mfano kama kule Pemba anaweza kuwa mhasibu katika Ofisi hii ya Rais, Katiba na Sheria anapata haki sawa na huku Unguja, lakini taasisi nyengine kama msaidizi mhasibu wa Baraza la Wawakilishi hawezi kupata kama hizo, kwa nini? Naomba atakapokuja anipe maelezo kitu hichi kwa nini kikafanyika hivi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa 23 kuhusu ufatiliaji, kifungu hichi kinazungumzia masuala mazima ya ufatiliaji. Je, wizara yako inafuatilia kuona kwamba waajiriwa wote wa serikali katika kujaza mikataba hii ambayo unasimamia katika kifungu hichi, ninavyoeleza wanapata kopi zao. Walio wengi anakwambia nimejaza mkataba lakini hana kopi, mimi mwenyewe binafsi nimeona wakati wa miaka ya nyuma mtu anafika kutengenezewa kiinua mgongo mkataba wake wa kazi haupo.

Kwa hivyo, ni vyema suala hili litiliwe mkazo kwamba unapotayarishwa mkataba na yule anayejaziwa mkataba awe na kopi yake kamili pamoja na Ardhilhali zote kama za kuingiziwa kazini awe nazo. Isifike wakati kwamba kuambiwa mkataba haupo, hili ni jambo kwa kweli nimeshalishuhudia na naomba lisiendelee. Lakini hata wale wafanyakazi wa Mabaraza ya Miji ambao wanaoajiriwa kwa muda hivi sasa ukimuuliza anakwambia nimejaza mkataba lakini hana, kwenye taasisi za binafsi mikataba hawana. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili naomba sana liangaliwe kwamba kila mmoja awe na mkataba wake.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 15, suala zima la Program ya Uendeshaji wa Uratibu wa Afisi ya Rais, Katiba Sheria na Utumishi wa Umma, kifungu cha 41. Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu

Kifungu cha 41 kinazungumza hivi:

> "Hadi kufikia Machi 2018, ofisi imeendelea kuwa na kiungo muhimu cha shughuli za wizara kisiwani Pemba kwa kuratibu shughuli za kitaifa, kazi za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na kufuatilia masuala ya kiutendaji …"

Mhe. Mwenyekiti, nina sikitiko langu kwamba Baraza lililopita kipindi kama hichi cha bajeti nilizungumzia tena suala hili kuhusu watumishi waliokuwepo Pemba katika Mikoa miwili ya Kaskazini na Kusini. Watumishi hawa kwa kweli waliokuwa hawana usafiri wanapata tabu sana. Watumishi wanafika wakati hukuchukua muda wa kufanya kazi ikawa bado wapo barabarani, kitu ambacho kinarudisha utendaji wa kazi. Watumishi wale wanahitajiwa katika ofisi zao, watu wametoka katika sehemu mbali mbali lakini ukifika utaambiwa mtu huyu hajafika. Nilishauri kuendelea kufanya utaratibu wa kuweka usafiri maalum, basi moja liwekwe Kaskazini, moja kusini na hili linawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Unguja tumeona mabasi yanatoka hapa kuelekea Kaskazini Unguja na wafanyakazi wanapata kufika kwa wakati na kuondoka kwa wakati, kwa nini hatuwezi kufanya hili, katika kitabu hichi sijaona. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anifahamishe kwa nini hadi leo amefikia hatua gani kuhakikisha kwamba usafiri wa wafanyakazi wa Pemba waliokuwa katika mikoa hii miwili ya Kusini na Kaskazini unakuwa wa uhakika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwenye taasisi zinazopata ruzuku serikalini kupitia wizara hii kama vile Wakfu na Mali ya Amana. Afisi hii ni muhimu sana kwa kweli na ina majukumu mazito, nayo inahitaji kuangaliwa sana kama tunavyoona kwamba Ofisi ya Mufti ina taasisi zake kama kule Pemba, lakini hata hapa Ofisi ya Katibu Mtendaji kuhusu suala zima la usafiri, usafiri hawana. Kwa mfano, leo Afisi ya Mufti sehemu ya Katibu Mtendaji sehemu ya Wakfu na Mali ya Amana wana majukumu ya kufuatilia sehemu mbali mbali, leo utakuta Afisi pengine Katibu Mtendaji anayo gari yake moja hakuna nyengine ya kufanyia wafanyaji kazi. Huku anataka kwenda kuangalia mirathi iko wapi na huku kwengine vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika na Pemba hakuna magari yametawanyika, lakini hapa tunaona kwamba tirka 1733 zilifunguliwa na 639 ndizo zilizofanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi, kama ingelikuwa kuna usafiri mimi nadhani ingeongezeka. Hapa niwapongeze kwa juhudi waliyoifanya, lakini ingelikuwa kuna ufasiri basi ingelikuwa kila pahali, kwa sababu madai sasa hivi ya mashamba ya mali mbali mbali za watu waliokufa zinabaki watu hawarithishwi mpaka na wale wanaotaka kurithi anarithiwa tena kutokana na urasimu mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, kupitia Mhe. Waziri namuomba sana suala hili aliangalie katika kuona kwamba wanapatiwa usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Afisi ya Mufti inashughulikia kusajili Misikiti pamoja na Vyuo yaani Madrasa tumeona kwamba Misikiti mbali mbali imejengwa mingi sana lakini na sasa vyuo au madrasa tuseme zimeongezeka. Ukiangalia madrasa za watu wazima akina mama natoa shukurani sana kwamba muelekeo wa leo ni mzuri sana, wameendelea kuwa wengi kwenye madrasa zao lakini hata hivyo na madrasa za watoto wetu zimekuwa nyingi, utaikutia madrasa ina watoto 250 lakini haina hata tundu moja la choo. Kwa hivyo, naiomba Afisi ya Mufti ifanye

utaratibu kuandika andiko la mradi auuze nchini popote pale katika ulimwengu akipata fedha, ili aweze kujenga vyoo mule tuweze kudumisha usafi, leo wanafunzi wale pale wanakuwa ni kero kwa majirani, anayetaka kwenda kujisaidia lazima aende kwa jirani kitu ambacho kwa uwezekano kuweka matundu manne matano katika Madrasa inawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika majimbo yetu tutasaidia na tunaendelea kufanya hivyo lakini na yeye nimuombe kufanya hivyo na yeye nimuombe kufanya hivyo. Pia katika Ofisi hii hii ya Mufti suala zima la kutoa elimu ya kutumia Afisi ya Mufti katika wananchi kupata haki zao badala ya kufanya kienyeji majumbani, wengi wao halafu inatokezea migongano katika hili. Namuomba sana Mhe. Waziri afisi yake hii ichukue hatua kama inaona ushauri huwo unafaa.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la Chuo cha Utawala wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa haraka sana kufanya mabadiliko ya uongozi wa chuo hichi. Kwa kweli chuo hii mimi mwenyewe binafsi nilikuwa napata malalamiko mengi sana, yaani chuo kilikuwa na migogoro na ukosefu wa mambo chungumzima, kulikuwa na ubadhilifu wa fedha unaotumika vibaya, ushirikishwaji mbovu wa walimu na watendaji wengine ambao wapo pale, kitu ambacho kilikuwa kinarudisha *morally* ya kufanya kazi kwa wale walimu pale. Lakini sasa leo amemteua kiongozi wa kusimamia chuo kile, imani yangu kwamba kitakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana na aliyechaguliwa chuo kile pale ajifunze kutokana na makosa ya mwenzake. Kwa kweli, mwenzake pale alikuwa na ukiritimba mwingi sana, kwa hivyo yeye abadilishe na kama hivi sasa tunapata taarifa kwamba chuo kinavuja, asingoje kwamba lazima serikali ije izibe, atafute namna ya kufanya ukarabati huo kwa kiasi anavyoweza.

Mhe. Mwenyekiti, chuo hichi ni muhimu sana kwa serikali yetu, kinatoa elimu mbali mbali na kila kukicha tunaongeza juhudi ili elimu iwe juu zaidi. Lakini, naomba ofisi hii itumie busara kupitia wafanyakazi wake na wao tuwafundishe kule kule waliko bila ya kwenda chuoni waandae utaratibu kama ni semina lakini na kuwafundisha Sheria za Utumishi. Wafanyakazi wengi wahawazijui Sheria za Utumishi, hata haki yake haijui wakati mwengine lakini pia na wajibu wake na hivi ni vitu vinavyokwenda pacha, haki na wajibu.

Mhe. Mwenyekiti, afisi yako ni vyema ichukue busara ya kuwapitia wafanyakazi kuwafundisha namna gani Sheria hizi za Utumishi zinafanya kazi, sio uje uitafute sheria kwa kupewa adhabu tu, leo kwanza ajue wajibu wake na akifanya nini atakuwa amekosa. Naomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mchango wangu uko katika ukurasa wa 25 katika Ofisi ya Mwnasheria Mkuu. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina kazi kubwa sana ya kutuletea miswada hapa na baadae tukaipitisha. Kwa kuwa, katika Baraza letu tukufu la Wawakilishi la Zanzibar tuna Kamati ya Bajeti, ambayo kuwa ni muhimu sana na hadi leo ndio tukafika pahali tukaweza kujadili vitabu hivi kupitia kamati hiyo ya bajeti baada ya kuzipitia, lakini kamati hii haina sheria. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mwanasheria Mkuu afisi yake itayarishe mswada na kuona kwamba ni sheria gani itakayotungwa, ili kuiwezesha Kamati ya Bajeti iweze kufanya kazi zake kwa mujibu wa kisheria. Kwa kweli, hivi sasa ipo tu inatumia kanuni lakini sheria haipo. Lakini katika ofisi hii itakapoleta hivyo itakuwa imesaidia katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Afisi hii kazi yake pamoja inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kukamilisha mapitio ya sheria na sisi hapa Barazani tumepitisha sheria ambazo kuwa zinaanza kutumika, lakini sasa tumeona kuna sheria zinaleta manung'uniko sana kwa wananchi. Sheria hizi zitatukumba hata sisi tuliyokuwemo humu au wale watakaorudi tena makazini kama sisi wengine basi haturudi tena kazini umri umeshapita.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kupitia Mhe. Waziri sheria tuliyoipitisha ya *ZSSF* ya kiinua mgongo kupitia *ZSSF*. Sheria hii ya kubakisha asilimia 40 ya kiinua mgongo zile kupelekwa kwenye pencheni bado ni kero kwa wananchi wengi na tunaonekana kama hatukufanya haki, lakini kwa sababu tumeiyunda sisi tunayo haki ya kuifanyia marekebisho. Sheria hii hii wenzetu imewaweka wakati mgumu kwa baadhi ya nchi kama kule Kenya. Nasema tena Kenya ilifika pahali mfuko kama huu ukaweza kushtakiwa, kwa hiyo tusingoje kufikia hayo katika serikali yetu, huku sheria inalalamikiwa na tumeshaona haifai, ni vyema tuifanyie marekebisho ipasavyo bila ya kuathiri. Kwa kweli, kila mmoja amejipangia malengo yake anapotaka kustaafu, lakini leo unakuta kama alitarajia apate milioni 20 anapata milioni 15. Tulione kama ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Ofisi ya Mdhibiti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nimeona mwaka jana tuliomba sana wafanyakazi waongezwe katika ofisi hii. Kwa kweli, kama walivyosema wenzangu ofisi imepewa wafanyakazi lakini leo wanatolewa, lakini ripoti zinazokuja mbona zinakuja nyuma sana, isingekuwa vizuri kujadili ripoti ya miaka minne nyuma ni sawa sawa na kufukua maiti, ni vyema ripoti raha yake ipite mwaka mmoja tukague aliyefanya makosa aweze kuwajibishwa. Lakini, kesi leo ripoti ambayo kuwa italetwa miaka mitatu nyuma pengie watu wameshastaafu au wameshaondoka kazini au wameshakufa ina maana gani. Kwa hiyo, ripoti iende na wakati na hasa kwa vile serikali inajitahidi kuajiri basi na wao wawatumie wafanyakazi hawa kufanya ukaguzi na ripoti iletwe iweze kukaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana kwa kunipa muda huo na naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, baada ya kupata maelekezo hayo. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar, Waheshimiwa Wajumbe nina mchangiaji mmoja ambaye nitamwita sasa hivi ni Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma. Kwa hivyo, nilikuwa ninaomba kama kuna wachangiaji wengine ambao wanataka kuchangia walete maombi yao.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kuweza kunipa nafasi ya muda mchache kuweza kuchangia yangu ambayo nimejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujaalia kufika katika siku hii ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tukiliwa leo ni mwezi mosi nategemea tutamaliza salama kama ambavyo tumeuwanza. Nichukue fursa hii kuwatakia kheri ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Waislamu wote duniani na wale tuliokuwepo Zanzibar katika mfumo huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuendelea kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, jana nilianza kumshukuru kwa kuweza kutuona vijana kwa

kuweza kutupa nafasi mbali mbali za uongozi na hatimae jana hiyo hiyo nadhani alinisikia aliweza kumteua Mkurugenzi wa Chuo Cha Utawala wa Umma Dkt. Mwinyi Talib Haji, na yeye akiwa ni kijana mwenye nguvu na mwenye busara za uongozi, kwenye hili tunamshukuru sana Rais wetu wa Zanzibar kwa kutuona na kujali. (*makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuwa mchangiaji katika hutuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, michango yangu niende moja kwa moja katika ukurasa wa 21 kwenye kesi ya Mahakama, kwanza niipongeze sekta hii kwa kazi zao nzuri ambazo wanazifanya katika kuleta haki na wajibu katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, tunatambua kwamba changamoto nyingi ambazo zinawakumba watu hawa wa Mahakama ni uhaba wa usafiri lakini ni uchakavu wa majengo ambayo wanafanyia kazi. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, atuwekee mazingira mazuri kwa wafanyakazi wetu hawa, ili tuone kazi zao wanazifanikisha vizuri na kuweza kutendea haki wale ambao wanahitaji haki zao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba katika kesi au katika utafiti ambao tumeufanya walikuwa wanalalamikiwa sana watu wa Mahakama katika kutoa maamuzi na maamuzi yenyewe hasa katika kesi za jinai, ikiwemo kesi za udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, huku kwenye *field* tulikokwenda tumekutana na matatizo na malalamiko mengi yametupiwa Mahakama hasa katika uendeshaji wa kesi za udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, wanyonge wengi wanategemea kwamba Mahakama ndio sehemu yao ambayo watapatia haki, lakini kwa masikitiko makubwa mtu tayari alishadhulumiwa, mtu tayari alishahujumiwa mtoto wake anakwenda Mahakamani lakini haki inadhoroteshwa, inacheleweshwa na hatimae kuikosa kabisa. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana muhimili huu hatuwezi tukauwingilia moja kwa moja, lakini tunawashauri waone utaratibu mzuri wa kuweza kuwasaidia hasa wananchi wake wanyonge ambao wanakwenda hapa kulilia haki zao (*makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa namba 33, Tume ya Utumishi Serikalini. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa usaili wao mpya unaoendelea siku hadi siku katika kutafuta wafanyakazi wapya kwenye hili tunashukuru sana, kwa sababu ili kuwa wakati mkubwa tu walisimamisha na kusema kwamba serikali naitathmini na inaangalia uajiri mpya. Kwa hiyo, kwenye hili tunashukuru lakini tuwashukuru pia kwa kutuwekea tathmini ambayo inaonesha imepanda na imejali sana vijana katika ajira hizi mpya kulingana na mda na wakati na umri ambao walokuwa nao kwenye nafasi za uajiri.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri matangazo wanayoyatoa bado changamoto kwa vijana ambao wanaotaka kuomba nafasi, muda unaotolewa matangazo ni mdogo na siku zinazomalizia matangazo hayo pia ni mdogo, yawezekana ikatolewa tangazo tarehe 01, ukaambiwa tarehe 04 ni mwisho. Kwa hiyo, kwa muda huu naomba na nishauri muda huu uongezwe, ili vijana wenzangu au vijana sisi tuweze kupata muda mzuri wa kuweza kuomba. *(Makofi)*

Lakini kwenye kesi za uajiri namuomba Mhe. Waziri hapa akae na tume uone mnajadiliana vipi kuhusiana na uajiri kuangalia na kuzigawa nafasi hizo kutokana na *geographia*. Mhe. Waziri,

hivi sasa tunatambua kwamba hakuna shamba wala mjini vijana wote wamehamasika katika kutafuta elimu hakuna Kaskazini wala Kusini ambapo vijana bado hawajachangamkia fursa za elimu. Kwa hiyo, kwenye ugawaji wa hizi nafasi tuangalie tusije tukawa tunaangalia sifa tu kwamba sifa hii imetokea wapi na wapi naamini kwenye mikoa mengine pia vijana wanasifa nao wamesoma na pia wameelimika. Kwa hiyo, kwenye kuangalia tusije tukatizama tu mlolongo lakini tuangalie na *geographia* (*makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika kesi hii naomba tuwaangalie watumishi wetu kwenye kesi ya kupatiwa Bima za Afya. Mhe. Mwenyekiti, hii niishauri wizara ione sasa kuwe kuna haja watumishi wetu na wao waweze kuwa na Bima za Afya, ili kuwaondolea usumbufu katika kupata huduma za afya, hili nimeona niliseme hasa hasa katika sekta ya walimu, walimu wanasumbuka, wanahangaika wao na familia zao katika kupata huduma hizi za Afya. Kwa hiyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa aone ushauri huu kwamba unafaida na unaumuhimu wa kuweza kuwafikiria wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa namba 16 kulipozungumziwa Chuo cha Utawala wa Umma, nimeanza kwa kuanza kumpongeza Mkurugenzi ambae ameteuliwa, lakini niipongeze serikali kwa ujumla kwa kuweza kuweka chuo hiki kwa kuweza kuwaandaa vijana wake vizuri katika utendaji wao wa kazi, kwa dhati kabisa niseme kwamba chuo hiki kinatusaidia na mimi mwenyewe nikiwemo kinatupa mafunzo ambayo nahisi yatatowa kwenye *stage* nyengine kwenda sehemu ya pili. *(Makofi)*

Lakini, Mhe. Waziri kama alivyogusia Mhe. Hamza Hassan Juma, tunaambiwa vyuo hivi vimeanza kuwa na mgogoro na kuwa havitambulikani na kuanza kusitishwa usaili wao katika maombi yao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri vijana wanakusikia, wasomi wanakusikia macho yetu yote sasa hivi yako kwako, ili utupe kauli ya kuweza kuona inatupa faraja lakini na hatimae kuwekwa wazi tukaona jambo hili likoje. Mhe. Mwenyekiti, naomba nishauri sana kama kuna mgogoro wowote tukae kitako na *NACTE*, ili tuone tatizo hili linaondokaje na kuweza kuwasadia vijana wetu. (*makofi)*

Suala jengine katika bajeti iliyopita kulikuwa kuna changamoto ya tawi lile ambalo tumelianzisha Pemba, changamoto kubwa ilikuwa hakuna walimu, usafiri na vitu vyengine. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa vile chuo hiki kimeanzishwa Unguja lakini sasa hivi kipo na Pemba basi tuone tatizo au changamoto hizi kwa wenzetu zimetatuka au bado linazidi kutusumbua na kama linatusumbua ufumbuzi wazi ni nini. Hivyo, kwa kuwasaidia vijana na kuwasaidia watumishi wetu naomba ufafanuzi wa mambo hayo, ili tuone tunakwenda sawa.

Baada ya usema hayo Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Mwenyekiti wa Vijana kutoka Kusini Unguja. Sasa naomba nimwite Mhe. Bi Panya Ali Abdalla atafatiwa na Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Salma Mussa Bilal ajiandae.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* ambae ametuwezesha kufika katika siku ya leo ambayo ni siku ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu

atujaalie afya njema tuweze kufunga mwezi huu Mtukufu na Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kuyapata yale yote mazuri aliyoyapanga katika mwezi huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuungana na wenzangu ambao wamechangia hutuba hii, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri, mwenye hikma, mwenye busara ambae katulia katika kazi zake, pia nimshukuru sana kwa uwasilishaji wake mzuri sana (*makofi).*

Lakini pia nimshukuru Naibu Waziri ambae inaonekana anafata nyayo za Waziri wake ametulia yuko makini lakini pia watendaji wote wa ofisi hii nawashukuru sana akiwemo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali nawapongeza sana (*makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu ni mdogo lakini ni vyema nikasema. Nianze mchango wangu katika Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini ambapo Mhe. Mwenyekiti wenzangu wengi wamesema na michango yao mizuri lakini naomba niengezee. Mhe. Mwenyekiti, imeonekana hapa idadi ambayo madrasa 104 zimesajiliwa na misikiti 61, na vyuo vya *Qur-ani* 58 na misikiti 50 ambavyo vimepata kufanyiwa ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niseme hii idadi bado ni ndogo Madrasa tunazo nyingi sana na hata hiyo miskiti bado idadi hii inaonekana ni ndogo tuendelee kufanya kazi hii ya usajili, kwani tukisajili inaonekana ndio ni utambuzi wa kuweza kuzijua madrasa zetu zote ziko ngapi na hata miskiti itakuwa iko mingapi. Jambo, ambalo litapelekea kuondosha ile mirundikano maana sasa hivi kuna mtu anaweza akakaa tu akaamua mimi sasa hivi nafungua tu madrasa yangu nakushanyika tu hapa na wenzangu bila ya utaratibu ambao unatambulikana.

Utaratibu wa kujisajili maana yake unaweza ukapelekea tukawatambua walimu wetu wa vyuo, ambao tumewakabidhi zamana za watoto wetu na hasa ukizingatia hivi sasa kuna mambo kadhaa yanayojitokeza ya udhalilishaji ni vyema madrasa hizi zikaweza kutambuliwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika madrasa hizi ningeomba serikali iweze kuzifanyia utafiti wa kina kwa sababu inaonekana katika madrasa hizi kuna upungufu mkubwa wa vyoo na ukilinganisha kipindi cha hichi cha mvua za masika na katika madrasa kuna watoto wengi. Kwa hiyo, tuone tunaweza kuwasaidia vipi wenzetu hawa ambao watakuwa wamekosa huduma hii ya vyoo na hali wanahudumia watoto wengi katika madrasa zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia mimi niliweza kuchangia kipindi kilichopita kusema jamani misikiti tunayo mingi sana kwa hivi sasa, tungeweza kuelekea upande wa pili wa Madrasa tukaweza kujenga madrasa zilizobora, zilizo nzuri ambazo watoto wetu nao wengepata faraja ya kuweza kusoma mahala pazuri. Jengine pia nilishauri tukawaandaa wanafunzi katika kuwasomesha, ili tuweze kuja kuwa na Maimamu wazuri, kwa sababu miskiti hiyo tunayo mingi lakini utakuja kuta kama hatujaandaa Maimamu wazuri tutakuja kuta ndio Maimamu wanapigana ngumi ni aibu Maimamu kupigana ngumi msikitini, ambapo sisi waumini wao tunawatarajia kwamba muislamu yoyote akipata shida anataka akimbilie kwa imamu au sheikh yoyote, ili aweze kupata fatua ya kutatua tatizo lake, sasa tukiona wao Masheikh wanapigana sisi imani itapungua.

Kwa hiyo, lazima tuweze kuandaa walimu hivi sasa, tuweze kuandaa wanafunzi hivi sasa ambao watakujakuwa Maimamu wetu wazuri ambao wataweza kuja kufundisha katika miskiti yetu lakini hata walimu wazuri ambao wataweza kuja kusomesha katika madrasa zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu pia niende katika wafanyakazi katika taasisi hizi ambazo zimetajwa hapa, katika taasisi hizi kumeweza kiambatanisho hichi kinatuonesha wafanyakazi ambao wameajiriwa lakini kwa upande wa Pemba naona kuna 000 katika taasisi nyingi.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atufahamishe huku hakuna uwakilishi wowote ambao wanafanya kazi hizi, kwa sababu ukenda katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma hapa Unguja wafanyakazi wapo, lakini Pemba inaonekana hakuna. Je, hawa huduma zao wanapata kupitia wapi. Lakini pia, Tume ya Maadili ya Viongozi, pia kunaonekana hapa hakuna watu kule upande wa pili kwa hiyo Mhe. Waziri utakapokuja au Chuo cha Utumishi wa Umma ambacho ni chuo muhimu sana wenzangu sasa hivi wametoka kukisifia. Lakini, kwa upande ule wa Pemba hakuonekani, na kule mimi najua liko tawi. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti utakapokuja hebu utuelekeze vizuri ni kwa nini hapa kunaonekana hakuna watendeaji wanaofanya kazi kule.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwanza kabla ya kusema yote nichukue fursa hii kumpongeza sana sana, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, mama huyu ametulia na yuko vizuri katika utendaji wa kazi zake, lakini niseme kitu mama huyu kama ikiwa kuna vikwazo ambavyo vinamzuia haweze kufanya kazi zake vizuri hata awe mzuri au hodari vipi atashindwa kuonekana uzuri wake kwa sababu ya vizingiti na vikwazo vinavyomkwaza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tangu mimi nimeingia katika Baraza hili kipindi kilichopita tunadai wafanyakazi mama huyu apatiwe wafanyakazi, ili aweze kufanya kazi zake kama inavyostahiki, leo bila ya wafanyakazi ataweza vipi kuripoti na hapa niseme ripoti hizi ambazo zinatufikia maana yake niseme kama hazina maana kwa sababu ripoti ya 2015/2016 ndio inatujia katika mwaka 2017/2018 ripoti hii haina kazi kwa sababu wale ambao tunawalenga kwenda kuwakagua maana yake hao pengine wameshastaafu au wengine Mwenyezi Mungu ameshawahitaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapokwenda kuleta ripoti hii maana yake tutashindwa sasa kuweza kuwabana hawa ambao tunamashaka nao. Kwa maana hiyo, naomba Mhe. Mwenyekiti ripoti hii inavyoeleza mapungufu haya ambayo anayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukosa wafanyakazi mahiri katika ofisi yake ufanisi hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, niseme ufanisi haiwezi ukapatikana kwa sababu hivi sasa na ishara na dalili zipo ambazo tunaziona kama ufanisi haupo kwa sababu ya kukosekana wafanyakazi, ili ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikaweze kufanya kazi vizuri. Hivi sasa miradi ya maendeleo haipati kukaguliwa na miradi hii ndio ambayo inatumia fedha nyingi sana, sasa miradi hii kama haipati ukaguzi kwa wakati wake muafaka hapa ni kupeteza fedha hizi nyingi bila ya mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti tuna miradi mingi mikubwa ya Serikali ambayo tunaiona majengo makubwa mazuri yamejengwa lakini hayana kiwango maana yake hapo fedha imetumika vibaya. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni muhimu sana, ili kazi zetu zende vizuri basi huyu mama lazima tuweze kumpatia wafanyakazi tena wafanyakazi wenye kiwango kizuri cha taaluma, ili aweze kufanya kazi kama vile anavyotarajia.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti ya kamati imetuonesha kuna mashirika ambayo yanakaguliwa lakini ripoti haziji. Sasa, naomba kujua mashirika hayo ni mashirika gani Mhe. Mwenyekiti tutajia ili tuweze kujua, kwa sababu hapa ripoti imetueleza hii ripoti ya mwenyekiti alipoisoma kama kuna mashirika yanakaguliwa lakini hayalete ripoti zake hapa kwa hiyo mashirika haya tuambiwe ni mashirika gani na ni kwa sababu gani hawaleti ripoti ambazo zingeweza kutusaidia sisi katika utendaji mkubwa wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa mdogo lakini naomba niungane na wenzangu wote ambao wameweza kuchangia ripoti hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii na nawaomba wenzangu tumsaidie Mhe. Haroun Ali Suleiman kuiunga mkono ripoti yake hii kwa sababu ni Waziri mmoja ambae ametulia katika wajibu wa shughuli zake za kazi anafanya kazi kwa kujituma ni mweledi mzuri Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Bi Panya Ali Abdalla Mwakilishi nafasi za wanawake kutoka Kaskazini. Sasa, naomba nimuite Mhe. Viwe Khamis Abdalla atafuatiwa na Mhe. Salma Mussa Bilali na Mhe. Machano Othman Saidi ajiandae.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa anavyoitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo aliahidi katika kipindi chake cha kampeni. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Vile vile, nichukue fursa hii nimpongeze Afisa Mdhamini ambae kuwa anafanya kazi zake Pemba. Pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kumteuwa kijana huyu ambae kuwa ni kijana mahiri anaefanya kazi zake kwa kujiamini kuwa Afisa Mdhamini katika Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utawala Bora. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo inipongeze wizara hii kwa kujenga jengo la kisasa Kisiwani Pemba ambalo kuwa litatumika katika Ofisi hii ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria na Utawala Bora. Kwa kweli, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba hawana jengo la kutosha au hawana jengo ambalo lina hadhi na ofisi hii ya Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe Mwenyekiti, nianze mchango wangu na ukurasa wa 11 Progamu ya Usimamizi wa Masuala ya Kidini. Katika ripoti hii ya Mhe. Waziri ametueleza kuwa kama kulikuwa na migogoro 63 ya ndoa. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli sasa hivi migogoro ya ndoa inaengezeka siku hadi siku kutokana na kuwa vijana wetu wanao owana wanakuwa bado ni wadogo hawana taaluma hii ya ndoa. Hivyo, nichukuwe nafasi hii niwapongeze hivi karibuni nilisikia katika vyombo vya habari kutoka Ofisi ya Mufti Mkuu kuwa wataanzisha Chuo Maalum cha Ndoa, ili kabla hujaoa utafika pale utasoma kwa muda wa miezi mitatu baadaye utaaingia katika ndoa ni jambo la faraja sana, kwa sababu vijana wetu hawana taaluma hii ya ndoa na ndio maana wanapooana hawafikia muda mrefu inakuwa wanaachana. Kwa hiyo, talaka zinakuwa zinaongeza siku hadi siku na baadaye husababisha watoto kuwa wanasumbuka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nende kwenye vitendo vya udhalilishaji. Katika mwaka huu wamesema katika kitabu chao hichi kuna kesi mbili ambazo kuwa zimeriporitiwa katika Ofisi ya Mufti, lakini kesi hizi zinakuwa zinaripotiwa mara kwa mara lakini wamesema ni kesi mbili tu ambazo kuwa zimeripotiwa na waweza kuzichukulia hatua. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atuambiye baada ya kuripotiwa kesi hizi hawa walimu wa madrassa bado wanaendelea kusomesha na madrasa haya bado vipo vinaendelea ni hatua gani ambazo kuwa wamezichukua katika kupambana na tatizo hili la udhalilishaji, kwa sababu janga hilo la udhalilishaji hapa Zanzibar linakuwa likiendelea siku hadi siku, na yote haya yanasababishwa na kuto kutolewa hukumu kwa wakati kwa kusingia kuwa kesi nyengine hazina ushahidi sijui wanataka ushahidi gani, wakati mtoto yule alofanayiwa udhalilishaji anasema na ameeleza na mtuhumiwa amemtaja lakini kesi bado tu tunakuwa tunawalea wadhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye majengo ya mahakama. Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Wete hairidhishi na ni bovu kwa sababu jengo lile ni la muda mrefu sana nimuombe Mhe. Waziri aje anieleza katika bajeti yake ya mwaka huu 2018/2019 wamepangaje katika kulifanyia ukarababti jengo lile la Mahakama ya Wete.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Tume ya Utumishi wa Umma Serikalini nichukuwe nafasi hii niwapongeze kwa jitihada zao ambazo kuwa wanazifanya. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hivi sasa tunasikia matangazo mengi ya ajira katika Tume hii ya Utumishi Serikalini. Lakini kuna changamoto katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Afya. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wamekaa wameomba nafasi ya ajira, lakini nafasi hizo zinakuwa zikitolewa mbili mbili wakati skuli zote ya Unguja na Pemba zina matatizo ya walimu pamoja na Wizara ya Afya, vituo vya Wizara ya Afya bado vina changamoto za wafanyakazi, lakini bado Tume ya Utumishi ni kikwazo kikubwa inayokwamisha hizi ajira kutoka Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja katika majumuisho yake atupatie maelezo, ni sababu gani ambazo kuwa zinakwamisha hizi ajira za walimu na ajira madaktari zikawa hazina kipauumbele wana ajiriwa watu wawili wawili, kumi, sita, nane wengine mpaka hufikia kuondoka wakaondoka kwenda kutafuta kazi katika nchi ya jirani, ili waweze kujikimu na maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika Tume ya Utumishi wa Umma kuna changamoto ambayo kuwa inawakabili walimu wetu. Walimu wanakwenda wanasoma tena wajisomesha wenyewe kwa gharama zao, baada ya kumaliza mafunzo yale ya kufuatilia haki zao, basi wanakuwa wanasumbuliwa mpaka walimu wale wanakata tamaa kabisa wakaweza kusamehe wakasema wao wanasubiri rehma za Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Wizara hili pia walishughulikie ili vijana wetu wanondokane na tatizo hili, kwa sababu mwalimu anatoka Tumbatu au Nungwi anakuja kulisikiliza hili anakuwa keshapoteza nauli. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia wizara yake suala hili walishughulikie na waweze kulitatua.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa niaba ya vijana Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Salma Mussa Bilali atafutatiwa na Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kwa kunijaalia mchana huu kuweza kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu na kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nipongeze sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuweza kutuandalia kitabu hichi na leo hii kutuwasilishia katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nisikupotezee muda moja kwa moja niende katika mchango wangu katika ukurasa wa 12 Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Kidini. Mhe. Mwenyekiti, naenda moja kwa moja katika kipengele ya 33 kuhusu udhalilishaji wa walimu wa madrasa.

Mhe. Mwenyekiti, alisema hapa kwamba kitabu chake kinasema vitendo vya udhalilishaji kwa Madrasa za *Qur-ani* vinaripoti mara kwa mara, lakini kwa kipindi hiki kuna kesi mbili zilizoripotiwa. Mhe. Mwenyekit, nadhani pamoja na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na serikali katika kulipiga vita suala hili bado suala hili linaendelea. Katika hili, Mhe. Mwenyekiti, naomba nataka kuuliza hawa walimu ambao wa madrasa ambao tunawategema kama sisi watu ambao hatumo majumbani mwetu saa zote kutwa tunategemea kwamba mwalimu wa madrassa kama ni kimbilio la watoto wetu, lakini kinyume chake sasa walimu wa madrassa wamekuwa ndio wanaowaharibui wa watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wanachukuliwa hatua gani? Je, Ofisi ya Mufti inaendelea kuwaruhusu hawa kuendelea kusoamesha ama vipi?

Mhe. Mwenyekiti, na halafu limetokea suala la udhalilishaji kwa mwalimu wa madrasa katika jimbo lake Mhe. Waziri tarehe 07 mwezi 03 kumetokea kesi ya mwalimu wa madrasa alimbaka

mtoto wa darasa la pili, alimughilibu kwa shilingi mia moja tu, sasa sijiu Mhe. Waziri kama analijua hilo na hatua ya kesi hii imefikia wapi? Kwa kweli, inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba sana Ofisi ya Mufti iendelee kutowa elimu kwa walimu wa madrasa na pia wachunguzwe walimu wote ambao wanajihusisha na masuala haya waondelewe kabisa katika kusomesha watoto wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, halafu nikitoka hapo nakwenda katika ukurusa wa 29 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwanza nataka nichukuwe fursa ya kipee kumpongeza sana mama huyu kwa juhudi zake anazozifanya katika kazi zake mbali mbali anazozifanya katika shughuli za Udhibiti na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto mbali mbali za ucheleweshaji labda wa ripoti, ucheleweshaji wa ukaguzi. Lakini hili linasababishwa Mhe. Waziri katika ofisi yake, kwa sababu suala la upungufu wa wafanyakazi limeshasemewa sana katika Baraza hili, lakini hadi leo bado linaendelea kunakuwa kuna upungufu wa wafanyakazi, bado serikali haija ajiri wafanyakazi wa kutosha na wataalamu katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri achukuwe juhudi za makusudi ili uajiri huo uweze kuajiriwa vijana na wataalamu ambao wataweza kumsaidia *CAG* katika kufanya shughuli zake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika ukurusa wa 31 kifungu G07 Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa. Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nipongeze sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa kwa kazi zake mbali mbali nzuri na jitihada zake mbali mbali amekukuwa akitowa elimu, akihamasisha jamii katika kuona umuhimu wa masuala haya ya vitendo vya kuzuwia rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika kitabu hiki kimesema kwamba ofisi hii ina jumla ya tuhuma 151 ya makosa lakini majadala 139 ndio ambayo yamepelekwa Ofisi ya *DDP*. Mhe. Mwenyekiti, nataja kujua ni kesi ngapi au ni watuhumiwa wangapi ambao wametuhumiwa katika kesi hizi na tayari wameshachukuliwa hatua za kisheria nataka kujua hili, kwa sababu Mkurugenzi anajitahidi anaibua anatoka watuhumiwa wanakwenda lakini tunataka kujua ni wangapi wameshachukuliwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika Ofisi ya *DPP*. Vile vile, naomba pia nimpongeze sana *DPP* kwa juhudi zake na wafanyakazi wake kwa kazi mbali mbali wanazozifanya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nina masikitiko Ofisi ya *DPP* ina kazi kubwa mno, kazi ngumu lakini kuna changamoto unaona kuna changamoto ya wana bajeti isiyo toshekeza mahitaji ya shughuli za undeshaji wa mashtaka. Ofisi ya *DPP* ina kazi ngumu narudia tena kusema ina kazi ngumu kuna wahalifu mbali mbali, kuna majambazi wote *DPP* anatakiwa atowe ushahidi wao sasa leo Ofisi ya *DPP* inakuwa ina upungufu wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri ofisi hii iangaliwe kwa hali ya juu kabisa iangaliwe vizuri kwa upeo waongezewe bajeti, ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Kwa mfano, kuna

ukosefu wa maslahi madogo ya wafanyakazi, kazi yao wanayo fanya ni ngumu leo hii mfanyakazi maslahi yake yanakuwa madogo, mfanyakazi huyo unamsababishia afanye mambo mengine ili angalau aweze kujikimu. Lakini, mfanyakazi huyo huyo kazi yake ngumu lakini maslahi yake madogo leo hii anakuwa na kesi nzito halafu mtuhumiwa anaweza akaenda kumhujumu anakwenda kupiga teke kibanda chake anaweza akamhujumu akamfanya lolote kwa sababu hana uwezo wa kuweza kukidhi maisha yake. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba pia maslahi ya wafanyakazi yatizamwe tena.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia katika hapo halpo Ofisi ya *DPP* kunakosekana jengo la kudumu kwa Ofisi ya Pemba inabidi pamoja na bajeti ndogo wanayopewa lakini hapo hapo wakodi jengo watoe pesa za kodi kwenda kulipia jengo, hivyo naomba pia hilo waliangalie. Mhe. Mwenyekiti, katika vifungu kitabu kikubwa Ofisi ya *DPP* ukiangali uendeshaji wa usimamizi wa kesi za jinai, mwaka uliopita ameidhinishiwa milioni mia tisa na themanini, laki nane na thamanini na moja lakini mwaka huu ameidhinishiwa milioni mia nne na thelathini, hizo za mwaka jana ambazo alikuwa anazipata zilikuwa hazikidhi haja leo mwaka huu amepunguziwa zaidi.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze vizuri kwa nini badala ya kumzidishiwa angalau akaweza kukidhi mahitaji yake, leo hapa amempunguzia, kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti naomba Mhe. Waziri aje anipe maelezo ya kina. Vile vile, kuna mambo mengi tu kuna kesi za jinai usimamizi wa kesi za jinai mwaka jana amepewa milioni mia mbili na sitini na tano mwaka huu amepewa milioni mia moja na ishirini na nane atazifanye kazi hizi *DPP*. Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kwa kina kwa nini ikapungua kwa kiasi hichi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye kiambatisho chake 6(c) hapa alisema kwanza za Ufunguwaji wa Kesi za Mahkama ya Kadhi kesi ambazo zimefunguliwa ni kesi 1249, lakini kesi zilopata maamuzi ni kesi 441 nataka ufafanuzi na hapa kesi zimekuwa nyingi zinalimbikana lakini maamuzi yanachelewa naomba ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikitoka hapo nakwenda kiambatisho 7(c) vile vile kiambatisho 7(c) katika *item* ya likizo bila malipo. Kwa kweli, tukiangalia hapa tutaona kwamba kwa mwaka huu wafanyakazi ambao wapo kwenye likizo bila ya malipo ni watatu tu na ambao wote wako Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, lakini ukiangalia humu katika Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti kuna wafanyakazi kibao ambao wana likizo bila ya malipo na humu kwenye kitabu hawamo, sasa nataka ufafanuzi hawa kwa mwaka huu tu au kwa jumla.

Ukiangali Wizara ya Afya wapo humu ndani ukiangalia Wizara ya Mawasiliano wamo humu ndani ukiangalia Uwezeshaji tumo, ukiangalia *SUZA* wamo lakini katika kitabu kimesema wafanyakazi watatu tu ndio wamo kwenye likizo bila ya malipo katika viambatisho vyake.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nyengine kuna *item* hii ya kupandishwa cheo katika kitabu hiki Mhe. Waziri kuwa anasema katika serikali nzima hii wamepandishwa vyeo watu hawa watatu na wote Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nataka ufafanuzi hivyo serikali nzima hakuna wafanyakazi ambao wana vigezo vya kupandishwa cheo isipokuwa watatu na wote Wizara Fedha na Mipango nataka anipe maelezo na hapo.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona nichangie tu hayo madogo kwa leo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Lakini, Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anijibu vizuri maswali yangu niliomuliza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Salma Mussa Bilal kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said kama muda utaruhusu nitampa Mhe. Ali Khamis Bakar.

Mhe. Machano Othman Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na afya lakini pia niwashukuru na kuwatakia kheri ya Ramadhan Watanzania Waislamu na wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wakuu wa Mamlaka mbali mbali ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum hivyo nitatoa mchango mdogo tu kwa ajili ya kuimarisha au kuboresha michango ya Waheshimiwa Wajumbe ambayo wametoa hapo mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumza kwanza kuomba tu kwamba kutokana na mwenendo wa baadhi ya mambo ambayo yapo yanaendelea kwa taasisi ambazo zinasimamiwa na wizara hii. Kwa hivyo, niombe ushirikiano uzidishwe zaidi katika taasisi za Polisi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu na Mahakama zetu katika kukabiliana na tatizo au wimbi la udhalilishaji wanawake na watoto. Ukiiangalia taasisi moja moja inafanya kazi vizuri kwa upande wake, lakini nahisi ule mshikamano wa pamoja ndio ambao unahitajika vizuri zaidi.

Tumewasikia baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe hapa wakizungumzia masuala ya uendeshaji wa kesi za udhalilishaji na hatma ya kesi hiyo, tumewasikia wengine wakizungumzia ushahidi jinsi unavyopotea katika mazingira ambayo hayana uhakika. Vile vile, asubuhi nilimsikia Mhe. Simai Mohamed Said alizungumzia mpaka na gazeti jinsi alivyozungumzia kama ile kesi ya Pemba anasuuliwa baada ya kukamatwa na madawa ya kulevya. Kwa hiyo, nadhani kwamba taasisi zetu hizi tatu, mbili ambazo ziko katika wizara hii *DPP* na Mahakama na moja ambayo iko nje ya Polisi wanatakiwa waendelee kuwa na ushirikiano wa karibu. Tukifanya mashirikiano mazuri haya mambo yanaweza yakakaa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili nizipongeze taasisi ambazo ziko chini ya wizara hii, bahati nzuri wizara hii ina taasisi nyingi ambazo zinajitegemea. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kipindi ambacho tumefanya kazi nao wamefanya kazi nzuri, nampongeza Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu na watendaji wao wote wametusaidia sana katika kutafsiri sheria, lakini pia kuelewa malengo ya serikali kupitia mkono wa sheria.

Pia, nimpongeze na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali ndugu Ibrahim Mzee Mohamed ni mzoefu wa sheria watendaji wake wote wamejitahidi sana kuona kwamba kesi kwa zile za jinai zinakwenda vizuri. Nimpongeze zaidi kwamba yeye alishirikiana vizuri sana na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Mhe. Jaji Mshibe Ali Bakar, kurekebisha ile Sheria ya Watoto na hizi za Adhabu. Kwa hivyo, sheria zile mkono wao ulikuwemo na walifanya kazi nzuri, nina hakika ni kazi ya kutukuka katika taratibu zetu hizi za kisheria. *(Makofi)*

Vile vile, niwapongeze na kule kwenye Tume ya Maadili ingawa bado kule Mhe. Waziri naomba sana Tume ya Maadili ya Viongozi ile ni taasisi muhimu na kubwa, kama ile *sub vote* yao bado basi napigia tena msumari wapewe fungu lao wale wajitegemee, ili shughuli zao zisiweze kuingiziwa mkono mkono na wizara au na mtu mwengine. Maana yake mpaka waziri kule unaambiwa upeleke fomu ya maadili, Katibu Mkuu anatakiwa apeleke fomu yake ya maadili. Sasa kama hawa watu ambao wanataka kukuchunguzeni halafu fedha hamuwapi au mpaka aje kwenu aombe basi itakuwa shida kidogo katika utendaji wa kazi zao. Kwa hivyo, naomba taasisi ile ya Tume ya Viongozi wa Maadili wawe na fungu lao ili waweze kufanya kazi kwa uhuru na kwa amani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba ukiachia Taasisi hii ya Tume ya Maadili pia naomba sana wafikirie kutoa fungu kwa Ofisi ya Mufti. Mhe. Mwenyekiti, kwa Zanzibar Ofisi hii ya Mufti ina majukumu mazito na ya muda mrefu. Kwa hivyo, kuwa na fungu lao ni jambo la muhimu na lalazima katika kuendesha shughuli ambazo wanataka kuzitolea fat-wa katika ofisi ile.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la mahujaji, hapa nitazungumzia kwa ujumla katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kwa kweli, suala la mahujaji wa Zanzibar wanapata tabu sana wanapokwenda kuhiji Makka. Kwa mfano, kama tutakumbuka mwaka jana kulitokezea migogoro ya kifedha na kuna taasisi zikaambiwa zinadaiwa, na kukawa na tishio la mahujaji kutokupokelewa. Sasa sijui Mhe. Waziri akija atatwambia mpaka sasa imefikiaje lile wazo la kuwa na *account* ya mahujaji kutoka Zanzibar mbali na kuwa na *account* ya mahujaji wa Tanzania Bara mbali, ili kunusuru na kuweka heshima Zanzibar katika masuala haya ya mahujaji.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana najua kwamba Waheshimiwa Mawaziri tulishazugumza lakini kwa sababu hili Baraza lazima na hapa tutilie nguvu. Yapo madai na malalamiko, kuna madai na malalamiko Wakfu wanadai kwamba kuna eneo katika Jimbo la Mfenesini, Shehia ya Mfenesini kuna eneo la Wakfu lakini wananchi ambao wanaishi pale kwa zaidi ya miaka 50 wanasema eneo lile walipewa tangu enzi ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kwa hivyo, bado naomba ule mgogoro tuutatue na Mhe. Waziri naomba kama tulivyokubaliana tufanye safari ya kwenda katika eneo lile mimi na watendaji wako tukaangalie tuweze kupata ufumbuzi wa suala lile ambalo linawaweka roho juu viongozi na wananchi wa eneo lile ambalo wanaishi katika Shehia ya Mfenesini.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, mazingira ya Mahakama yetu Kuu ambayo yapo sasa yamekuwa madogo kwa sababu pale sasa hivi Mjini harakati nyingi hakuna maegesho, njia ile karibu na Ikulu. Kwa hivyo, wameamua kujenga Mahakama Kuu Tunguu kiwanja kizuri wamepewa, na kwa bahati nzuri katika bajeti hii lipo

fungu limewekwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa Mahakama Kuu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kwa miaka hii mitatu ya kibajeti 2018/2019 na 2019/2020 na 2020/2021 wajitahidi lile jengo la Mahakama Kuu liwe limemaliza ikiwezekana tukimaliza awamu hii ya uongozi wa nchi yetu basi na Mahakama Kuu tuwe na jengo jipya katika uendeshaji wa utoaji haki kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia mwaka huu tunaomaliza wa kifedha wizara yake kupitia Mahakama ilifanya kazi nzuri Mwanakwerekwe, wameibadilisha sana Mahakama ya Mwanakwerekwe baada ya matengenezo. Tulikwenda kuitembelea tumeona zamani ilikuwa ofisi zao ni ndogo hawawezi kukaa wafanyakazi, sasa hivi wana ofisi nzuri, lakini kwa bahati mbaya siku ya ufunguzi Mhe. Waziri alisahau kuwaalika kamati.

Lakini tulikuwa tunaomba kwamba pale pembeni ya Mahakama ya Mwanakwerekwe pana kama kimkahawa na tuliulizia tukaambiwa cha Wizara ya Maji. Kwa kweli mkahawa ule haufai pale eneo lile halistahiki kuwa ni eneo la Mahakama, ili Mahakama ikaweza kufanya kazi zake kwa uzuri zaidi na kwa nafasi zaidi. Kwa hivyo, nimuombe basi azugumze na watu wa Wizara ya Maji, ili lile eneo wakabidhiwe Mahakama kwa sababu Mahakama ni ya serikali, taasisi ya maji ni ya serikali wapewe pale wafanya shughuli zao za kimahakama ambazo zitakuwa nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie *ZAECA* Taasisi yetu hii Kupambana na Rushwa. Katika maelezo yao wamesema watajenga makao makuu ni jambo jema lina maana sana katika kuimarisha taasisi. Lakini pia kuwapa mafunzo wafanyakazi wao waweze kufanya kazi kwa weledi na kiutaalamu, wakati mwengine wanafanya kazi za kubakabaka tu lakini hawana uweledi. Kwa hivyo, lazima wawe na uweledi na utaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la msingi ukienda kuangalia ofisi zao za Pemba *ZAECA*, Pemba nzima wana gari moja wanafanya kazi za kuwatafuta watu wahujumu kwa vespa, na Masika kama haya nafikiri wahujumu kule ndio wanacheza kwa sababu hawafatwi tena, hawezi kufanya kazi ya serikali kwa vespa kwenda kumtafuta muhujumu hiyo ni hatari. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba uwafikirie sana wale wafanyakazi wa taasisi hii kisiwani Pemba, ili waweze kupata usafiri wa maana na wa kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni la Tume ya Utumishi Serikalini na kwa bahati nzuri mahitaji ya ajira ni mengi kuliko uwezo wa serikali, lakini ziko baadhi ya taasisi za serikali ambazo wafanyakazi wao wameshastaafu zinakaa kuliko miaka miwili hazijaajiri tena nafasi zile. Kwa mfano, unaweza kwenda Wizara ya Afya unamkuta Daktari Dhamana wa Kituo analalamika anasema tupo watu watatu, *orderly* sasa anapiga sindano mtu, *orderly* amekuwa mfamasia anatoa dawa, kwa sababu wafanyakazi ambao wanastahiki hawajaajiriwa tena. Kwa hivyo, niomba angalau kwa zile nafasi ambao watu wanastaafu basi kuwe na mpango wa kuzijaza haraka kwa sababu mishahara ya wafanyakazi wale ipo katika *payroll* ya serikali. Sasa kwa nini mfanyakazi anastaafu nafasi inakaa wazi kwa mwaka mmoja au miezi sita hivi zile pesa zinakwenda wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba wafanyakazi na lazima mnajua kwamba mwaka huu wa fedha katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunatarajia wafanyakazi 2,500 watastaafu kwa hivyo lazima mjiandae kuona kwamba mnarejesha wafanyakazi alau kwa kiwango kile ambacho wamestaafu. Kwanza kupunguza tatizo la ajira kwa wananchi lakini pia kuwapunguzia mzigo

wale wafanyakazi ambao sasa wanakuwa na kazi kubwa wengine na ngumu. Kwa hivyo, lazima hili lifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia huu utaratibu wa wafanyakazi wa serikali kwanza kuanza wanapewa siku ya mafunzo kupitia Chuo cha *IPA* nafikiri. Ni mzuri kama kuna utaratibu mzuri maana yake tuliwahi kusikia kwamba kabla ya kuthibitishwa kazini lazima kwanza uwe umekwende kwenye *fresh course* fulani unafanyika huu au uko katika maelezo tu. Hivi wafanyakazi wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kweli wanapata hizi kozi, kama hawapati inakuwaje?

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hii ni changamoto tu mimi sikutaka kuchangia sana kwa sababu mambo mengi ya wizara hii nimeyapitia na nimeyaona na nimeridhika kwamba wanafanyakazi nzuri. Lakini kwa hayo niliyozungumza nafikiria mtaongezea kwa yale ambayo tumeshazungumza ili kuweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nikushukuru lakini pia niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza kwamba bajeti hii nayo ni muhimu sana tuijadili kwa kuwasaidia maneno ya kuweka sawa, lakini hatimae kesho tukijaaliwa na Mwenyezi Mungu penye uhai na uzima tuwapitishie fungu lao lote hili ili waende wakafanye kazi. Nakushukuru tena Mhe. Waziri, nakushukuru Naibu Waziri, nakushukuru Mwanasheria Mkuu nawashukuru na wale wengine ambao kwa vyeo vyao hawakuingia Barazani wanasikiliza katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, nilimtaja mchangiaji Mhe. Ali Khamis Bakar lakini kutokana na muda hauturuhusu kumpa nafasi hiyo, kwa hiyo atakuwa mchangiaji wetu wa mwanzo kesho tukijaaliwa na atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif na wengine wapo hapa chini. Tuna wachangiaji karibu watatu.

Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa michango yenu lakini pia nimshukuru waziri pamoja na watendaji wake wote katika kuwasilisha hotuba yao na naomba niwatakie Ramadhani njema na niakhirishe kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 18/05/2018 saa 3:00 asubuhi)